ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.

14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34 .Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg. Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nne – Tarehe 2 Aprili 2012

(Kikao Kilianza Saa. 3.00) Asubuh

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka hati hizi zilitajwa kuwasilishwa Barazani siku ya Ijumaa, lakini ikawa kuna matatizo katika mswada Mhe. Mwanasheria Mkuu akaomba arudi na Kamati ya Katiba Sheria na Utawala kupitia upya, kiasi cha kwamba sasa hata hizo hati zenyewe zinabadilika. Kwa sababu hiyo ndio utakuta kwamba imerejeshwa tena hapa kwamba hati hizi sasa ziwasilishwe upya.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani yake.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani yake.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Vipimo na Tathmini ya Elimu Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Vipimo na Tathmini ya elimu Zanzibar na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 50

Ahadi za Viongozi Wakuu

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:

Viongozi wetu Wakuu wamekuwa wakitoa ahadi mbali mbali katika kutembelea miradi ya ujenzi wa skuli zinazojengwa kwa nguvu za wananchi. Je, ni kwa nini ahadi hizo za Viongozi wetu wakuu hazitekelezwi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa wamekuwa wakitoa ahadi mbali mbali ikiwemo miradi ya Skuli zinazojengwa kwa nguvu za wananchi, ahadi hizo zinazotolewa katika ziara zao za kukutana na wananchi pamoja na kutembelea miradi mbali mbali ya maendeleo. Aidha ahadi hizo zinakuwa zipo zinazoweza kutekelezwa katika kipindi cha muda mfupi na zipo zinazohitaji muda kwa utekelezaji wake.

Mhe. Spika, Viongozi wetu wote huwa wanatekeleza ahadi zao na endapo ahadi za viongozi zimechelewa kutekelezwa ni vyema wahusika kukumbushia kwa vile viongozi hao nao ni binaadamu na wana majukumu mengi ya kitaifa. Si nia ya viongozi kutokutekeleza ahadi ambazo wamezitoa wenyewe.

Mhe, Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa ahadi hizi zimekuwa zikichelewa Je, kuna utaratibu gani wa serikali imekuwa ikijiwekea ili kutimiza ahadi hizo za viongozi wetu wakuu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Sasa tumeweka utaratibu wa kuwa na waratibu katika kila Wilaya, kwa hivyo tumetoa maagizo maalum kwamba viongozi wetu hawa wa kitaifa wanapotembelea katika maeneo Mbali Mbali ya Wilayani, Majimbo na Mikoa waratibu wetu wanatakiwa wafuate ziara hizo kwa nia Mbali Mbali ya kujua wanachozungumza waheshimiwa viongozi wetu, lakini pia waweze kuelewa ahadi wanazozitoa ili wazilete wizarani na baada ya hapo tuweze kuwakumbushia Waheshimiwa viongozi wetu.
Lakini pia niwajibu kwa makatibu wa viongozi wetu kuwakumbushia viongozi wetu wakuu hawa kwenye zile ahadi zao, lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba wao nao binaadam na sote binaadamu inaweza kutokea kuhafilika kutokana na majukumu Mbali Mbali, kwa hivyo jambo la msingi zaidi ni mwenye ahadi yake pia kukumbushia kwa katibu muhusika kwa kiaongozi husika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa viongozi wetu wakuu hutembelea sehemu Mbali Mbali na kutoa ahadi, ninavyoelewa baadhi ya ahadi wakuu zetu wanazitoa na wanazipeleka kunako husika. Lakini Je, mbona kuna minong'ono na saa nyengine aho viongozi wa Mikoa au Wilaya huwa hawazipeleki mpaka ziara nyengine ya wakuu wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, sana ulikuwa ushauri wa Mhe Asha Bakar. Nataka nimuhakikishie kwamba tutalifuatilia jambo hili, ili katika mikao na wilaya ahadi hizo za viongozi wakuu zinapotolewa basi wasimamie na watekeleze mara moja. Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya atakayeshindwa kufanya hivyo, basi hatua za kinidhamu zitachukuliwa.

Mhe. Moh'd Haji Khalid: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Hawa viongozi wetu wakuu wa kitaifa hutoa ahadi na mara nyengine hufikia kuondoka madarakani bila ahadi hizo kutekelezwa.

Je, kama ahadi hizo hazikutekelezwa na viongozi wetu waliopita, sasa kuna mpango gani ahadi hizo kutekelezwa kwa kuwa zimetolewa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, serikail ni endelevu, anapoondoka kiongozi mmoja basi kiongozi anayefuata ana wajibu wa kutekeleza ahadi ambazo zimetolewa.

Nam. 133

Mbwa wa Kunusa Madawa ya Kulevya

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali kwa kuchukua juhudi za kupiga vita madawa ya kulevya kupitia hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutafuta mbwa wa kunusia madawa hayo. Hata hivyo, kwa muda mrefu sasa mbwa huyo amefariki na bado Serikali haijamtafuta mbwa mwengine kwa kazi hiyo.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea kutotafutwa kwa mbwa mwengine.
(b) Je, kwa kiasi gani kukosekana kwa mbwa huyo kunazorotesha juhudi za kupambana na tatizo la madawa ya kulevya nchini.
(c) Je, ni lini Serikali itatafuta mbwa mwengine kwa ajili ya kuendeleza juhudi za kupambana na madawa ya kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu :-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.
133 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo :-

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kueleza kwamba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, haihusiki moja kwa moja katika utekelezaji wa baadhi ya shughuli zikiwemo za kuwakamata watuhumiwa wanaohusika na dawa za kulevya. Shughuli za kumtafuta na hatimae kumuweka Mbwa wa kunusa dawa za kulevya zinatekelezwa na Jeshi la Polisi.

Hata hivyo, Mhe. Spika, kutokana na mawasiliano tuliyofanya na Jeshi la Polisi kuhusiana na Mbwa wa kunusa dawa za kulevya, naomba nichukue fursa hii kutoa majibu kwa swali lake nambari 133 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo :-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba ilichukua muda mrefu kupatikana mbwa mwengine baada ya mbwa aliekuwa akitumiwa kunusa dawa za kulevya kufariki. Hata hivyo, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba tayari sasa mbwa mmoja ameshapatikana na tayari ameaza kutumika kwa doria za kawaida.

(b) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba mbwa hutumika katika upekuzi wa dawa za kulevya, pia kuna njia nyengine nyingi zinazoweza kutumika katika kupata taarifa ya usafirishaji, wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevya. Ingawaje kukosekana kwa mbwa huyu kuliathiri kwa kiasi fulani juhudi za kupambana na dawa za kulevya, lakini bado kuna njia nyengine nyingi zinazoweza kutumika katika kupata taarifa kwa ajili ya wasafirishaji, wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevya.

(c) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali kwamba sasa mbwa mmoja ameshapatikana na muda mfupi ujao atakuwa ameshamaliza mafunzo na kuwa tayari kuanza kutumika. Aidha, mbwa wengine wawili (2) tayari wameshatolewa kutumika kwa Jeshi la Polisi Zanzibar, juhudi zinafanywa ili kuwasafirisha kutoka Moshi kuja Zanzibar.

Nam. 60

Uingizaji wa Kuku Kutoka Nje

Mhe. Ashura Sharif Ali - Aliuliza :-

Katika jitihada za kuwakwamua wananchi kiuchumi Serikali inawashajiisha wananchi kufanya shughuli mbali mbali zikiwemo kilimo na ufugaji.

(a) Je, Mhe. Waziri kuruhusiwa uingizwaji wa bidhaa ya kuku wa nyama katika nchi yetu huoni ni kuwavunja moyo wafugaji wetu wazalendo pamoja na kuwapunguzia au kuwakosesha soko la kuuza bidhaa hiyo.

(b) Je, kuku hawa wanaoletwa wana usalama gani kwa afya ya mlaji na je, kuna utofauti gani na kuku wanaofugwa hapa nchini kwetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi) – Alijibu :-

Mhe. Spika, kwa idhini yako kabla ya kujibu swali la Mhe. Mjumbe, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, mahitaji ya soko la kuku wa nyama ndani ya nchi yetu ni tani 520, uzalishaji wa ndani wa kuku wa nyama kutokana na wafugaji wetu ni tani 162, hivyo ni dhahiri kwamba kuna nakisi ya tani 358.

Vile vile naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba serikali ya Tanzania ilisaini mkataba wa biashara wa WTO, ambao unaruhusu biashara huria duniani. Kwa hivyo kuku wa nyama kutoka nchi za nje wanaruhusiwa kuletwa ndani ya nchi yetu ili kukidhi mahitaji ya walaji wanaohitajia, lakini vile vile kuku wa nyama wanaozalishwa hapa kwetu wanaweza kusafirishwa nje ya nchi yetu kwa ajili ya biashara.
Mhe Spika**,** kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Uingizwaji wa kuku wa nyama haupo kwa madhumuni ya kuwavunja moyo wafuagji wetu, bali ni hatua ambayo itaweza kuwaongezea ari ya ushindani kwa kuweza kuzalisha zaidi na kwa ubora ikiwa tu patajengwa madhingira ya kuwasaidia wafugaji wetu kukabilaana na ulimwengu huu wa ushindani wa kibiashara ambao hatuwezi kuuepuka. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaangalia uwezekano wa jinsi ya kuweza kuwasaidia wafugaji wetu kwa kuwapatia nafuu katika bei ya chakula cha kuku, vifaa na dawa. Vile vile inaendeleza juhudi za kuwapa ushauri wa kitaalam ili waweze kuzalisha kuku wenye nyama na wenye ubora ili kukabiliana na ushindani wa soko.

b) Mhe. Spika, kwa mujibu wa ripoti ya bodi ya chakula dawa na vipodozi Zanzibar ambayo ndio yenye mamlaka ya kuruhusu uingizaji wa bidhaa hiyo na pia kuangalia usalama wa chakula, kuku hawa wa nyama ni salama kwa afya ya mlaji

   Mhe. Spika, tafauti kubwa iliyopo kati ya kuku wetu hawa wa nyama na wale wanaotoka nje ni kwamba kuku wanaotoka nje wamefikia viwango vya ubora kwa uzito na lishe, kutokana na kuwa na viwango vizuri wa vifaranga vyenyewe, lishe bora na pia mazingira mazuri na mtunzo bora katika ukuaji wa kuku hao.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa mahitaji ya nchi yetu kwa nyama ni tani 520 na wafugaji wetu wanazalisha tani 162 kwa nini Wizara yako haifanyi juhudi ya kuweza kuwakomboa wafugaji hawa nao wakaweza kuzalisha kwa asilimia hiyo kwa kukidhi mahitaji ya nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi) Mhe. Spika, naomba kumuarifu Mhe. Ashura Sharif Ali kwamba utafiti wa kina umefanyika juu ya suala hili, ni nia ya serikali kuwaendeleza wafugaji wetu ili waweze kuzalisha zaidi sio kwa ajili ya kukidhi soko la ndani, lakini vile vile kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi. Jitihada hizo zinafanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuangalia kwanza kuweza

kupata vifaranga ambavyo vina ubora kuweza kuzuia Maradhi kutokana na jinsi ya kuwafuga kuku hawa. Lakini vile vile kuhakikisha kuwa lishe wanayopatiwa ni ile ambayo imetimiza ubora ambao umetakiwa kwa ajili ya kuku wale kukua na kuweza kutimiza kiwango ambacho baadhi ya watumiaji wa soko la Zanzíbar wanawahitajia.

Mhe. Spika, masoko ya utalii ndio zaidi wanaotumia kuku wale wanaotoka nje kwa sababu ndio wanaotaka wa kiwango kile na hawa wa kwetu wengi wanatumika kwa soko la humu humu visiwani kwa ajili ya matumizi yetu wenyewe.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri katika kulitatua tatizo hili alilieleza Baraza lako tukufu kwamba tayari ameshatiliana mkataba na wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza mifugo hii ya kuku ili kuondoa tatizo hili. Sasa napenda kumuuliza Mhe. Waziri je, muwekezaji huyo ameshawekeza na kama bado ni lini hasa atawekeza hiyo biashara.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi) Mhe. Spika, sijui Mhe. Mwakilishi majibu hayo ameyapata wapi maana yake sikuyatoa katika majibu yangu.

Mhe. Spika: Nadhani kama kuna muwekezaji ameomba lijibu tu hata kama halikutoka kwenye majibu yako.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi) Mhe. Spika, naomba suala hilo nijibu kwa maandishi kwa kua data hizo sina hapa mkononi.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kua Zanzíbar wakazi wake wengi karibuni asilimia 99 ni waislam na kwa kua kuku hawa wanatoka pengine sio nchi za kiislam,

Je, Serikali inawahakikishia vipi kuhusu uhalali wa kuku hao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi) Mhe. Spika, kuku hawa wanaoletwa hapa Zanzibar wamechinjwa kihalali na kuna jopo la mashekhe ambalo ndilo linatoa *certificate* huko Brazil, kuhakikisha kwamba kuku hao wamechinjwa kwa njia ya kiislam.

Lakini vile vile hapa kwetu pia nafikiri kama Mhe. Mwakilishi hajasikia tayari pia hata vyombo vyetu vya ndani vinavyohusika na masuala haya, nafikiri tumemsikia Ndugu Soraga akitoa uthibitisho huo kwamba kuku hawa ni halali kuliwa na wasilam, kuku hawa hawaji kwetu tu wanakwenda katika nchi za kiarabu zote ambazo nazo kuna waislam wengi na wanawapokea kwa sababu wamethibitishwa kwamba wamechinjwa kihalali.

Nam. 70

Umuhimu wa Masjala

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-

Kama tunavyofahamu Masjala ndio roho ya Wizara kwa kuhifadhi nyaraka na mara nyingi wafanyakazi wa sehemu hii huonekana ndio wa mwisho. Kama tunavyofahamu katika Wizara kuna Masjala mbili ya Siri na Bayana na muda mrefu sana ukitilia maanani Masjala ya Siri, Masjala ya Bayana inaweza kufanyakazi kwa mwezi mzima lakini Masjala ya Siri inaweza kupokea barua moja kwa mwezi.

(a) Je, Mhe. Waziri unaweza ukatueleza ni vigezo gani vilivyochukuliwa hata ikawa mfanyakazi wa Masjala ya Siri anapandishwa daraja na kuachwa wafanyakazi wa Masjala ya Bayana.

(b) Ni sababu zipi za msingi zilizomfanya mfanyakazi huyo wa Masjala ya siri kuongezewa mshahara.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya sijamjibu suala hilo naomba kutoa maelezo ya msingi yanayohusiana na suala hilo, kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wafanyakazi wa masjala ya siri na masjala ya bayana wanapata mafunzo ya aina moja ikiwa ni pamoja na utunzaji wa siri za Serikali, Ofisi yangu kwa kutumia chuo chake cha Utawala wa Umma inaendelea kutoa mafunzo mbali mbali kwa watumishi wa masjala, yakiwemo ya utunzaji bora wa kumbu kumbu za kiofisi kupitia idara ya nyaraka na kumbu kumbu za taifa na kitengo cha usalama katika utumishi wa umma yaani GSO.

Katika utekelezaji huo masjala ya bayana husimamia taarifa za mawasiliano kwa njia ya maandishi ambayo yapo bayana, wakati masjala ya siri inasimamia mambo ambayo ni ya siri na nyeti kwa mawasiliano ya kiofisi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kama nilivyokwisha kusema kabla sina taarifa ya mfanyazi wa masjala ya siri kuongezwa mshahara kwa utaratibu wa kupandishwa daraja, kama hoja ni mabadiliko tu ya mshahara haya yalifanyika kwa wafanyakazi wote wa utumishi wa umma, kwa kutumia vigezo vya taaluma, uzoefu na dhamana walizonazo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuweza kuuliza suala la nyongeza kama ifuatavyo:

a) Pamoja na majibu mazuri lakini Je, Mhe. Waziri anaweza kutwambia ni chuo gani ambacho hao watu wa masjala wamepita.

b) Ni wangapi mpaka sasa hivi ambao wamepata mafunzo hao watu wa masjala.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Vyuo vingi vinavyohusika na masuala ya kutunza kumbu kumbu, lakini ni wangapi ambao wamepata mafunzo hii kwa sababu karibu Ofisi zote zina watumishi ambao wamepata mafunzo ya kutunza kumbu kumbu kwa hivyo hilo naomba anipe muda nifanye utafiti, au kuwasiliana na Wizara mbali mbali ili kujua kila taasisi ina watumishi wangapi ambao wamepata mafunzo haya ya kutunza kumbu kumbu.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nitamuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo.
Atakubaliana nami Mhe.Waziri kwamba mambo yote ya serikali ni siri ingawa kuna siri ambazo hazitakiwi mtu mwengine azione. Lakini neno serikali ni “siri kali”, atakubaliana nami kwamba barua zozote zile iwe za bayana na za siri kwamba kitu chochote cha serikali ni siri.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe.Spika, kwanza nataka niseme Mhe. Mwakilishi, hiyo taminoloji ya “siri kali” haiko rasmi. Kwa hiyo naomba ibakie kama alivyokwisha kuisema, maana yake yeye anaelewa hivyo.

Lakini nataka nikubaliane na yeye kwamba, shughuli zote za serikali ni siri kwa maana zinamuhusu yule ambaye anastahiki kuzijua, na zipo shughuli nyengine za serikali zinakuwa ni siri kweli kweli. Kwa hiyo nataka nitoe wito katika kujibu swali hili kwamba, wafanyakazi wote wa Masjala za Umma wanastahiki kutunza siri za ofisi zao. Kwa sababu shughuli hizi zinakuwa ni shughuli za kiserikali na zinakuwa zinawapasa wale tu ambao wanatakiwa wazijue.

Nam. 30
Vikundi vya Wajasiriamali

Mhe. Kazija Khamis Kona - Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali inahimiza wananchi wake kuwa wajikusanye vikundi ili inapopata msaada, wapatiwe kwa vikundi na wanalazimika wana vikundi wavisajili vikundi vyao.

Je, Mhe. Waziri ni gharama ya kiasi gani inayotolewa kwa kupatiwa huo usajili.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 38 kama ifuatavyo. Mhe.Spika, ni kweli serikali inahimiza wananchi wajikusanye, waunde na wasajili vikundi vyao ili vitambulike rasmi kwa kurahisisha kuwapa huduma mbali mbali za kitaalamu.

Mhe.Spika, wizara yangu inahusika na usajili wa vikundi vya kiuchumi ambavyo wanachama wake wamekubali kuvisajili kama vyama vya ushirika. Sheria ya Ushirika Nam. 4 ya mwaka 1986, kifungu nambari 43 (1) kinaruhusu kutoza ada mbali mbali kwa vyama vya ushirika, ikiwemo ada ya usajili.

Aidha, kifungu Na. 41 (1) cha Sheria hiyo, kinampa mamlaka Waziri anayeshughulikia masuala ya ushirika kuandaa kanuni zitazosaidia utekelezaji wa masuala mbali mbali yaliyomo kwenye sheria hiyo. Kwa mujibu wa kanuni, ada ya usajili kwa chama cha ushirika cha msingi chenye wanachama 20 ni Sh. 30,000/= tu.

Mhe.Kazija Khamis Kombo: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe.Spika, namuuliza Mhe. Waziri hii takwimu aliyoitoa ni tofauti na takwimu tunayopewa na malalamiko na wananchi wetu. Je, Mhe. Waziri kwa kuwa ushahidi huu upo tofauti ya takwimu unayoitoa wewe na wanayoitoa wananchi ambao wanaojikusanya katika vikundi, ikiwa ushahidi huo utaletewa uko tayari kuufatilia na kuufanyia kazi ipasavyo.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, taarifa ambazo nimezitoa hapa ni za uhakika kwenye chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi. Na kama kuna ada nyengine zinatozwa za ziada ambazo ni kinyume na haya niliyoyasema sio tu aniletee kwa ushahidi, lakini pia nitachukua hatua kwa hai maafisa wanaofanya hivyo.
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi hii kuweza kumuuliza Mheshimiwa swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali la (a) na (b).

(a) Hiyo ada tunaomba utwambie ni kiasi gani mpaka kufika pahali ukaweza kupata usajili.

(b) Tunaomba utwambie hivi sasa hivi Zanzibar ina vikundi vingapi vilivyosajiliwa kihalali vya Ushirika.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwenye jibu langu nilisema kwamba:-

(a) Ada ya kikundi cha ushirika ni Sh. 30,000/= tu.

(b) Idadi ya vikundi ambavyo tumevisajili sasa hivi siwezi kutoa *figure* hizo, kwa sababu tumeanza utafiti kwa Mkoa wa Mjini Magharibi. Na katika Mkoa wa Mjini Magharibi vikundi ambavyo tumevikuta ambavyo vipo hai vyama vya Ushirika ni 2671. Natarajia Ishallah tutakapomaliza zoezi hili lote basi Inshallah Mheshimiwa nitamtayarishia vizuri kwa kila Mkoa nimletee ili zimsaidie kwa kumbukumbu zake za baadae.

Nam. 24

Jumba la Kulelea Watoto Forodhani

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza:

Mhe. Waziri, siku ya ufunguzi wa Bustani ya Forodhani, aliyekuwa Rais wa Zanzibar Dk. Amani A. Karume aliahidi kuwa ataagiza Wizara yako kulifanyia matengenezo jengo la Watoto Mayatima hapo Forodhani kuwa ni *(MUSEUM FOR MARITIME FOR EAST AFRICAN),* ambapo Makumbusho hayo yangeliweza kusaidia kuitangaza Zanzibar kwa kuzidi kuwavutia watalii na watafiti ili kuongeza ajira na mapato kwa nchi yetu.

(a) Mhe. Waziri, Je, taarifa hiyo unayo.
(b) Kama Wizara yako inayo taarifa hiyo Je, mmechukua juhudi gani kulitekekeza suala hilo.
(c) Je, Wizara yako inawaambia nini wananchi kuhusu jengo hilo la Watoto yatima hapo Forodhani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:
Mhe. Spika naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, taarifa hiyo ipo.

b) Mhe. Spika, juhudi iliyochukuliwa hadi hivi sasa katika kulitekeleza suala hilo, ni kufuatilia ubadilishwaji wa umiliki kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kuwa chini ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Jengo hilo la zamani la Watoto yatima ambao kwa hivi sasa wamehamishiwa katika jengo lao jipya hapo Mazizini. Pia matayarisho ya ramani za awali zilikwisha wasilishwa mamlaka na kutolewa marekebisho kwa usahihishwaji.

c) Mhe. Spika, wizara yangu bado imo mbioni kutafuta fedha ama kuwasiliana na mfadhili wa kulijenga, pamoja na kugharamia uanzishwaji wa Makumbusho hayo yatakayojulikana kama *"MUSEUM FOR MARITIME FOR EAST AFRICA* kwa vile gharama za uanzishaji wa Makumbusho unahitaji fedha nyingi.

Mhe.Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura naomba nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri wa Maji Ardhi, Makaazi na Nishati kama hivi ifuatavyo:-

Mhe.Spika, kwanza nashukuru sana kusikia jawabu la Mhe. Waziri kwamba Wizara yake taarifa hii wanayo na wamo katika jitihada za kuifanyia kazi. Jengo lile sasa hivi lilokuwa la Watoto Forodhani, tunajua sasa hivi kuna muwekezaji pale ameanzisha Mkahawa.

(a) Kwa kuwa sasa hivi wao wamesema wameshalifanyia michoro jengo lile na wanatafuta hizo fedha. Je, katika kulifanyia hiyo michoro yule muwekezaji ataendelea kuwepo au vipi. Lakini muwekezaji yule kama alikuwa ana mkataba ulikuwa ni mkataba wa muda gani.

(b) Na je, katika huo ujenzi utakapopata ufadhili, huo mkataba utavunjwa, na kama utavunjwa serikali itaingia hasara kiasi gani.

(c) Kwa kuwa Jumuia ya *Agakhan Foundation* wao walikwisha kuonesha nia ya kuweza kuiboresha ile nyumba ili iwe *Museum for Maritime for East Africa,* Je Wizara yako iko tayari kushirikiriana na jumuia ya Agakhan ili kuweza kuwakabidhi mradi huu kwa kuweza kuukamilisha kwa haraka. Hasa kwa kusema kwamba serikali ule mradi utakuwa wa fedha nyingi, serikali itakuwa haina fedha za kutosha kwa kipindi hichi.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika,

(a) Ni kweli kwamba jumba lile sasa limekuwa linaendeshwa Mkahawa na anayeendesha mkahawa kakodi kwa mkataba maalum. Lakini azma ya kulifanya jengo lile kuwa *museum* iko pale pale. Hatua za kufikia huko zinachukuliwa, wakati utakapofika mkataba ule utafutwa kwa makubaliano na kama kuna fidia ya kulipa italipwa.

(b) Hii hasara kiasi gani kama mkataba huo ukifutwa. Kwa sasa ni vigumu kuisema hasara ni kiasi gani. Lakini tutazungumza na wahusika na kwa kuwa agizo hili lilitoka kwa Rais Mstaafu, tutazungumza na Rais Mstaafu vile vile katika kushirikiana kupatana na yule mwenye mkataba wa kukodi hoteli ili tufikie makubaliano yaliyo muafaka.

(c) Maritime Museum ni Museum ambayo inahitaji utaalamu wa kutosha, inahitaji utulivu na inahitaji fedha. Kama *Maritime Museum* hii alitwambia Mhe. Rais Mstaafu kwamba hii ijengwe kwa ajili ya Wazanzibari wenyewe. Sisi katika ufuatiliaji wetu ni kutafutwa kwa yeyote yule ambaye ataweze kutusaidia ama kifedha au kitaaluma ili tuweze kuijenga hii *museum*. Kama *Agakhan Foundation* watakubali maana walikataa na walijitoa katika miradi yote inayohudumiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na ule mradi wa *fronts wall*. Kwa hivyo kama watakubali kurudi tutawaweka katika ushindani na wale wengine watakaotokea, na tutamchagua mmoja wapo ambaye tutahakikisha atatusaidia kwa kutufanyia kazi nzuri zaidi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Katika majibu yake amesema serikali iko tayari kutekeleza mkataba iwapo wenzetu wa Agakhan watakubali, kwa sababu wamejitoa kwenye mikataba ya miradi mingi.

(a) Je, anaweza Mhe. Waziri akatwambia ni sababu zipi ambazo zilipelekea Shirika la Agakhan kujitoa kwenye miradi ya Zanzibar.

(b) Mhe. Waziri katika jibu lake la nyongeza amesema kwamba sehemu ya jengo hilo licha ya kuwepo agizo la Rais Mstaafu, lakini wao kama Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, waliamua kulikodisha, ni hatua nzuri ya maendeleo. Anaweza akatwambia ni nani aliyekodi jengo hilo.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika,

(a) Sababu zilizomfanya *Agakhan Foundation* ajitoe, mimi kwa kweli sizijui. Lakini ametuandikia rasmi kwamba amejitoa katika mradi huu, amejitoa katika mradi huu na amejitoa katika mradi huu. Sababu zilimzomfanya ajitoe kwa bahati mbaya sana hakutuandikia alipotuandikia najitoa katika miradi hiyo.

(b) Aliyekodi jengo hilo nitamuandikia kwa maandishi.

Mhe.Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza nina swali (a) na (b).

Mhe.Spika, katika majibu yake Mhe. Waziri alisema kuna Mkahawa pale umekodishwa.

(a) Nilikuwa nataka kujua gharama za ukodishwaji ni kiasi gani analipa mtu huyu.
(b) Na mkataba wa ukodishwaji ni wa muda gani.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, masuala haya ya (a) na (b) nitayajibu kwa pamoja na nitayajibu kwa maandishi muda si mrefu kuanzia sasa.

Nam. 40

Uendelezaji wa Majengo ya Taasisi ya Sayansi Mbweni

Mhe. Rashid Seif Suleiman (Kny: Mhe. Hija Hassan Hija) - Aliuliza:

Mhe. Spika, tokea kuanzishwa kwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia hapo Mbweni nini kimefanyika kuendeleza majengo ya taasisi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu;
Mhe. Spika**,** naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 39 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, tangu kuanzishwa kwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume mwaka 2009, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ilianzisha mradi wa uimarishaji wa elimu ya ufundi. Madhumuni ya mradi huo ni kuimarisha masomo ya ufundi katika Skuli ya Sekondari ya Kengeja na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume kwa ajili ya kufanya ukarabati wa majengo na ununuzi wa vifaa na zana za kufundishia masomo ya Sayansi na Teknolojia pamoja na Ufundi.
Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, jumla ya T.Shs110,000,000/= zilipatikana na kati ya hizo TShs. 50,000,000/= zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa ukuta unaozunguka Taasisi kwa ajili ya kulilinda eneo la taasisi lisivamiwe, matengenezo ya vyoo vya dakhalia ya wanaume na ununuzi wa vitabu. Katika mwaka 2011/2012, jumla ya T.Shs 100,000,000/= zimepatikana hadi sasa katika mradi huu na kati ya fedha hizo TShs. 70,000,000/= zimetumika kwa kazi za kuendeleza ujenzi wa ukuta, vifaa vya kufundishia, vyoo vya dakhalia ya wanawake na ununuzi wa vifaa vya karakana.

Mhe.Spika, katika mpango wa muda wa kati, taasisi inakusudia kufanya upanuzi na ukarabati wa majengo na ujenzi wa vyumba vya kompyuta na maktaba kupitia mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Nakushukuru sana Mhe.Spika.

Nam. 81

Ujenzi wa Viwanda vya Kusindika Samaki Zanzibar

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Kwa kuwa jamii ya wavuvi katika Visiwa vya Unguja na Pemba imekuwa ikijishughulisha na kazi ya uvuvi kwa muda mrefu bila ya kuwa na soko la uhakika, na hivyo kukosa bei nzuri ya samaki wao.

(a) Mhe. Spika, ni lini serikali itatimiza azma ya muda mrefu ya kuhakikisha viwanda vya kusindika samaki vinajengwa katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

(b) Mhe. Spika, kwa kuwa viwanda hivyo bado havijajengwa, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi kwa kuwapatia vifaa vya kuhifadhia samaki, hatua itakayosaidia wavuvi hao kutouza samaki wao kwa bei ya chini kwa kuepuka samaki hao kuharibika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe.Spika, azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wanawekeza katika sekta ya viwanda hasa vile vinavyotumia malighafi inayopatikana hapa nchini, na kutoa kama samaki kwa lengo la kutoa ajira kwa wingi kwa wananchi na hasa vijana.

Mhe.Spika, katika kutekeleza azma hiyo nzuri, kazi kubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ni kuweka misingi ya kisera na vivutio kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji. Uwekezaji wenyewe hufanywa na sekta binafsi. Kwa upande wa uwekezaji katika viwanda, imebainika kuwepo kwa vivutio hafifu kuvutia uwekezaji. Hivi sasa Serikali inaendelea na kuifanyia mapitio sera ya Maendeleo ya Viwanda ili kuimarisha vivutio na kuweka mazingira bora zaidi ya kisera.

Baada ya utangulizi huo Mhe.Spika, sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa upande wa uwekezaji katika sekta ya uvuvi, naomba kukiri kuwa bado utekelezaji wake ni mdogo, licha ya hatua mbali mbali zilizochukuliwa na Serikali za kuhamisha uwekezaji katika eneo hilo. Hata hivyo, kwa kipindi kirefu serikali imekuwa ikitoa leseni za uvuvi wa Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing)* ili kuweza kuongeza mapato yake wakati juhudi za kuwakaribisha wawekezaji katika eneo hilo zinaendelezwa. Juhudi hizo zinafanywa kwa mashirikiano na Wizara ya Uvuvi na Mali Asili, Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi yaani (ZIPA), pamoja na Wizara iliyopewa jukumu la kusimamia masuala ya Maliasili.

(b) Mhe. Spika, ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kuhifadhia samaki pamoja na nyenzo za kisasa za kuvulia, ni miongoni mwa changamoto zinazowakabili wavuvi wa hapa Zanzibar. Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo kupitia miradi wanayoifadhili kama *MACEMP, UNDP, Join Program No 5* imekuwa ikitoa vifaa mbali mbali vya kuhifadhia samaki kama (*Deep Freezers)* kwa baadhi ya wavuvi wa maeneo ya Nungwi na Kizimkazi, kwa ajili ya kuhifadhia samaki wakati wa dharura ili kuepuka uharibifu.

Mhe.Spika, kuhusiana na suala zima la soko la samaki naomba kumtoa wasi wasi Mhe. Mjumbe. Kwa sasa hali ya Soko la Samaki limeongezeka kutokana na hali ya bei ya samaki kuwa juu katika masoko yote ya Unguja na Pemba. Mhe.Spika, kwa mfano bei ya samaki aina ya nguru, ndoaro, jodari, pweza, ngisi, kamba na kaa ziko juu sana kutokana na kuongezeka kwa hoteli za Kitalii hapa nchini.

Mhe.Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Viwanda na masoko naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:
Mheshimiwa kwa kuwa inapofika wakati wa msimu, wavuvi huvua samaki wengi, na wakauza katika masoko yanayohusika, na inapotokea kuwa hawajamaliza na kuenda katika masoko ya dharura ya mitaani, kwa hapa Unguja wanatumia sehemu ya Mikunguni na kwa Pemba hutumia sehemu ya Machomane.
Je, ni lini serikali kupitia Wizara yako itafikiria angalau kujenga viwanda vya barafu ili kupata kuhifadhi samaki hao na kufika kwa mlaji wakiwa salama.

Mhe.Naibu Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nimesema kwamba suala la biashara ya samaki ni miongoni mwa biashara ambayo inaipa changamoto sana serikali kupitia Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko. Nikasema kwamba Wizara ipo kupitia na kuandaa sera ambayo pamoja na masuala mengine katika viwanda itashughulika na masuala ya kuanzisha viwanda ambavyo malighafi inapatikana hapa hapa Zanzibar ikiwemo samaki.

Sasa ningemuomba Mhe.Mwakilishi atupe muda kwa sababu suala hili linafanyiwa kazi na Ishallah atapata taarifa yake.

Mhe.Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Spika,naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, mara baada ya kuingia kwa Serikali ya Awamu ya Saba, kulitolewa taarifa ya kuwepo kwa Kampuni ya *Tawasul* kutoka Falme za Kiarabu ambayo ilieleza azma ya kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na kujenga kiwanda cha kusindika samaki. Mradi ambao ulizungumzwa sana, wakiwemo na viongozi wetu wakuu wa kitaifa, mradi huo hausikiki tena hivi sasa.

Je, nini kimekwamisha utekelezaji wa mradi huo wa Tawasul katika kujenga kiwanda cha kusindika samaki na kuanzishwa kwa Bahari Kuu Zanzibar.

(b) Katika majibu yake Mhe. Waziri amezungumzia moja ya sababu zinazokwamisha uwekezaji katika sekta hii ni kukosekana kwa vivutio vya kutosha kwa wawekezaji wa viwanda vya aina hii. Je, anaweza kulieleza Baraza, ni vikwazo vipi au vivutio gani vimekosekana vinavyopelekea kukosekana kwa miradi kama hiyo hapa Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe.Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, Ni dhahiri kwamba katika uwanzishwaji wa viwanda panahitajika umeme wa uhakika. Kwa hivyo kutokana na tatizo hilo ambalo bado tunalifanyia kazi ndani ya serikali, si rahisi kuanzishwa viwanda. Na naamini ni

moja ya sababu ambayo muwekezaji huyu imemfanya asitishe azma yake ya kuja kuwekeza kampuni yake ya kusindika samaki hapa nchini.

Lakini Mhe. Spika, nimesema tena kwamba sera ya kuanzisha viwanda Wizara tunaifanyia kazi na kwa sababu sio suala la siku moja au mbili, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi waipe muda Wizara basi kwa sababu kunatakiwa kufanywe mapitio ya masuala mengi.

Lakini kubwa zaidi Mhe.Spika, ni hii changamoto ya umeme wa uhakika kwa sababu kuja kujenga kiwanda halafu ikawa umeme haupatikani, umeme ni wa mgao itakuwa hata huyo muwekezaji faida aliyoitegemea itakuwa haipati.

Nam. 45

Ujenzi wa Njia

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:

Ni lini serikali itaijenga njia ya Chake Chake – Mkoani na Chake Chake – Wete kupitia Ziwani.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 kama ifuatavyo:-

Kuhusu barabara ya Chake Chake-Mkoani.

Wizara kwa sasa hivi, haina mpango wa kuijenga barabara ya Chake Chake-Mkoani kwa vile barabara hii ilifanyiwa matengenezo makubwa katika mwaka 2002 kwa msaada wa *World Bank.* Ujenzi huu uligawika sehemu mbili, kilomita 7 kutoka Mkoani hadi Mtuhaliwa kulikuwa na *up grading number one* ambayo iliigharimu *World Bank* na serikali jumla ya shilingi bilioni 2.1. Kutoka Mtuhaliwa mpaka Chake Chake urefu wa kilomita 23 ulifanyiwa *over laying* kwa gharama ya shilingi bilioni 7. Kwa hivyo, kwa barabara ya Mkoani-Chake Chake kwa sasa hivi haiko katika mpango wa ujenzi mwengine. Lakini barabara hii kama zilivyo barabara nyengine zinazotumika zinafanyiwa matengenezo kila mahali ambapo panataka kufanyiwa utunzaji wa barabara hiyo.

Kuhusu barabara ya Chake Chake – Wete kupitia Ziwani.

Mhe. Spika, barabara hii ni miongoni mwa barabara zinazofadhiliwa na Benki ya *BADEA*, na *SAUDI FUND* ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ujenzi wa barabara ya Chake Chake - Wete kupitia Ziwani umewekwa katika awamu ya pili ya mradi wa barabara tatu za Kaskazini – Pemba ambao unajumuisha pamoja na barabara ya Wete - Konde na Wete – Gando na barabara hii ya Wete-Chake Chake. Mhe. Spika, nifafanue vizuri kwamba tunaposema Wete-Chake Chake kwa barabara hii tunakusudia ni Wete hadi Meli tano.

Mhe. Spika, hivi sasa mradi huu wa barabara tatu unajengwa kwa kutumia awamu ya kwanza ya ujenzi wa barabara hizo unaendelea kwa barabara ya Wete – Konde, na Wete – Gando na barabara ya Wete – Chake baada ya kumalizika *phase* hii ya kwanza matumaini yetu ni kwamba endapo fedha zitapatikana tutajenga barabara ya Wete- Chake Chake kwa kupitia Ziwani.

Mhe.Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifutavyo:

a) Kwa kuwa katika jibu lake amekiri kwamba hakuna mpango wa matengenezo, au ujenzi wa njia ya Chake Chake - Mkoani, lakini kutokana na harakati zinazoongezeka na gari kuongezeka na njia ni nyembamba ilivyo. Haoni kwamba umefika wakati sasa kwa wizara yake kufanya utaratibu, hasa kutokana na hiyo *master plan* yao waliyonayo kuona kwamba barabara ile sasa inakwenda kwa usalama.

b) Je, kwa nini akamalizia Meli tano na Chake Chake hatujafika.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika mpango wetu mkuu wa usafiri Zanzibar, ni kwamba barabara zote zinazotoka Mijini ama kwenda mashamba au mji na mji zimo katika mpango mkuu, ambao ni utanuzi wa barabara hizi kufuatana na kiwango cha sasa cha *traffic*, na kwa taarifa ya Baraza hili ni kwamba, mpango huo tumeanza na hapa Unguja kuna barabara 7 zenye urefu wa kilomita 70, na tarehe 7 au 8 wiki ya pili ya mwezi huu, upembuzi yakinifu wa mradi huu kwa Unguja barabara 7 utakuwa umekamilika, na utakabidhiwa rasmi serikalini na mshauri. Baada ya kupata ufadhili wa mradi huo hapa Unguja tutaelekea Pemba kufanya *study* kama hiyo, *study* hii ya hapa ilifadhiliwa na *World Bank* pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, mpango huu umo katika mpango mkuu wa usafirishaji Zanzibar.

Mhe. Spika, kuhusu barabara ya Wete-Chake Chake ikaishia Meli tano, ni kwa sababu hii barabara hii ni kwa awamu, na kama nilivyosema Chake Chake na Wete ni miji miwili ambayo shughuli zake zinakaribiana. Kwa hivyo, ikaonekana kwamba kwa fedha ambazo zinaombwa, tusingeweza kujenga kutoka Chake Chake mpaka Wete, lakini tungeweza kujenga kutoka Wete mpaka Meli tano, ni sababu hiyo tu. Pia awamu ya pili ya barabara hiyo ni kuiombea fedha kutoka Meli tano hadi Chake Chake. Kwa hivyo, mpango wa kufika Chake Chake kutoka Wete upo, lakini tunakwenda kwa awamu kutokana na maombi ya fedha na ambapo Benki wame-*respond*.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika kujibu swali Nam. 45 alisema kuwa barabara ya Wete –Chake Chake hadi Meli tano itatengenezwa na kampuni ambayo inashughulikia barabara ya Konde-Wete na Gando – Wete. Lakini kwa sababu kampuni hii imeanza zamani kutengeneza barabara hizi na mpaka leo hawajafika popote.

a) Je, tunafikiria ni mwaka gani itakuwa wamemaliza barabara hizi mbili na kuanza hapo Wete kuelekea huko Chake Chake.

b) Ni kuwa tuliilalamikia kampuni hii kutokana na kwamba kazi zake zilikuwa haziridhishi, na Mhe. Waziri akasema atalifuatilia na kutoa jibu, kwa sababu hiyo je leo anatupa jibu gani kuhusu kampuni hii.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kampuni ambayo tulitiliana saini kujenga barabara tatu ni *MECCO (Mwananchi Engeneering Construction Company)*, awamu ya kwanza ya mradi huu ni barabara mbili za Wete-Gando na Wete – Konde. Baada ya kumaliza awamu hii, ndipo ambapo tungeweza kupata fedha za kumalizia barabara ya awamu ya pili ya Wete –Chake Chake kwa maana ya Wete –Meli tano. Mhe. Spika, *contractor* huyu hivi sasa anaendelea na ujenzi wa barabara mbili awamu ya kwanza, barabara ya Wete-Gando na Wete – Chake Chake.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa mkataba tarehe 31 Januari, 2012 mradi ule wa barabara mbili uwe umekamilika, lakini mradi ule wa barabara mbili Wete-Gando na Wete – Konde ungekamilika tu, kama masharti ya mkataba yangetimizwa asilimia 100 kwa pande zote. Mhe. Spika, sasa hivi barabara ya Wete-Gando utekelezaji wa mradi ni asilimia 26, Wete – Konde ni asilimia 37. Mhe. Spika, nataja viwango hivi makusudi mtakuta kwamba asilimia kubwa imebaki na muda wa ujenzi umekwisha matatizo yafuatayo:-

1. Mhe. Spika, hadi sasa serikali tumeshindwa kulipa fidia kwa nyumba zilizovunjwa ili kumpa mjenzi nafasi ya kujenga. Hii ni kutokana na uwezo wenyewe wa serikali, pia nikiri kwamba kila serikali inapopata fedha basi wanalipa fidia katika mradi huu.

2. Mhe. Spika, jengine ni kuchelewa mno kwa *BADEA* na *SAUDI FUND* katika kulipa fedha kwa mjenzi, tumekuwa tukifuatilia mara kwa mara lakini kama unavyojua hizi Benki ni za Kiarabu, na wao vile vile wana sababu zao, sitaki niseme sababu zipi lakini wakati mwengine inaweza ikalipwa *certificate*. Kwa mfano, mwezi wa Januari, lakini *certificate* hiyo mpaka kukamilika pengine fedha zikapatikana Mei au Juni. Kwa hivyo, nasema haya ni mambo ambayo mimi siwezi kueleza undani wake, lakini pia na yeye mjenzi ana mapungufu yake. Tatizo la mapungufu ya mjenzi ni kwamba unapowaambia hili, yeye anakuoneshea kidole na wewe hili. Kwa hivyo, tumefika mahali ambapo sasa hivi Wizara ya Fedha wenyewe inatufuatilia sio kwa e-mail tena *physical* kwenda Benki ya *BADEA* pamoja na *SAUDI FUND* ku-*negotiate* namna ambavyo mradi huu wa barabara mbili hizi wapi umefikia.

Mhe. Spika, ni imani yetu kwamba huenda tatizo hili likakwamuka, mjenzi akalipwa fedha, *certificate* zake tatu ambazo hajalipwa, na serikali ikavuta wakapata pesa halafu tukaendelea na kazi. Sitaki kusema zaidi lakini nasema kwamba, kwa mradi huu matatizo ambayo yamejitokeza zaidi ni katika ulipaji wa fedha kuliko kitu chengine chochote.

Mhe. Spika, mradi huu unaojengwa na *MECCO* ingewezekana kabisa kwamba *MECCO* akaendelea na mradi huu huu wa Wete-Meli tano. Lakini baada ya walipaji kuona matatizo yaliopo wakasema hapana, huu mradi umeshamalizika, kwa hiyo mradi wa Wete- Meli tano tutaifanya ni *project* mpya. Mhe. Spika, wamesema kwamba wao watasaidia lakini hawajaandika kwa maandishi kwa hivyo bado mradi huu wa Wete-Meli tano kwa maana ya jina la mradi, nao

vile vile ukawa hautajengwa mpaka pale tutakapopata *commitment* na *funding* ya hawa hawa, ambao wamefadhili barabara ya Wete-Gando na Wete-Konde.

Nam. 166

Kukosekana Mahkama na Mahabusu za Watoto Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ripoti ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora ya mwaka 2007/2008, imesema haki za watoto zimekuwa zikivunjwa Zanzibar, kwa kukosekana Mahkama na Mahabusu za Watoto, kinyume na misingi ya haki za binaadamu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahabusu za Watoto na kuondoa tatizo la kuchanganywa na watu wazima katika Vyuo vya Mafunzo na Vituo vya Polisi.

(b) Wizara ina mpango gani wa kuanzisha Mahkama za Watoto na Mahabusu ili kuepusha uvunjaji wa haki za watoto Zanzibar.

(c) Kwa kuwa Serikali imepitisha Sheria ya Kulinda Haki za Watoto Zanzibar, na lini Mahkama za Watoto zitaanzishwa Unguja na Pemba.

Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 166 lenye kifungu (a), (b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza sikubaliani na ripoti ya haki za binaadamu ya mwaka 2007-2008, ambayo ripoti hiyo inasema kwamba haki za watoto zinavunjwa kwa kutokuwepo Mahkama za Watoto. Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria zetu Mahakama za Watoto zipo kwa muda mrefu sana, na zinaendelea kufanya kazi zake katika kila Mkoa. Kwa mujibu wa sheria Nam. 6 ya mwaka 2011 kifungu cha 18 Mwenyekiti wa Mahakama hiyo ni Hakimu wa Mkoa akiwa na wajumbe wengine wasiopungua wawili, ambao watachaguliwa na Mhe. Jaji Mkuu kama ilivyoainishwa katika kifungu Nam. 18 (4) cha sheria hiyo. Kwa maana hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijavunja haki za binaadamu kwa watoto kwa sababu Mahakama za Watoto zipo kisheria.

Mhe. Spika, suala la mahabusu za watoto halimo katika mamlaka ya wizara yangu, Vyuo vya Mafunzo kwa ujumla vipo chini ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar, inajua umuhimu wa kuwatenganisha watoto na watu wazima ndani ya gereza au ndani ya Chuo cha Mafunzo au wakiwa katika mahabusu, ndio maana basi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar, imechukua hatua maalumu za kuhakikisha kuwa watoto wanatenganishwa na watu wazima wakiwa mahabusu au gerezani. Wakati serikali ikitambua hayo, inajitahidi kutafuta ufumbuzi wa kudumu katika suala hili, hivi sasa serikali imeshapata eneo kubwa hapo Hanyengwa Mchana ambalo limeshapimwa na kufanyiwa michoro ya ujenzi wa Chuo cha Mafunzo. Mhe. Spika, katika ujenzi huu suala hilo limezingatiwa na watoto watakuwa na sehemu yao tofauti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri ambayo hayafanani na suala langu nililomuuliza, hivi karibuni tumepitisha sheria ya kuwalinda watoto. Je, sheria hiyo itaanza lini kufanya kazi pamoja na Mahakama za Watoto.

Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu ni kuwa sheria Nam.6 ya mwaka 2011 ambayo ni sheria ya watoto imeshaanza kufanya kazi zamani, na ndio hii iliyoanzisha hizo Mahakama za Watoto, na sheria hii ndio iliyofuta sheria nyengine kwa mfano sheria Cap. Nam. 55, Cap. Nam. 58, Cap. Nam. 59 ambazo nazo zilikuwa zinaanzisha Mahakama za Watoto. Kwa hivyo, sheria hii imeshaanza kufanya kazi Mhe.Spika.

Mhe.Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe.Spika, Mhe. Waziri amesema kuwa Mahakama za Watoto zipo.

Je, Mhe. Waziri Mahakama hizo zipo wapi na mpaka hivi sasa kuna kesi ngapi ambazo zimeanza kuhukumiwa.

Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kila Mkoa kwa mujibu wa sheria Nam. 6 ya mwaka 2011 ina Mahakama ya Watoto na Mwenyekiti wa Mahakama hii ni Hakimu wa Mkoa, na kwa mujibu wa sheria hii, Jaji Mkuu ana uwezo wa kuteua watu wawili zaidi kuingia katika Mahakama hiyo, na watu hao inategemea hasa wale watu ambao wanasaikolojia ya kitoto, watu ambao ni *probation officer*s.

Kwa hivyo, hao wanateuliwa na Jaji Mkuu kuingia katika Mahakama za Watoto. Kwa hivyo, jibu lake Mhe. Spika, ni kwamba kila Mkoa Mahakama za Watoto zipo, kesi ngapi siwezi kujua kwa sababu inategemea katika Mkoa ule mtoto kama kafanya kosa atapelekwa Mahakamani. Kwa hivyo, kama anataka kujua ni kesi ngapi itabidi nimfanyie utafiti na nimpe kwa Zanzibar nzima.

Nam. 87

Ujenzi wa Kiwanja Kipya cha Michezo

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Moh'd Shein katika hotuba zake mbali Mbale, amekuwa akiahidi Serikali kujenga Kiwanja kipya cha kisasa cha michezo, na pia kuufanyia matengenezo makubwa Uwanja wa Mnazi mmoja.

(a) Je, ahadi hiyo ya Rais wa Zanzibar utekelezaji wake utaanza lini.

(b) Je, ni lini Kiwanja hicho cha Kisasa cha Michezo kitajengwa pamoja na Kiwanja cha Mnazi mmoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tayari imeshaanza kutekeleza ahadi hiyo. Kiwanja hicho kipya kitajengwa kwenye eneo la Uwanja wa Mao Tse Tung kwa kuubadilisha uwanja huo na kuwa wa kisasa utakaotumika kwa michezo mbali mbali.

b) Mhe. Spika, hivi sasa kazi ya uchoraji wa ramani ya kiwanja hicho inafanywa na wataalamu wetu, na mara baada ya kukamilika juhudi za kutafuta fedha za ujenzi kupitia njia mbali mbali zitakazochukuliwa ili kutimiza azma iliyokusudiwa.

Mhe.Spika, kuhusu ujenzi wa Kiwanja cha Mnazi Mmoja, shughuli hizo zinafanywa na Baraza la Manispaa la Mji wa Zanzibar ambalo ndilo lenye mamlaka la uwanja huo. Kwa mujibu wa Baraza hilo ujenzi huo unategemea kuanza mara baada ya kupata fedha za kutosha. Mazungumzo ya awali ya kupata mshiriki wa kusaidia yameshafanywa ambapo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China inatarajiwa kusaidia.

Kuhusu Mradi wa kutengeneza bwawa na ujenzi wa marekebisho ya mitaro ya Kiwanja cha Mnazi Mmoja umepangwa rasmi kufanyika mwishoni mwa mwaka huu wa bajeti ya mwaka 2011/2012, chini ya mradi wa kuendeleza miji ya Zanzibar (*Zanzibar Urban Service Project*). Mradi huu tayari umekubaliwa na hatua zote muhimu zimekamilika, na upo katika hatua za utekelezaji, mradi uliopo chini ya Manispaa ya Zanzibar.

Mhe.Spika, awamu ya kwanza ya utekelezaji utafanyika katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kwa mujibu wa vipengele vilivyokubalika na Benki ya Dunia, ambao ndio wafadhili. Mradi huu ni endelevu kwa miaka mitano (5) ambapo kazi zake zitafanyika na kutekelezwa ndani ya miaka mitano sio mwaka mmoja. Hivyo, ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni endelevu katika kipindi cha mwaka 2011 – 2015.

Mhe.Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe.Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na kuweza kuleta matumaini mapya kwa wana michezo Zanzibar, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, hivi sasa hali ya viwanja vyetu ni vibovu hasa katika maeneo ya Unguja. Je, wizara haioni kwamba ipo haja ya kuweka nyasi bandia katika Uwanja wa Amaan ili kuondoa tatizo la viwanja hapa Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Mwakilishi kwa kuuliza maswali haya kwa sababu na yeye ni mwana michezo, kwa kweli ukiwa wewe ni mwana michezo na ni Mjumbe wa Kamati ya Mapinduzi Cup, hivyo naomba tushirikiane na wizara ili kutekeleza ahadi hizi zote zinazotolewa na Mhe. Rais pamoja na wizara.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ni lini serikali itajenga uwanja wa kisasa katika Mkoa wa Kusini Unguja ili wana michezo wa Mkoa huo kuweza kufaidika na viwanja hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli wizara yangu ina mikakati thabiti ya kuweza kutekeleza ahadi zote tulizoahidi, pamoja na serikali kujenga viwanja kila wilaya. Mhe. Mwakilishi kwa kushirikiana pamoja na wewe tutafute viwanja ili tuweze kutekeleza majukumu ya michezo na vijana wetu.

Nam. 97

Kilimo – Mabonde ya Jimbo la Chambani

Mhe. Mohammed Haji Khalid (Kny: Mohammed Mbwana Hamad) – Aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo bado kinaendelea kuwa mhimili mkubwa wa maisha ya Wazanzibari, na kwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Moh'd Shein amesisitiza mapinduzi ya kilimo katika hotuba zake mbali mbali ikiwemo ile ya uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi tarehe 5 Novemba 2010, na kwa kuwa Waziri wa Kilimo aliwajenga matumaini makubwa wakulima, hasa katika hotuba yake ya Bajeti 2011/2012, na kwa kuwa hadi leo kuna mabonde mengi hayajalimwa na wananchi wanasubiri matrekta kwa ajili ya kulimiwa hasa katika Jimbo la Chambani, kama vile Bonde la Kichimba, Darajani, Mabieni, Miembeni na kadhalika, mabonde ambayo yakinyeshewa na mvua tu hayalimiki kwa hali yoyote.

(a) Je, wizara ina mipango gani katika kipindi hiki kulitatua tatizo hilo.

(b) Wizara ina tamko gani kwa wakulima wanaosubiri matrekta kwa ajili ya kulimiwa katika msimu huu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 97 lenye kifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe.Spika, kwa Pemba kilimo cha mpunga mwaka huu 2011/12 kilianza rasmi tarehe 1/11/2011, hadi kufikia tarehe 16/03/2012 jumla ya ekari 3,349.5 zimelimwa na matrekta ya Serikali sawa na asilimia 152.25 ya lengo lililowekwa (ekari 2,200) sawa na asilimia 160. Mhe.Spika, kati ya ekari 587 zilizolimwa Wilaya ya Mkoani ekari 309.25 sawa na asilimia 52.7 zimelimwa katika Jimbo la Chambani katika mabonde ya Chanjaani, Matele, Tunguni, Kwakimee, Kwakigenda, Kifuwa, Miguu Nje, Iju, Ziwani, Vimbuni, Tumbini, Kipapa, Agoni, Ndagoni, Chachani na Maziwapacha.

Mabonde haya yalilimwa katika mzunguko wa kwanza kuanzia tarehe 8/11 hadi tarehe 18/12/2011.

Mhe.Spika, nachukua fursa hii kumfahamisha Mhe.Mwakilishi, kwa wakulima wa mabonde ya Miembeni na Darajani ambao tayari wamelipia gharama za ukulima, wamo katika mzunguko tunaoendelea nao, na tunatarajia tutawalimia. Kuhusu wakulima wa Kichanje wanaosubiri huduma hii watalimiwa mara tu baada ya kulimiwa wakulima ambao wameshalipia gharama kwenye mabonde mengine. Kwa upande wa bonde la Miembeni wakulima wameshalima na kwa sasa wanasubiri kupatiwa mbegu na mbolea ambazo tayari zimeanza kuuzwa katika vituo vyetu vya mauzo.

b) Mhe. Spika, katika kutatua tatizo la wananchi wanaosubiri matrekta kwa ajili ya kulimiwa, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kuwalimia wananchi wote ambao kwa sasa wamelipia gharama ya huduma. Baada ya kukamilisha zoezi hilo tutaendelea na kuwalimia wale waliobakia ambao watazikusanya fedha zao na kuziwasilisha kwetu kupitia jumuiya zao kama ilivyoelekezwa hapo awali.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa katika maelezo yake Mhe. Waziri ameseme kwa Pemba tumevuka lengo la kilimo kwa msimu huu. Je, katika Jimbo la Mtambile ni ekari ngapi zimelimwa katika msimu huu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Haji kanitia mtihani, siwezi kujibu ghafla kwa Jimbo la Mtambile limelimwa ekari ngapi najua kwa Wilaya ya Mkoani ndio hizo ekari nilizozitaja sasa hivi, kwa hivyo hizo itabidi asubiri nimletee kwa maandishi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kua Mhe. Waziri amekiri kwamba Pemba wamevuuka lengo la kilimo kwa msimu huu. Je, anaweza kututhibitishia kua matrekta mangapi yako yanayofanya kazi na je, yanatosheleza na ikiwa hayatoshelezi Wizara yake inachukua hatua gani ya kupeleka matrekta haraka ili kile kilimo kilichotajwa hapa katika Baraza kiweze kufanikiwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, mwanzo Pemba yalipelekwa matrekta sita, na mara ya pili tulipopata mapya kutoka Dodoma tukapeleka matrekta manne, lakini hayo matrekta sita yaliyopelekwa mwanzo mengi yamepata matatizo kutokana na jua kali lililotokea wakati wa kilimo. Kwa hivyo, matrekta tuliyoyategemea hasa ni haya manne ambayo kusema kweli yanafanya kazi vizuri kwa sababu ni mapya na yameshapata kwa sababu ile ardhi imesharegea kutokana na mvua za rasha rasha zilizokua zinapita.

Kwa kweli matrekta hayo hayatoshi lakini hata hivyo wafanyakazi wa kilimo wamejitahidi kuhakikisha kwamba wanalima tena kwa bidii kubwa sana na ndio maana likavukwa hili lengo ambalo tuliliweka kwa ajili ya Pemba.

Hata hivyo, mimi nawapongeza kwamba walikua wamepanga kulima ekari 2,200 na wameshalima sasa hivi karibu ekari elfu 3, mia tatu na tisini na kitu, kwa hivyo wamejitahidi sana kusema kweli ndio maana wakafika hiyo asilimia 160. lakini matrekta kweli hayatoshi na sio Pemba tu hata Unguja hayatoshi.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kutuongoza vyema katika shughuli za Baraza letu kwa hekima na busara kubwa. Aidha napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

Mhe. Spika, Mswada huu ulikusudia kufanya marekebisho kwa sheria mbili, sheria hizo ni Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na pili ni Sheria ya Ruzuku kwa vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1997.

Mhe. Spika, baada ya mswada huo kupitishwa na kamati, Serikali ilipata ushauri kutoka kwa wadau wa mswada huu kwamba kuna haja ya kuiangalia Sheria ya Ruzuku ya Vyama vya Siasa kwa kina zaidi badala ya kufanya marekebisho katika kifungu kimoja tu cha sheria hiyo. Ingawa muda wa kutoa na kupokea maoni kuhusiana na mswada huo ulishapita, lakini Serikali iliona ni vyema kuyazingatia. Hivyo Serikali imeafiki kwamba Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa inahitaji kufanyiwa mapitio ya kina zaidi baada ya mashauriano na wadau wa sheria hii.

Mhe. Spika, kwa sababu hiyo na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 83(2) na (4) (b) naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali unafanyiwa marekebisho mawili muhimu.

Kwanza kwa kubadili jina la mswada kua Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011. Marekebisho hayo ni ya lazima kwa vile baada ya kuondoa sehemu inayohusu marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa katika mswada huu utakua unarekebisha sheria moja tu na hivyo haitakua sahihi kuuita Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

Marekebisho ya pili ni kufuta katika mswada huo sehemu ya tatu ya mswada inayohusu marekebisho ya Sheria ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1997. Marekebisho mengine ni ya mpangilio wa vifungu ambayo ni kama yalivyooneshwa kwa ukamilifu katika jadweli la marekebisho ambalo limegawiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, baada ya marekebisho haya naomba kuchukua fursa hii kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuupitia mswada huu mara mbili, kabla na baada ya marekebisho na kutushauri baadhi ya marekebisho muhimu. Mchango wao umesaidia sana kuufanya mswada huu kua bora zaidi.

Mhe. Spika, Sheria ya Utumishi wa Umma ni sheria ambayo ilitungwa ili kutoa nguvu za kisheria kwa mageuzi makubwa ya utumishi wa umma ambayo yanaendelea kufanywa. Hata hivyo, na kama ilivyotegemewa wakati wa utekelezaji baadhi ya mambo yamejitokeza ambayo yanahitaji marekebisho haya madogo ya sheria. Miongoni mwa mambo yaliyojitokeza ni pamoja na yafuatayo:-

a) Ni kuhusiana na muundo wa kitaasisi wa utumishi wa umma ambao haukuwepo wakati sheria inatungwa. Imejitokeza kwamba baadhi ya mambo hayo hayakuwekwa bayana ndani ya sheria, kwa mfano, uhusiano baina ya Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu Mkuu wa Utumishi hauko wazi, wakati Katibu Mkuu Kiongozi ndiye kiongozi wa Utumishi wa Umma, Katibu Mkuu wa Utumishi ndiye msimamizi wa kila siku wa shughuli za utumishi wa umma na ndiye mtendaji mkuu wa Ofisi Kuu ya Utumishi. Hivyo ni lazima hilo liwekwe bayana katika sheria. Aidha limejitokeza tatizo la Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuonekana kua na baadhi ya kazi ambazo ni za kiutendaji zaidi badala ya kua za kiusimamizi wakati Kamisheni yenyewe ni ya kiusimamizi.

b) Jambo jengine limetokana na hali halisi ya baadhi ya kada za kitaalamu kua na upungufu wa watendaji wapya kujaza nafasi zinazoachwa wazi na watumishi wanaostaafu. Mfano mzuri ni kada ya afya, sheria chini ya kifungu cha 60 (sheria ya utumishi wa umma) inaweka bayana kua baada ya muda wa kustaafu mtumishi anaweza kuongezewa muda wa ziada usiozidi miaka mitatu. Tatizo ambalo limejitokeza kwa baadhi ya kada hasa hiyo ya afya ni kua baada ya kumaliza muda huo wa miaka mitatu bado mtumishi huyo imeonekana anahitaji kwa vile hakuna watumishi wapya wa kushika nafasi hiyo. Ingawa tatizo hili linaweza kua la muda lakini hapana budi kutoa ruhusa kisheria katika kukabiliana nalo. Hivyo mswada unapendekeza kumpa uwezo Waziri wa utumishi kuainisha kada ambazo watumishi wanaweza kuajiriwa kwa mkataba baada ya kustaafu.

c) Mhe. Spika, suala jengine ni uhamisho wa watumishi na pia taratibu za kupangiwa kazi watumishi wa baadhi ya kada kama vile wahasibu na wakaguzi wa hesabu. Kwa upande wa uhamisho wa watumishi utaratibu uliopo katika sheria sasa hivi hautoi fursa kwa ofisi kuu ya utumishi ambayo ndio inayoratibu ikama za watumishi kuhusika kwa namna yoyote ile katika kuhamishwa watumishi kutoka Wizara au taasisi moja kwenda nyengine, jambo ambalo ni upungufu. Aidha, kwa upande wa utumishi wa kada maalum sheria haielezi chochote kuhusu uwezo wa baadhi ya taasisi zinazotumia baadhi ya kada kuwapangia kazi na kuwahamisha watumishi wa kada hizo. Sheria kama ilivyo sasa hivi imeondoa uwezo huo wakati haikukusudiwa iwe hivyo.

d) Mwisho Mhe. Spika, sheria hii ina jumla ya vifungu 105, lakini vifungu vmbavyo vinakusudiwa kufanyiwa marekebisho chini ya mswada huu ni vifungu saba, ambavyo ni kifungu cha tatu, kifungu cha 25, kifungu cha 29, kifungu cha 47, 9, 60 na kifungu cha 65.

Mhe. Spika, ni matumaini yetu ya dhati kwamba marekebisho haya yatasaidia sana mageuzi katika utumishi wa umma. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wajadili na kuyapitisha marekebisho haya ili kutoa nguvu ya kuendelea kuimarisha utumishi wa umma.

Baada ya kueleza hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

Mhe. Panya Ali Abdalla: (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujalia neema ya uhai pamoja na afya njema miongoni mwetu na kutuwezesha kukutana tena asubuhi hii ya leo katika ukumbi wetu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, katika kutekeleza majukumu yetu muhimu ya kitaifa.

Mhe. Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada huu muhimu wa Sheria ya Marekebisho ya Utumishi wa Umma Nam 2 ya 2011.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naomba kutoa mkono wa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Wananchi wa jimbo la Bububu, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu kufuatia kifo cha Mheshimiwa Salum Amour Mtondoo.Tunamuomba Mungu amlaze marehemu mahali pema peponi AMIN. Aidha, awajaalie wafiwa wote kuwa na moyo wa subra katika kipindi hiki kigumu,

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii vile vile nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kuhakikisha kua marekebisho haya ya sheria ni mazuri na pia yanaendana na wakati pamoja na mahitaji ya Wazanzibari wote.

Naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Raisi Utumishi wa Umma na Utawala Bora na watendaji wao kwa mashirikiano yao ya dhati waliyotupatia muda wote tulipokua tunajadili na kuuchambua Mswada huo kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, niruhusu niwapongeze na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora kwa mashirikiano makubwa wanayonipa pamoja na michango yao madhubuti waliyoitoa ili kuleta tija zaidi katika mswada huu. Mhe. Spika, ili kuzipa nguvu shukurani zangu hizo napenda kuwatambua wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
7.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
8.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
9.	Ndg. Abubakar Mahmuod Iddi	-	Katibu

Mhe. Spika, malengo ya Mswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam 2 ya 2011 ni kuifanya sheria hii iweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi.

Sheria ya Utumishi wa Umma ilikua na mapungufu kama ifuatavyo: Kwanza kabisa muundo wa kitaasisi wa umma haukuwepo wakati sheria inatungwa, pili kulijitokeza tatizo la Kamisheni ya Utumishi kuonekana kua na baadhi ya kazi ambazo ni za kiutendaji zaidi badala ya kua za kiusimamizi (*regulatory*).

Mhe. Spika, kutokana na hali halisi ya baadhi ya kada za kitaalamu kua na upungufu wa watendaji wapya kujaza nafasi zinazoachwa na watumishi wanaostaafu. Hivyo, mswada unapendekeza kumpa uwezo kisheria Waziri wa Utumishi kuainisha kada ambazo watumishi wanaweza kuajiriwa kwa mkataba baada ya kustaafu. Aidha, mswada huu unatoa fursa kwa Katibu Mkuu Utumishi wa Umma ambaye ndiye mratibu wa Ikama za watumishi kufanya uhamisho wa wafanyakazi katika utumishi wa umma kutoka Wizara au ofisi moja kwenda Wizara au ofisi nyengine kwa kushauriana na watendaji wakuu wa taasisi zinazohusika na uhamisho huo

Mhe. Spika, baada ya kazi ya kuupitia mswada huo, kamati yetu imependekeza na kuyakubali marekebisho kadhaa yenye lengo la kusaidia kuboresha mswada huo yakiwemo ya kilugha. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niainishe baadhi ya marekebisho ambayo kamati iliyapendekeza.

Kwanza, kamati yetu ilipendekeza ukurasa wa 51, sehemu ya kwanza katika kifungu cha kwanza neno la tatu kutoka mwanzo "**itajuulikana**"lisomeke "**itajulikana".** Pia sehemu ya pili ukurasa huo huo wa 51 kifungu cha 3(a) mstari wa tatu kutoka juu neno la kwanza "**itakayosimamiwa"**lisomeke "**itakayosimamia**"na kwa ukurasa wa 52 kifungu cha 5, kijifungu cha 29(1) mstari wa nne kutoka juu neno "**ataiwasilishwa"**liliopo baada ya neno "**thelathini"** lisomeke "**ataiwasilisha**", mstari wa sita kutoka juu neno la mwanzo "**kuiwasilishwa"** lisomeke "**kuiwasilisha**". Pia kifungu cha **3, 4, 5, 6, 7, 8** na **9** vibadilike na kuwa **2, 3, 4, 5, 6, 7** na **8**.

Mhe. Spika, kimsingi huo ndio mukhtasari wa kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka masharti bora ndani yake. Nawaomba wajumbe wote wa Baraza hili nao wauchangie vizuri Mswada huu kwa madhumuni ya kuiimarisha zaidi lakini hatimae kuukubali na kuupitisha bila ya pingamizi yoyote.

Baada ya kutamka hayo Mhe. Spika, natamka bayana kuwa mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naunga mkono Mswada huu kwa asilimia zote mia moja.

Mhe. Spika**,** naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru sana kuweza kunipa nafasi hii na mimi kwa upande wa wachangiaji ukiacha Mhe. Mwanasheria Mkuu ambaye ndiye aliyewasilisha huu mswada na Mhe. Panya ambaye ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa hivyo, mimi kwa upande wa wachangiaji nakua ndie wa mwanzo, nakushukuru sana kwa hilo.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Nataka nimpongeze kwa kuona baadhi ya mapungufu ya huu mswada wa Utumishi wa Umma ambao

tuliupitisha sio zamani sana. Mhe. Spika, lakini namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu tukijaaliwa kwenye uhai na uzima leo mswada huu au kesho baada ya waheshimiwa kuongeza yale wanayoyahisi tutaupitisha bila ya pingamizi yoyote.

Lakini Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu baadae katika michango yangu nitajaribu kutoa baadhi ya maangalio ambayo yatahitaji baadae huu mswada tuje tuufanyie marekebisho mengine. Kwa sababu, Mhe. Spika, tunakushukuru sana kwa namna kua kila unapopata nguvu sisi wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kutupatia mafunzo mbali mbali aidha kupitia njia ya semina, lakini baadhi ya mafunzo mengine ya muda mfupi ya ndani lakini hata mafunzo ya muda mfupi ya nje ya nchi yetu.

Mhe. Spika, hii inatupa upeo mkubwa sana wa kuweza kujadili mambo, kutafakari mambo, halafu vile vile kupambanua lipi linatakiwa liwe wakati gani na lipi liwe pahala gani. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nitaanza kuingia kwenye huu mswada lakini kuna baadhi ya mambo humu ukija kwenye masuala ya utawala bora bado hayako sawa sana, lakini kama ingelikua katiba yetu ina mwanya huu basi ningelijaribu kushauri kwamba hata jina la huu mswada basi pia tungelibadilisha au kuna baadhi ya vifungu ingebidi visisomeke kama vinavyosomeka sasa hivi.

Lakini tukiangalia katiba yetu bado inalazimisha baadhi ya mambo ambayo kwa sheria hii lazima itabidi tuyakubali, lakini bado tunahitaji katiba yetu si muda mrefu sana tuifanyie marekebisho mengi ambayo hayo ndio yatakayoweza hasa kuipelekea Zanzibar ikazidi kusifika katika suala zima la utawala bora katika nchi za Afrika lakini vile vile na duniani kwa jumla.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo sasa nitaomba niingie moja kwa moja katika mswada wenyewe. Kwanza nataka niendelee tena kumshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kua ni msikivu lakini vile vile ni mpokeaji wa ushauri. Naipongeza sana Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuona muono wa mbali kwa kuona kwamba huu mswada wa marekebisho ya sheria ulikuja na sheria mbili tofauti, lakini kwa busara tukasema tusifanye haraka hebu twende hatua kwa hatua. Mimi namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu amekua msikivu na nadhani baadae atajiandaa atatuletea mswada mwengine ambao tutakua tunashughulikia ile sheria ambayo inaangalia zaidi masuala ya vyama vya siasa. Nakushukuru sana Mhe. Mwanasheeria Mkuu.

Baada ya shukurani hizo tunamuomba vile vile aendelee kua msikivu kwa yale ambayo tutayatoa hasa ya kuisaidia nchi yetu katika masuala mazima ya kuimarisha utawala bora.

Mhe. Spika, mimi nataka nije katika kwenye mswada wenyewe na nitaanza moja kwa moja katika hiki kifungu cha tatu cha sheria hii ambacho kinasema kwamba, kifungu cha tatu cha sheria mama kinarekebishwa. Sasa Mhe. Spika, kwa kua mswada huu unakwenda kurekebisha mswada ambao tayari ulikuwepo kwa hivyo nitaomba uniruhusu nijaribu kukiangalia hiki kifungu cha tatu ili tuangalie je, kile ambacho tunakirekebisha kitakuwa ni kizuri zaidi kuliko kile kilichokuwepo mwanzo?

Mhe. Spika, hapa suala lililorekebishwa ilikua ni tafsiri ya Ofisi Kuu na hapa katika sheria hii ya mwanzo inasema kwamba, “Ofisi Kuu maana yake ni Ofisi Kuu inayosimamia Utumishi wa Umma iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 46 cha sheria hii”. Sasa kifungu cha 46 cha sheria

mama ambacho tunakifanyia marekebisho kifungu cha 3 cha sheria hii kinarekebishwa kinasema, 'Kufuta tafsiri ya neno Ofisi Kuu'.

Mhe. Spika, hili nadhani halina tatizo sana lakini nakuja zaidi huku mbele kunakosema maana yake Ofisi Kuu itakayosimamia Utumishi wa Umma kama ilivyoanzishwa chini ya kifungu cha 47 cha sheria hii.

Mhe. Spika, kifungu cha 47 cha sheria hii kilikua kinasema hivi "Kuanzishwa kwa ofisi ambayo itajulikana kama Ofisi Kuu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma ambayo itakua chini ya Katibu Mkuu"

Mhe. Spika, hapa (d) kinasema kwamba, "kuongeza tafsiri mpya ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa mpangilio wake, hapa kinasema, nafasi maalum maana yake ni utumishi wa umma kama inavyooneshwa katika kifungu cha 60 cha sheria hii". Mhe. Spika, nitaomba univumilie kwa sababu mswada huu una kazi kubwa kweli kuuchangia kwa sababu unataja vifungu ambavyo viko katika maeneo tofauti. Sasa kifungu (b) kinasema,

"Kuongeza tafsiri mpya ya maneno yafuatayo kwa mpangilio wake kiherufi. "Nafasi maalum" maana yake ni utumishi wa umma kama inavyooneshwa katika kifungu cha 60 cha sheria hii ambapo wataalam wake ni adimu, au inahitajika watu wenye ujuzi na uzoefu maalum au kwa maoni ya Waziri nafasi hiyo inahitaji wataalam maalum kutoka ndani na nje ya Zanzibar."

Mhe. Spika, hapa kifungu 60 (b) kilikuwa kinasema kuna mkataba wa muda mfupi au muda mrefu wa mtumishi ambao utakuwa kipindi cha kurejea rejea baina ya miezi 6, miaka mitatu utafungwa baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu kwa idhini ya Tume ya Utumishi wa Umma inayohusika. Kwa hali yoyote mwajiriwa wa utumishi wa umma aliyefikia umri wa kustaafu kwa lazima akiwa katika utumishi aliyeajiriwa kwa mkataba mfupi au kwa mkataba maalum katika nafasi ile ile aina ya ajira lakini anaweza kuongezewa ajira ya utumishi.

Mhe. Spika, sitaki nisome nasihi lakini nilikuwa nataka nije katika yale madhumuni hasa ambayo nimekusudia kuyasema. Mhe. Spika, ndio maana tukasema tunampongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea marekebisho haya. Kwa sababu bado sheria yetu ya Utumishi wa Umma ilikuwa inatoa *loophole* kwa watu ambao wameshastaafu kazi kuendelea kuajiriwa tena kwa mikataba. Ukiangalia ilikuwa haikuwekewa mipaka mtu yeyote alikuwa anaweza kuajiriwa kwa mkataba.

Sasa hii Mhe. Spika, kwa kweli ilikuwa inawavunja moyo sana watumishi wetu. Ukiangalia Mhe. Spika, tunaishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar kuanzia miaka ya 2000 mpaka mwaka 2010 serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali walifanya jitihada kubwa ya kuanzisha vyuo vikuu hapa Zanzibar.
Mhe. Spika, zamani enzi zetu sisi tuliobahatika kupata hiyo *degree* ya *form IV* basi unajilabu huko mitaani yaani unatamba mpaka ukenda ile mikono unaitanua kama hivi. Mhe. Spika, lakini kwa wakati wa sasa hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wamefanya jitihada kubwa kupitia jitihada za serikali yetu ambayo tulianzisha vyuo vikuu. Leo Mhe. Spika, unaposema unataka wanafunzi wenye *degree* hapo nje utakuwa huna pakuweka mguu.

Mhe. Spika, sasa hivi ukitaka vijana wenye *masters* na elimu nyengine za juu basi tuna benki nzuri ya vijana wenye taaluma waliosoma ambao wanahitaji kuja kusaidia serikali katika kujenga nchi yetu. Sasa ile *loophole* iliyokuwepo mwanzo ya kusema mtu ameshafikia umri wa kustaafu na tumepitisha sheria hapa miaka 60, wengine miaka 55 au 65 lakini bado huku mtu anaambiwa aendelee kupata ajira ya mkataba. Lakini ukiangalia pengine hata ile taaluma yake yule mtu ambaye anapewa mkataba bado itakuwa ni ya chini.

Lakini vile vile Mhe. Spika, mambo yanabadilika sasa hivi Waswahili wanasema tunakwenda na wakati, kasi ya dunia sasa hivi inakwenda mbio kuliko ile miaka ambayo tuliyokuwepo sisi huko nyuma, kwa hiyo sheria ilikuwa inaruhusu watu kuajiriwa kwa mikataba.

Mhe. Spika, tuna kumbukumbu nzuri hapa katika nafasi za uteuzi kuna watu wameteuliwa katika ngazi mbali mbali wananchi wanalalamika, lakini wananchi wakilalamika watasema wapi pakusemea hapana kwa sababu mamlaka ya uteuzi hatukuiwekea mipaka ya ule uteuzi. Kwa hiyo, utakuta kuna wakurugenzi wakati mwengine wanateuliwa wameshastaafu lakini wanaendelea kuteuliwa tena.

Sasa wale vijana waliosoma wenye shahada nzuri ambao wametoka vyuoni wengine wanafanya kazi wana uzoefu zaidi ya miaka mitano sita kwa kweli wanavunjika moyo. Hii Mhe. Spika, ilikuwa inapelekea hata kwa yale mambo ambayo si ya kuyaamini sana lakini bado katika mazingira yetu tunayaamini.

Mhe. Spika, inapokuwa ajira haina mpaka watu unawafanya mpaka kwenda kwa babu, maana yake mtu anaona kwamba huyu jamaa umri wake wa kustaafu umeshamalizika na hapa tunategemea kutokana na ngazi yangu ya elimu niliyokuwanayo basi akiondoka kiti kile aidha huenda nikakikalia mimi, lakini sasa baada ya muda nasikia bomba linamtangaza yule yule anarudi. Sasa hii ilikuwa inapelekea watu kuanza kutafuta mafusho kwa wingi, udi kwa wingi, kwenda kwa babu sasa kumuondoa mtu kwa nguvu.

Sasa Mhe. Spika, sheria hii sasa hivi marekebisho haya tunamuondoa mtu kisheria sio kwa nguvu ya kiza. Mimi kwa kweli nashukuru sana hii itatupunguzia hata chuki.
Mhe. Spika, hili suala tunaliona dogo lakini ni suala kubwa sana, hili linaondosha chuki mpaka kule mawizarani kwamba huyu mtu jamani kishastaafu tena kishafanyiwa sherehe kishapewa baiskeli na *package* yake yote lakini kesho kutwa unamsubiri anarudi tena pale pale.

Kwa hiyo, nilitaka nikifafanue sana kifungu hichi kwa sababu ya ule umuhimu wake. Kwa kuwa hapa amepewa mamlaka waziri ili kutangaza zile nafasi au kada maalum naomba sana Mhe. Waziri hapa ajaribu kufanya *research* ya kutosha kuangalia ni maeneo gani ambayo tuna upungufu wa wataalam, tuna maeneo gani ambayo akiondoka huyu utaalam wake tunauhitaji tutaukosa. Kwa hiyo, hili nilikuwa naliomba sana hapa Mhe. Waziri ana kazi kubwa, ana changamoto kubwa ya kuweza kukaa na kutathmini halafu aangalie ile *package* ya wataalam waliokuwepo Zanzibar.

Sasa Mhe. Spika, sijui kama tunayo *data base* hapa Zanzibar ambayo inasema katika kada hii mambo ya *engineering* tuna watu idadi fulani ambao wenye *CV* fulani, katika kada ya mambo ya afya tuna watu wangapi wenye *CV* fulani. Kwa hiyo, hili ni suala muhimu sana hasa kwa Waziri

wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, lazima ahakikishe kwamba ana *data base* ya kutosha kujua wataalam wetu wa kada zote Zanzibar ili asije akasema kwamba anatoa *loophole* ya kumpa ajira mtu ya mkataba au ya kuruhusu Katibu Mkuu Kiongozi kumpa ruhusa mtu mkataba wa muda lakini kumbe halafu baadae watu wanakuja kuanza kushtuka anasema mbona fulani ana *Phd* ya somo fulani. Sasa mimi nafikiri sheria hii tunapoipitisha lazima kuwe kuna kazi nyengine ya kufanyika, hapa tunampa kazi Mhe. Waziri ili atengeneze *data base* sasa ya kuhakikisha kwamba tuna wataalam kiasi gani hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, hii *data base* yenyewe tusiangalie labda wale Wazanzibari tuliokuwanao humu ndani ya nchi. Mhe. Spika, sasa hivi kuna wataalam wetu wa Kizanzibari wako Tanzania Bara pengine kutokana na mazingira moja au mengine wameamua kuhama kutokana na kwamba wanashindwa kuutumia utaalam wao vizuri kutokana na vikwazo mbali mbali, chuki, ubinafsi, fitna na mambo mengine. Sasa hii itajaribu kutupelekea kwamba kuangalia na wataalam wetu ambao wako Tanzania Bara tunaweza tukaja tukawapa nafasi hizi za kuweza kuja kushika nafasi kubwa sana hasa katika utumishi wa umma.

Sasa hii Mhe. Spika, utaona nilikuwa naogelea sana kwa sababu tayari nilikuwa na mifano mingi iliyokuwepo ambayo wananchi wanakuwa wanalalamika. Lakini hii vile vile itawapa motisha vijana wetu waliokuwepo maskulini. Juzi tu tulikuwa tunapiga kelele hapa serikali yetu mfuko wa elimu ya juu kuna wengine walituona labda wakorofi aaa, tulikuwa tunajaribu kuikumbusha serikali kwamba huku kuna wasomi wanataka kuongeza taaluma ili waje kuisaidia Zanzibar.
Mhe. Spika, utafika wakati ndani ya chombo hichi cha kutunga sheria hata ile sheria yetu ya kusema kwamba mtu ambaye anaingia humu ndani ya Baraza la Wawakilishi awe anajua tu kusoma na kuandika tena Kiswahili, nafikiri lazima itabidi baadae si muda mrefu sana na hasa kutokana na jitihada ya serikali yetu kuongeza madarasa, kuongeza elimu kubwa sana Zanzibar, sasa hivi tunataka lazima chombo hichi kiwe na watu ambao wanaweza kujua mambo na kupima mambo na kuweza kuamua mambo kwa maslahi ya Wazanzibari na wakati mwengine wa miaka 50 au 100 inayokuja.

Kwa hiyo, hii itatoa motisha kwa vijana wetu waliokuwepo vyuoni kuzidi kuendelea kusoma hivi sasa ili kuhakikisha kwamba kuna nafasi sasa hivi zinakuwa hazina mjomba, nafasi zitakazokuwepo hasa nafasi kubwa kubwa itategemea na ile elimu uliyokuwanayo.

Mhe. Spika, mimi nataka nikutolee mfano mdogo hivi karibuni kuna wenzetu wanaotaka kugombania nafasi ya ubunge ya Bunge la Afrika Mashariki. Mhe. Spika, kwa mara ya mwanzo kabisa tumeweza kuona vijana wadogo ambao wana taaluma kubwa wanataka kuchukua nafasi hizi. Mhe. Spika, nadhani hata Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au vile vyombo vya maamuzi vinavyojaribu kutaka kupitisha kuchuja watapata kazi kubwa sana ya kuweza kuangalia nani hasa mwenye hizi sifa zinazotakiwa.

Sasa hii inatokana na jitihada za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuweza kufungua langa la elimu ili wananchi wetu waweze kusoma. Tunawashukuru wananchi wetu wameweza kuitumia fursa hiyo kwa kiasi kikubwa sana.

Mhe. Spika, sitaki nikuchoshe sana kwa maneno mengi nataka niendelee vile vile katika kifungu cha 29 (5) cha mswada wa marekebisho. Anasema “Kifungu cha 29 cha sheria hii mama

kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo.” Mhe. Spika, kifungu cha 29 cha mswada huu kilikuwa kinasema “Kamisheni sio zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha itatayarisha na kuwasilishwa kwa Rais nakla kwa Waziri ripoti ya mwaka juu ya hali ya ufanisi wa utumishi wa umma.”
Halafu 29 (2) kinasema “Pamoja na mambo mengine itajumuisha mambo yaliyobainishwa chini ya kifungu cha 15 (2) cha sheria hii.”

Sasa mimi narudi katika hichi kifungu cha 29. Mhe. Spika, kifungu hichi kilikuwa kinaleta urasimu kidogo katika kazi. Tunamshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuliona hili sasa naomba nikisome hivi ambavyo kama kitakavyokuwa kinasomeka.

Kifungu cha 29 kinasema “Kamisheni sio zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka juu ya hali ya ufanisi wa utumishi wa umma na Waziri ndani ya siku 30 ataiwasilisha kwa Rais na iwapo ndani ya siku 30 Waziri ameshindwa kuiwasilisha kwa Rais Kamisheni itawasilisha wenyewe ripoti hiyo.”

Sasa hapa Mhe. Spika, kwanza nilikuwa nataka nipongeze kwa sababu pale mwanzo ilikuwa iko *vice versa* inakwenda kwa Rais halafu nakala kwa Waziri. Kwanza barua au jambo lolote linalokwenda kwa Rais halina nakala, sasa unapopeleka nakala ina maana inakuwa masikio yamekiuka kichwa. Kwa hivyo, hili tunaishukuru Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeliona kwamba sasa hivi moja kwa moja ile ripoti itakwenda kwa Waziri na baada ya siku 30 ambazo Waziri kama hajaipeleka kwa Mhe. Rais Kamisheni itapeleka wenyewe.

Sasa hapa kidogo Mhe. Mwanasheria Mkuu nitaomba ufafanuzi. Kwa sababu ile ripoti atapelekewa Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndani ya siku 30 anatakiwa ampelekee Mhe. Rais, lakini ndani ya siku 30 kama hajaipeleka Kamisheni itapeleka wenyewe. Je, Kamisheni itajuaje kwamba Waziri ampelekea Mhe. Rais maana yake sasa itabidi waende wakamuulize Rais kule vipi wameshakuletea vitu ambavyo haviendani. Sasa hapa nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu aje atupe ufafanuzi je, Kamisheni hii taarifa itaipata vipi ili kuona kwamba kweli Mhe. Rais ile taarifa ameshapelekewa.

Lakini jengine Mhe. Spika, nakuja katika kifungu cha 47 (1) ambacho kinasema “Kifungu cha 47 cha sheria mama kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo.” Naomba Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nikinukuu kifungu cha 47 kwa sababu kama nilivyosema kwamba marekebisho ya sheria lazima tujue kwamba je, tunachokifuta na tunachokiweka kipi kinakuwa kiko bora zaidi.

Kifungu cha 47 katika sheria mama kinasema kwamba “Kuanzishwa ofisi ambayo itajulikana kama Ofisi Kuu ya Usimamizi w Utumishi wa Umma ambayo itakuwa chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu.”

Sasa hapo katika marekebisho Mhe. Spika, kinasema kifungu cha 47 (1) kunaanzishwa ofisi ambayo itajulikana kama Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma ambayo itakuwa chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu ambaye atakuwa msaidizi mkuu wa Katibu Mkuu Kiongozi kwa mambo yote yanayohusiana na Utumishi wa Umma.

Halafu kifungu cha 47 (2) kinasema hivi “Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma itakuwa ni chombo cha kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Katibu Mkuu Kiongozi katika Utumishi wa Umma.”

Sasa hapa Mhe. Spika, ndio pale niliposema kwamba katika siku za mbele tunahitaji hii katiba yetu lazima tuje tuifanyie maboresho mengine ambayo itaonesha hasa ile *separation of power*. Mhe. Spika, ukiangalia hii Katiba ya Zanzibar kifungu cha 5 naomba nikinukuu kinasema “Zanzibar itafuata mfumo wa demokrasia wa vyama vingi vya siasa wenye kuheshimu utawala wa sheria, haki za binaadam, usawa na amani, haki na uadilifu.”

Halafu kifungu cha 5A (1) cha Katiba ya Zanzibar kinasema “Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu, Mamlaka ya Utendaji, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma na Mamlaka ya Utekelezaji wa Utoaji Haki.”

Sasa hapa Mhe. Spika, ukiangalia kifungu hichi cha 5 (2) cha Katiba ya Zanzibar kinasema “Mamlaka ya Utendaji ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli zai Umma ni Baraza la Wawakilishi na Mamlaka ya Utekelezaji na Utoaji Haki ni Mahakama.”

Sasa hapa Mhe. Spika, tunapopitisha sheria hii tukasema kwamba Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma itakuwa ni chombo cha kusimamia na kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Katibu Mkuu Kiongozi katika Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, sisi kwa bahati tulipata nafasi ya kuonana na Wabunge wa Mabunge mbali mbali ambao walitembelea hapa Zanzibar tukajaribu kubadilishana mawazo namna wanavyoendesha Mabunge yao, lakini vile vile tumepata nafasi ya kuonana na wenzetu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujifunza na kuona ni namna gani wenzetu wanavyoendesha shughuli zao vile vile.

Mhe. Spika, hapo nyuma kabla Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawajapitisha ile sheria yao ya *Parliamentary Service* Zanzibar tulionekana kwamba tuko mbele sana hasa katika utekelezaji wa utawala bora na *separation of power*. Kwa sababu ndani ya Katiba ya Zanzibar ilitoa mamlaka ya Baraza la Wawakilishi kuweza kutunga sheria ambayo itaweza ku-*govern* masuala yao mpaka ya utumishi. Lakini ikaelezwa vile vile ndani ya katiba kwamba katika kifungu cha 76 cha katiba hii kama sikosei kilieleza vile vile hata katika suala zima la uteuzi wa Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

Lakini ukiangalia katika kifungu cha 77 hichi ndio kinaeleza wazi wazi kimeipa hasa ile mamlaka ya Baraza la Wawakilishi katika kujipangia zile taratibu zao. Naomba kidogo nikinukuu kifungu cha 77 (2) cha Katiba ya Zanzibar kinasema “Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi ambayo itakuwa na uwezo wa kuwaajiri maafisa na watumishi wote wa Baraza, kuwapandisha vyeo, kuwachukulia hatua za kinidhamu na kufanya kazi nyengine zozote zitakazoelekezwa na sheria kuhusu utumishi katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi, isipokuwa kwamba Katibu wa Baraza la Wawakilishi atateuliwa na Rais kwa mujibu wa kifungu cha 76 cha katiba.”

Sasa Mhe. Spika, ukiangalia kifungu hichi cha 77 kiliipa mamlaka kamili Baraza la Wawakilishi kujipangia shughuli zake mpaka za utumishi. Lakini ukija katika sheria hii bado mamlaka ile vile vile tunapokonywa kwa upande mwengine hasa katika usimamizi. Ukiangalia Mhe. Spika, wenzetu Bungeni walikuja kujifunza hapa Zanzibar matokeo yake sasa hivi sheria yao wao iko *more advance* kuliko ilivyo yetu hii sasa hivi.

Mhe. Spika, sasa hivi wenzetu kule katika ile sheria yao ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba "Uajiri ambao unaofanyika ndani ya Bunge ni mwenyewe Katibu wa Bunge kwa kushirikiana na Kamisheni ya Bunge wao ndio wanafanya uajiri na watumishi wale wa Bunge hawatoweza kupokea maagizo na maelekezo kutoka taasisi nyengine yoyote nje ya Bunge."

Sasa Mhe. Spika, ukiangalia wenzetu walikuja kujifunza kwetu matokeo yake sasa hivi wao wako *more advance* kuliko sisi sasa hivi. Kwa hiyo, ndio maana tukasema kwamba katiba yetu baada ya muda mfupi nadhani iko haja ya kufanyiwa marekebisho kidogo ili kama pale mwanzo tulikuwa tuko mbele na sasa hivi tuzidi kuwa mbele zaidi tusiwe tunarudi nyuma.

Mhe. Spika, nilikuwa najaribu kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya yale mambo ya angalizo hapo baadae ili serikali yetu ipate muda mzuri wa kuweza kujaribu kuangalia hayo marekebisho.

Lakini Mhe. Spika, la mwisho kabisa nataka nipongeze zaidi katika suala zima la uhamisho kifungu cha 9. Mhe. Spika, hapa namba 9 kifungu cha 65 cha sheria mama kinarekebishwa kutokana na muda sitoweza kukirejea, kinafuta kifungu cha 3 na badala yake kuweka kifungu kifuatacho. Kifungu 9 (3) kinasema "Uhamisho wa wafanyakazi katika utumishi wa umma katika wizara na ofisi moja kwenda wizara au ofisi nyengine ndani ya utumishi wa umma utafanywa na Katibu Mkuu wa Utumishi wa Umma baada ya kushauriana na watendaji wakuu wa taasisi zinazohusika na uhamisho huo."

Mhe. Spika, hapa Mwanasheria Mkuu kaona mbali, sasa hivi kuna malalamiko hasa katika kada ya hawa wahasibu. Mhe. Spika, wakati mwengine ule utaratibu wa uhamisho wao unakuwa unatuletea malalamiko mengi hasa tunapokuwa katika shughuli zetu za kamati hawa wahasibu pamoja na wakaguzi. Mhe. Spika, suala hili kwa sababu ule mwiba ulikochomea ndio unakotokea kule kule. Sasa ni vizuri hapa sasa hivi kwamba katika suala zima la uhamisho wa hawa watendaji kutakuwa kuna chombo chengine kinachosimamia ule utendaji. Mhe. Spika, katika kamati zetu tunapotembelea kwa kweli tunaona mambo mengi ambayo wakati mwengine yanaleta malalamiko yanayotokana na ule uhamisho ambao unaleta na dhana pengine wala haipo.

Lakini sasa katika suala zima la uhamisho kwa kuwa Wizara yenyewe inayoshughulika na Utumishi wa Umma itakuwa ni msimamizi vile vile kwa kushirikiana na ile taasisi inayohusika, hapa nadhani yale malalamiko sasa hivi yataweza kuondoka na tutaweza kuhakikisha kwamba ule uhamisho unaofanywa utakuwa hauna upendeleo wowote wala haulengi labda maslahi ya mtu fulani au maslahi ya watu wachache.

Mhe. Spika, nilikuwa na mengi ya kuzungumza katika mswada huu lakini kutokana na muda nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu wa mawazo, nadhani imeweza kukidhi kwa yale niliyokuwa nayatarajia na mengine yaliyobakia nitawapa wenzangu ili waweze kutia nyama. Mhe. Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuchangia mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Mhe. Spika, kabla sijafanya hivyo naomba uniruhusu nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa mara nyengine tena kutujaalia neema zake tukaweza kukutana tena hapa kujadili masuala yanayohusu maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, niungane na Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuipongeza serikali na hasa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuleta mswada huu wa marekebisho ya sheria hii ambayo tuliipitisha mwaka jana.

Mhe. Spika, nampongeza Mwanasheria Mkuu kwa sababu ni moja katika misingi ya utawala bora tunapoona kwamba tumepitisha sheria halafu tukaigundua katika utekelezaji kwamba kuna mambo ambayo yanaleta kwa lugha za miaka ile wakisema mikingamo basi si vibaya kuletwa hapa ikafanyiwa marekebisho tena. Kwa sababu Mhe. Spika, sisi sote si wakamilifu mkamilifu ni mwenyewe tu Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala.*

Mhe. Spika, kabla ya kuingia katika vifungu vya mswada huu na mimi naomba uniruhusu nizungumze mambo machache ya jumla halafu niingie katika mswada lakini yanahusika na suala hili.
Mhe. Spika, kwanza kabisa nataka nitoe wito kwa serikali kwa sababu serikali inawajibika kwa pamoja hapa kwamba baada ya kulitazama sana suala hili la utumishi wa umma ambao ulitokana na utafiti uliofanywa wa namna gani ya kufanya mageuzi katika sekta hii ya utumishi wa umma. Kazi nzuri imefanyika pia sasa lile eneo la pili linalohusu mageuzi katika serikali za mitaa litazamwe kwa makini mambo haya yalikuwa yanakwenda pamoja *Public Service Sector Reform* na *Local Government Sector Reform.*

Kwa hivyo, nilikuwa nadhani Mhe. Spika, suala hilo serikali wakati umefika ilitazame badala ya kupewa ahadi kila siku ambazo hazitekelezwi tuone kwamba mswada huu pia wa *Local Government Sector Reform* unaletwa ili Zanzibar nayo iwe na mfumo wa uhakika wa Serikali za Mitaa zinazotokana na matakwa ya wananchi wenyewe. Hiyo ndio misingi ya utawala bora.

La pili Mhe. Spika, mimi vile vile nataka nizungumzie la jumla kwamba tulipokuwa tukijadili katika kamati mwaka jana sheria hii ilipokuwa ndio kwanza inakuja na nashukuru ulinipanga katika Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala tulijadili mambo mengi sana. Moja la jumla ambalo nataka serikali ilitazame tena na tena pamoja na kuleta marekebisho haya ni suala zima la kuangalia uzoefu wa wenzetu katika nchi hasa za Jumuiya ya Madola *(Commonwealth)* ambazo mara nyingi katika mifumo yao kunakuwa na Waziri Mkuu mwenye madaraka ya mfumo kama wetu ambao tumo katika Jumuiya ya Madola lakini tumechanganya mfumo wa

Rais kwenye madaraka kwa maana ya *Presidential System* na mfumo wa Kibunge *(Parliamentary System).*

Mhe. Spika, kwa nini nalisema hilo. Katika nchi za wenzetu ambapo kuna Waziri Mkuu mwenye madaraka na ndio mwenye nguvu mfumo wa utumishi wa umma unakuta unajiweka wenyewe kwa sababu Katibu Mkuu Kiongozi anakuwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu katika mfumo kama ule si aghlabu kukuta kuna Wizara ya Utumishi wa Umma lakini kwetu sisi hali tofauti.

Sasa ndio mara nyingi tunakuta kunakuwa na mgongano wa madaraka baina ya Katibu Mkuu Kiongozi ambaye yuko Ikulu ofisi kubwa na Katibu Mkuu na Wizara yake inayoshughulikia Utumishi wa Umma ambayo nayo ni afisi ya Rais lakini ni Wizara ambayo imewekwa kama vile inajitegemea kwa kiasi fulani. Kwa hivyo kunatokezea mvutano na tunaona hata marekebisho haya yanajielekeza huko huko Mhe. Spika. Nadhani sio katika maeneo hayo ambayo hivi sasa Serikali imeona, mimi nadhani bado yako maeneo mengi ambayo Serikali inapaswa iyatazame katika mfumo wetu ili tuone vipi tutaondosha huo mgongano ambao upo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa niende kwenye vifungu na kutoa maoni yangu. Mhe. Spika, niseme ilipaswa maoni haya mengi niyatoe kupitia Kamati, lakini kutokana na dharura, mara hii sikuwahi kushiriki katika Kamati. Nawashukuru wenzangu waliofanya wameyaona na mimi nitumie fursa yangu kama mjumbe kutoa maoni machache na pia kutaka ufafanuzi katika yale maeneo ambayo naona bado sijatoshelezeka juu ya ule ufafanuzi uliotolewa.

Mhe. Spika, kifungu cha 3 ambacho katika marekebisho sasa kinasomeka kama cha 2, lakini nitafuata kama ulivyo katika mswada tuliopewa. Kifungu hiki kimetoa tafsiri mpya ya ofisi kuu ya utumishi, ambayo kimsingi ina boresha zaidi, lakini nilipo mimi zaidi ni pale kwenye kifungu kidogo cha (b) kinachozungumzia nafasi maalum. Maoni yangu haya Mhe. Spika, nitayatoa kuhusiana na kifungu cha 3 hicho, lakini pia kifungu cha 8 cha mswada huu ambacho kinarekebisha kifungu cha 60 cha sheria. Vifungu hivi kijumla vinazungumzia juu ya hizi nafasi maalum ambazo zinatoa nafasi ya kuweza kuajiriwa watu hata nje ya utaratibu ambao umezoeleka kwa kuwaongezea muda watumishi ambao wameshastaafu.

Hoja yangu Mhe. Spika, ni indhari tu kwamba tunatoa nafasi hii lakini itumike vizuri sana Mhe. Spika. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan, kuwa Zanzibar hivi sasa tunaongezeka kiidadi, lakini pia idadi ya wanafunzi wanaohitimu katika vyuo vikuu inaongezeka. Mhe. Spika, na tuna wengine kwa maelfu bado wako skuli wanahitimu kila mwaka, wanaingia katika kada hizi wakimaliza nao wanategemea ajira hizi hizi.

Mhe. Spika, katika nchi yetu Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aliwahi kutuambia kwamba bahati mbaya sekta binafsi haijakuwa. Kwa hivyo, bado ajira katika sekta binafsi ni ndogo mno, matokeo yake asilimia kubwa ya watu wetu bado wanategemea sekta hii hii ya umma. Sasa tunapotoa nafasi kama hizi zikitumika vibaya, tukaendelea kuweka watu ambao wameshamaliza nafasi yao ya kutumikia umma, tunawazuilia wengine ambao walipaswa kupewa nafasi hii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tuseme kitu kimoja, uendeshaji huu wa mambo unabadilika kila siku katika Serikali na kila siku dunia inabuni njia mpya. Vijana wapya wanaosoma sasa wanapata nafasi ya kujifunza mambo haya, hivyo wanapaswa na wao wapewe nafasi ya kutumia taaluma zao ili kuingiza huu ubunifu mpya ambao wameupata huko uingie katika Serikali ili tubadilishe utendaji mzima wa Serikali. Lakini tunapoendelea kuwaweka watu wale wale Mhe. Spika, chini ya vifungu vya kuwaongezea muda au kuwapa mikataba wastaafu, basi tunawazuilia hawa wengine wasipate nafasi zao na hatutendi haki Mhe. Spika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nataka nitoe mfano hai, hiki ni chombo cha wananchi tunapaswa tuwe wazi hapa. Mfano hai unaonekana katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Serikali pale imerundika wastaafu katika nafasi kubwa kabisa za utumishi, matokeo yake katika Wizara ambayo inakabiliwa na utendaji mbovu moja ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Kamati ya Baraza lako ikienda inayaona hayo.

Juzi tu Mhe. Spika, tumeshuhudia katika ziara iliyofanywa ya Makamo wa Kwanza wa Rais katika vikao nilivyovifuatilia pale vilivyofanywa na watendaji, basi Mhe. Waziri kavumbua mambo mengi sana ambayo yametolewa na watumishi wadogo na mengi ukitizama yanakwamishwa na wakuu wa idara zile ambao wengi ni wastaafu ambao wamechoka Mhe. Spika, hawana mawazo tena. Niliwahi kusema mara nyingi na wajumbe wenzangu walisema katika Baraza hili.

Mhe. Spika, wastaafu hawa unaweza kuwachukua kwa mkataba maalum ikiwa wana kumbukumbu nzuri, kwa hivyo unawahitaji waendeleze kutoa utumishi wao. Lakini wastaafu hao Mhe. Spika, wengi wao ni *total failure* katika idara wanazoziongoza, wameondoka pale wakiwa wameacha kumbukumbu mbovu halafu wanarejeshwa, matokeo yake ndio haya ambayo yanaonekana. Kama nilivyosema Mhe. Spika, sisemi mimi juzi yamedhihirika katika ziara ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika Wizara hii, yamezungumzwa na wafanyakazi wenyewe wa Wizara, wakilalamikia idara mbali mbali ambazo nyingi zinaongozwa na wastaafu kama hawa ambao wamechoka Mhe. Spika.

Kwa hivyo, nasema kifungu hiki nakikubali. Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu kinalenga kushughulikia maeneo, kwa mfano Wizara ya Afya kuna uhaba wa wafanyakazi, nakubali. Lakini ninachosema kisitumike vibaya kuleta watu kama hawa ambao wameshachoka na hawana mawazo tena, wanazuia nafasi ambazo wangeweza kupewa vijana wakaleta mawazo mapya, wakaleta mitindo ya kisasa ya uendeshaji wa Serikali na nchi yetu ikapata mabadiliko Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niende katika kifungu cha 4 ambacho kinarekebisha kifungu cha 25 cha sheria mama. Mhe. Spika, suala hili naomba ufafanuzi tu sina maoni. Kifungu hiki kimesema kinafuta aya ya (L) na (N). Tunamshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kajenga misingi mizuri ya utawala bora, katupatia mpaka jedwali ambalo linaonesha vifungu vilivyokuwepo na ambavyo vinarekebishwa.

Mhe. Spika, ukivitazama vifungu hivi, mimi kwa mtazamo wangu vina mambo ya msingi kabisa, sasa najiuliza kwa nini vinafutwa.

Kwa mfano kifungu hicho cha 25 kinazungumzia, (*L) to keep public service structure operations management relationship and deliver under regular review and recommend to the President measure necessary to rectify.*
Sasa ndio nikajiuliza kwa nini hilo tuliondoe, hasa tukizingatia Kamisheni hii ya Utumishi wa Umma hii inawajibika kwa Rais.

Vile vile (N) iliweka jukumu la, *to issue and review public service staff manual from time to time.*

Mhe. Spika, katika nchi ambazo zimejiweka vizuri, hili lililozungumzwa kwenye kifungu (N) ni jambo la msingi sana. Nimebahatika kuona Mhe. Spika, katika kumbukumbu za zamani wakati wa ukoloni hapa, hii *public service manual* ilikua inaonesha watumishi wote waliokuwepo Zanzibar, tena katika kitabu kidogo, ikieleza tarehe zao za kuzaliwa, wasifu wao, historia yao ya kufanyakazi na mpaka viwango vyao vya mishahara viliwekwa hakukuwa na usiri ambao tunauweka leo. Sasa ndio nauliza kwa nini tunaviondosha vifungu hivyo, ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja tuelezwe hili, kwa nini Serikali imeona kuna haja ya kuviondoa vifungu hivi vya (L) na (M).

Mhe. Spika, kifungu cha 5 ambacho kinarekebisha kifungu cha 29 cha sheria mama, maoni yangu hayako mbali na maoni ya Mhe. Hamza Hassan, nataka niyaunge mkono kabisa. Mhe. Spika ni kwamba hapa utaratibu ulikua ni kua Kamisheni inapeleka ripoti kwa Rais, sasa ndio katika ile niliyosema mwanzo tatizo la kua na upinzani baina ya Katibu Mkuu Kiongozi Ikulu na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inasema ripoti itapelekwa kwa Waziri, Waziri atapeleka kwa Rais. Lakini ikiwa hakuipeleka ndani ya mwezi mmoja basi kamisheni itapeleka jibu.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan sisi tunajiuliza hii kamisheni itajuaje, mawasiliano baina ya Waziri na Rais ni yao wao wenyewe, hayapaswi kupitiwa wala hawawezi kuyajua Kamisheni ya Utumishi wa Umma, sasa itajuaje ile. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikua naomba tuelezwe, kama kuna haja ya kufanya marekebisho zaidi ili kuona vipi tutaweka utaratibu mzuri zaidi basi nilikua nadhani tulizingatie hilo katika kifungu hicho cha 29 kinachorekebishwa.

Mhe. Spika, kifungu cha 6 kinachorekebisha kifungu cha 47, sina matatizo sana, kwa sababu kimsingi kifungu hiki kinasema vile vile kwamba kutakua na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye kwa mujibu wa katiba yetu kifungu cha 49 ndiye kiongozi mkuu wa utumishi wa umma, sasa katibu mkuu katika Ofisi hii ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora amefanywa kama ni msaidizi wake katika suala la kuanzisha Ofisi Kuu ya Utumishi. Kwa hivyo, hilo mimi sina mashaka nalo sana.
Mhe. Spika, nirudi tena kwenye kifungu kile cha 60 kuna nukta nyengine. Kifungu cha 8 ambacho kinarekebisha kifungu 60, kuna (a) na (b). Hapa mawazo yangu Mhe. Spika, inahusu pia aliizungumzia Mhe. Hamza Hassan, suala zima la ugawaji wa madaraka katika mamlaka tatu. Mhe. Spika, tulipokua tukiujadili mswada huu katika kamati mwaka jana, wajumbe wenzangu wanakumbuka, hata Mhe. Waziri anakumbuka. Mnajua alikua Mhe. Makungu ndiye alikua Mwanasheria Mkuu. Tulichukua nafikiri wiki nzima kuupitia mswada ule, mambo mengi yalituhangaisha.

Moja ni kuona vipi sheria hii haiji kukiuka misingi ya katiba tuliyoweka Mhe. Spika. Sasa hapa pamefanywa marekebisho, moja nataka kusema na lugha nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu alizingatie. Pale palipotajwa *respective services commission*, nadhani katika sheria tuliweka *boards* kuzitofautisha hii kamisheni na zile mamlaka, maana yake kuna mamlaka nne ya Serikali, kuna Baraza la Wawakilishi, Mahakama ni idara maalum, nakumbuka zile kwa Kiingereza tuliziita *boards*, kwa hivyo hilo ni la lugha tu.

Lakini mbali ya hilo, ukitizama marekebisho haya Mhe. Spika, bado yana muweka Katibu Mkuu Kiongozi katika mamlaka ambayo yuko juu ya Tume zote, ningetoa mfano Mhe. Spika. Hapa nikisoma ilivyorekebishwa inasema, mfano (b), Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kushauriana na Tume husika anaweza kutoa ruhusa ya kuajiriwa kwa mkataba maalum kwa mtu ambaye ana sifa, utaalamu na uzoefu katika nafasi iliyotangazwa na Waziri chini ya kifungu cha 60(1)(b) cha sheria hii.

Mhe. Spika, utakuta mwenye madaraka hapa ni Katibu Mkuu Kiongozi hawa wengine anawashauri tu, lakini mimi kwa mtizamo wangu hii bado inapingana kwa kiasi fulani na katiba yetu, namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu akija suala hili atusaidie Mhe. Spika kwa sababu mbali ya kile kifungu cha 5(a) ambacho Mhe. Hamza Hassan alikisoma kilichozungumzia mgawanyo wa madaraka.

Mhe. Spika, unapokwenda katika kifungu cha 77(1) cha katiba yetu Mhe. Spika, kinasema, kutakua na Afisi ya Baraza la Wawakilishi itakayoongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi na itakua na nafasi za madaraka kama itakavyoidhinishwa na Tume ya utumishi wa Baraza la Wawakilishi.

Halafu kifungu cha (2) kinasema kutakua na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi ambayo itakua na uwezo wa kuwaajiri maofisa na watumishi wote wa Baraza, kuwapandisha vyeo, kuwachukulia hatua za kinidhamu na kufanyakazi nyengine zozote zitakazotungwa na sheria kuhusu utumishi katika Afisi ya Baraza, isipokua Katibu wa Baraza la Wawakilishi atateuliwa na Rais kwa mujibu wa kifungu cha 76 cha katiba.
Kifungu cha (3) Muundo na taratibu za Tume ya utumishi ya Baraza utakua kama utakavyoelezwa na sheria itakayotungwa kwa madhumuni hayo. Na

Kifungu cha (4) kinasema, Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria ya kuweka mfumo wa utawala na uendeshaji na mambo mengine yanayohusu Afisi ya Baraza la Wawakilishi. Hili la kifungu cha (4) ndilo ambalo Mhe. Hamza Hassan analishughulikia kutaka kuleta mswada, nafikiri wanasaidiana na Serikali kuona kama Serikali ama yeye alete, lakini madhumuni ni kuisaidia Serikali. Nilipo mimi zaidi ni katika hiki kifungu kidogo cha (2) yaani kifungu cha 77(2) cha katiba.

Mhe. Spika, kifungu hiki kimeweka madaraka yote ya kuhusu kusimamia watumishi wa Baraza la Wawakilishi kwa Tume hii, lakini hapa inaonekana Katibu Mkuu Kiongozi ndiye mwenye madaraka ya kutoa ruhusa ya kuajiriwa kwa mkataba kwa watu wote waliokua katika kada za utumishi wa umma, ikiwemo Baraza la Wasakilishi. Yanayopaswa ni kushauriana tu na kushauriwa Mhe. Spika, unayemshauri ana haki ya kukubali au kukataa ushauri. Kwa hivyo,

nadhani kwa mtazamo wangu hili linagongana na katiba. Namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu akija atusaidie ili tusije tukafanya maamuzi katika chombo chako ya kuvunja katiba yetu.

Mhe. Spika, sio hapo tu, lakini pia niendelee hapo hapo katika kifungu hichi ninachokijadili cha 60. Ukenda katika katiba yetu vile vile katika kifungu cha 118, kinasema bila kuathiri masharti ya katiba Tume za utumishi zilizotajwa ndani ya katiba zitakuwa na mamlaka yafuatayo.

(a) Kuajiri watu kushika nafasi za utumishi.
(b) Kuthibitisha ajira zao za utumishi.
(c) Kusitisha au kuachisha utumishi wao.
(d) Kupendekeza Serikalini mishahara na marupurupu ya watumishi wao. Na
(e) Mamlaka mengine yoyote zitakazopewa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Sasa Mhe. Spika, utaona hizi Tume nne, Tume ya utumishi Serikalini, Tume ya utumishi Baraza la Wawakilishi, Tume ya utumishi ya Mahakama na Tume ya utumishi ya idara maalum, kila moja imepewa mamlaka yake haya yaliyotajwa hapa. Sasa ukisema kwamba sasa zinashauriwa tu lakini mwenye mamlaka ni Katibu Mkuu Kiongozi. Je, Mhe. Spika, hapa hatukiuki katiba, nilikua naomba hili pia tulitizame sana.

Mhe. Spika, mbali ya hapo, kuna suala jengine la jumla lakini naliunganisha hapo kwa sababu hapo panazungumzwa madaraka ya Katibu Mkuu Kiongozi. Mhe. Spika, katika ile ibara niliyosema mwanzo na sijui hii katiba yetu inagongana. Kifungu cha 49(2) kinasema Katibu Mkuu Kiongozi atakua ndiye kiongozi wa utumishi wa umma kwa Zanzibar na hatoanza kazi zake mpaka atakapoapishwa na Rais.

Lakini ukija kwenye kifungu cha 116(1) cha katiba, kinasema kutakua na Kamisheni ya utumishi wa umma ambayo itakua ni chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za utumishi chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya utumishi wa umma kwa Zanzibar. Huku mamlaka Katibu Mkuu Kiongozi kafanywa ndio kiongozi mkuu wa utumishi wa umma, lakini huku kamisheni ya utumishi wa umma ndio chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za utumishi. Ni sawa, tumeambiwa kama ni *Regulator Authority* au ni *Regulator Board*. Lakini je, hapa hapana mchanganyiko na hili huko mbele Mhe. Mwanasheria Mkuu haoni kama kuna haja ya kulitazama na kufanya marekebisho hapa. Nilikua nadhani suala hili Mhe. Spika, tulitazame kwa makini sana ili kuepusha mgongano ambao unaweza ukatokea. Hilo kama nilivyosema linahusu kifungu cha (b).

Mhe. Spika, nadhani niseme la mwisho la jumla, kuhusu haya yaliyokuwepo ndani ya mswada kwa jumla nadhani nitakua nimemaliza. Namuomba vile vile Mhe. Mwanasheria Mkuu na Serikali kwa jumla walitazame suala moja Mhe. Spika, katika marekebisho ambayo yanaweza kuja baadae.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kamati yetu ndio inayoshughulika na Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala. Tuliwahi kukutana na Kamisheni ya Utumishi wa Umma, tukataka kuwasikiliza uzoefu wao katika kipindi hiki kifupi, walikua na malalamiko mengi sana ambayo tuliyazungumza na Mhe. Waziri na aliahidi kuyafuatilia.

Lakini moja walilolizungumza Mhe. Spika, ni kuhusu hadhi zao. Hebu hili suala kwa sababu umekuja mjadala huu basi tusaidiwe. Mhe. Spika, wamenukuu kifungu cha 111(5), kifungu hiki kinazungumzia malipo ya baadhi ya maafisa, na kile kinachofungua kifungu cha 111(1) kinasema, watumishi wa Serikali wanaohusika na masharti ya kifungu hiki, watalipwa mishahara na posho kama itavyoelezwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Sasa wao wanaacha yote katikati wanakwenda kwenye hiki cha (5), kinasema kifungu hiki kinawahusu Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais, Spika, Jaji Mkuu, Majaji wa Mahakama Kuu, Kadhi Mkuu, Wajumbe wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Mwanasheria Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Sasa hoja yao Mhe. Spika, wanasema hawa wengine waliotajwa hapa wote wana mishahara, wao wamefanywa kama vile ni bodi ya shirika, wanalipwa posho kwa mujibu wa vikao, hili linaleta msuguano mkubwa sana Mhe. Spika, na wao wametumia sana kifungu hiki cha katiba kwa sababu ndio wanapoegemea, hebu tupewe ufafanuzi usahihi uko wapi na kama kuna matatizo hili suala ni la kiutawala tuelimishwe lizungumzwe ili lipatiwe ufumbuzi.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, suala hili vile vile ni la jumla. Sijui kama wakubwa watatuambia siri yao. Mimi nilikua naomba kujua katika suala hili la jumla. Sheria hii inahusu utumishi wa umma na utumishi wa umma umefafanuliwa katika katiba kwenye tafsiri huku na wametofautishwa na watumishi wa kisiasa ambao wanajumuishwa Mawaziri.

Sasa Mhe. Spika, katika huu umbea umbea wetu wengine, mara nyengine husikia Waziri kaitwa na Katibu Mkuu Kiongozi, hebu leo tunaomba tuekewe sawa. Katibu Mkuu Kiongozi ana mamlaka ya kumwita Waziri. Kwa sababu ninavyojua mimi kwamba Wawaziri wanawajibika kwa Rais na pengine kwa sababu wasaidizi wake wa karibu ni Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wao wanaweza wakawaita, lakini Katibu Mkuu yeye kaandikwa katika katiba kama ni kiongozi wa utumishi wa umma. Sasa kama nilivyosema umbea umbea, lakini umbea pia sio sahihi watatuambia wenyewe. Lakini nilikua nataka kujua hivi Katibu Mkuu Kiongozi anayo mamlaka ya kumwita Waziri au naibu Waziri au haya ni mamlaka ya Rais, naomba aje atuweke sawa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na haya mapendekezo niliyoyatoa kama yatazingatiwa, basi naomba niseme kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe ninaowawakilisha hapa, naunga mkono hoja hii mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mawazo yangu mawili au matatu juu ya marekebisho ya sheria hii inayohusu utumishi wa umma, marekebisho ambayo ni mafupi lakini yamekua yakitolewa maelezo marefu.
Mhe. Spika, mimi kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuweza kuona haja ya kufanya marekebisho katika sheria hii. Pia amekua na kawaida ya kufanya marekebisho katika sheria mbali mbali katika yale maeneo ambayo yanakua na kasoro, hivyo nampongeza sana.

Moja kati ya jambo ambalo nimekua nikilizungumza sana Mhe. Spika, katika Baraza lako ni juu ya namna ya kuwasaidia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kujadili hizi sheria, hasa

wakati wa kujadili marekebisho ya sheria mbali mbali ambapo kwa wakati huu mara nyingi tumekua tukitumia Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya shughuli hiyo.
Mhe. Spika, katika kikao kilichopita niliwahi kujenga hoja ya aina hii ambapo niliiomba Serikali kwa mara nyengine wanapofanya marekebisho kama haya, basi angalau watutayarishie, kwa wakati ule waliita bango kitita au jadweli ambayo itakua iko wazi inaonesha kile kifungu ambacho ni cha zamani kilichokuwepo na ioneshe kile kifungu kipya ambacho kinataka kurekebishwa. Hii ina maana kwamba Waheshimiwa Wajumbe kama tunavyofahamu na sote tunajuana majukumu yetu, mambo yetu mengi vichwani tuliyokuwanayo, lakini itaturahisishia kujua Serikali inakusudia kurekebisha kifungu kipi na kilikua kinasemaje na kwa wakati huu.

Mhe. Spika, hili safari hii limekuja lakini halikuja kwa mujibu wa katiba hii. Kwa sababu katiba yetu hii ya mwaka 1984, inaeleza kwamba lugha rasmi itakayotumika katika chombo hiki ni Kiswahili. Sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu ametuletea bango kitita leo, tumepewa hapa. Lakini halikuandikwa kwa lugha rasmi ya Kiswahili, jambo ambalo huenda likatupa tabu kuelewa kile kilichokua kimekusudiwa.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu au Waziri yeyote wakati anapoleta *amendment* juu ya sheria yake, basi kwanza atuletee mapema hili bango kitita, tena liwe kwa lugha zote mbili, iwepo ya Kiingereza na iwepo ya Kiswahili, ili Waheshimiwa Wajumbe wapate uelewa, kwa sababu lengo letu ni kuelewa kile tunachokifanya. Sio vizuri Waheshimiwa Wajumbe wafanye mambo waliyokua hawana uhakika nayo au hawayaelewi.

Kwa hivyo, utakapoleta marekebisho au bango kitita kwa lugha Kiswahili, maana yake tabaan Kiswahili ndio lugha yetu tunaweza tukafahamu vizuri zaidi na zaidi ukizingatia kwamba lugha za kisheria za Kiingereza ni ngumu mno, labda kina Mhe. Ismail Jussa Ladhu ndio watakua wepesi wa kuzifahamu kwa sababu tayari wameshapitia katika fani kama ile.

Kwa hivyo, kwa mara nyengine tena nimuombe Mhe. Waziri, tunamshukuru ametuletea bango kitita leo, lakini wakati mwengine atakapofanya marekebisho madogo madogo, basi kwanza bango kitita lile mapema, tena liwe kwa lugha ya Kiswahili zaidi. Sio vibaya kama ikibidi kua la Kiingereza basi hakuna tatizo. Hilo ni moja.

Mhe. Spika, marekebisho haya ambayo yako mbele yetu, pengine au kama ndio ilivyo yana nia njema katika kurekebisha mambo yanayohusiana zaidi na utumishi wa umma. Lakini kama wenzangu walivyotangulia, suala hili la utumishi wa umma bado linaonekana lina mazonge, yaani lina utatautata na utata wenyewe kumekua kuna wasimamizi wengi, kumekua na vyombo vingi. Mimi hii Mhe. Spika, imekua inanipa wasi wasi juu ya namna ya ufanyaji wa kazi au namna ya kuwasimamia hawa watumishi wetu wa umma. Kama wenzangu walivyotafsiri katiba juu ya vifungu mbali mbali ambavyo vinazungumzia masuala ya utumishi wa umma, nidhahiri inaonekana kwamba kuna mkanganyiko.

Katika Katiba kifungu cha 116 ambacho baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wamekinukuu, kimeizungumzia Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwamba ndicho chombo cha juu kabisa chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote ya Utumishi wa Umma kwa Zanzibar.

Mhe.Spika, hiyo ni lugha ambayo iko wazi, yaani unapozungumzia chombo cha juu kabisa tunajua tafsiri yake nini, kwamba hakuna chengine. Lakini unapozungumzia suala la kuratibu, tunajua namna ya kuratibu ni nini, kusimamia masuala ya utumishi wa umma, sote tunafahamu nini madhumuni ya Katiba hii. *(Makofi)*

Lakini sheria hii inapoleta marekebisho na kuweka chombo chengine, ambapo ibara ya 47 kifungu (1) na (2) kinazungumzia kuanzishwa kwa Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma. Kwa kweli mmekuwa mkitusumbua na kutuchanganya.

Mhe.Spika, nina wasi wasi mchanganyo huu ambao Waheshimiwa Wajumbe wanaoupata sasa, unaweza ukavichanganya hata hivi vyombo vyenyewe. Lakini hatimae pia unaweza kuwachanganya watumishi wenyewe wa umma. *(Makofi)*

Mhe.Spika, naomba kunukuu ibara ya 47(1)

Ibara ya 47(1) (2) Kuanzishwa kwa Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma kinaeleza hivi:-

(1) "Kunaanzishwa Ofisi ambayo itajulikana kama ni Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma, ambayo itakuwa chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu, ambaye atakuwa Msaidizi Mkuu wa Katibu Mkuu Kiongozi kwa mambo yote yanayohusiana na Utumishi wa Umma.

(2) Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma itakuwa ni chombo cha kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Katibu Mkuu Kiongozi katika Utumishi wa Umma".

Mhe.Spika, mimi kwa kweli Mhe. Mwanasheria Mkuu wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi atupe ufafanuzi wa kutosha, yaani wa kina, tena atupe sababu ya sisi Waheshimiwa Wajumbe kukikubali kifungu hiki. Kwa hivyo, ni vyema atushawishi, atupe maelezo ya kina kwa ajili ya kututoa wasi wasi, ili tukubaliane na kuanzishwa kwa ofisi hii, vyenginevyo tutasema kwamba ofisi kwa hivi sasa isiwepo, kwa sababu tuna wasi wasi kuwa huenda ikatuchanganya katika *masuala mazima* ya kusimamia Watumishi wetu wa Umma. *(Makofi)*

Mhe.Spika, sisi tusingependa kuwe na mambo kama hayo, yaani tusingependa Mhe. Spika kwamba Baraza lako litumike kuanzisha sheria ambayo ina migongano. Hivyo ni vyema tungependa tupitishe sheria ambayo iko wazi, yenye kutoa majukumu kwa kila chombo, ili yanapotokea matatizo, basi tujue mtu gani wa kumshika katika matatizo ambayo yamejitokeza. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu, eneo jengine ambalo ningependa nilizungumzie ni juu ya eneo la tafsiri ya nafasi ya maalum, ambayo iko kwenye kifungu cha 3(b), Mhe. Spika, naomba nikinukuu.

Kifungu cha 3(b) Nafasi Maalum kinaeleza hivi:-

"Nafasi Maalum, maana yake ni Utumishi wa Umma kama

ilivyooneshwa katika kifungu cha 60 cha Sheria hii, ambapo wataalamu wake ni adimu au inahitajika watu wenye ujuzi na uzoefu maalum au kwa maoni ya Waziri nafasi hiyo inahitaji wataalamu maalum kutoka ndani au nje ya Zanzibar".

Mhe.Spika, tafsiri hii maana yake imetafsiriwa katika kifungu cha 60 cha marekebisho haya, ambapo kumeongezwa maneno kifungu cha 1(b), Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 60(1) (b) kinaeleza hivi:-

"Isipokuwa kwa nafasi maalum ambazo zitatangazwa kwa Waziri katika Gazeti Rasmi la Serikali".

Lakini katika kifungu hicho cha 60(5) Mhe.Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 60(5) kinaeleza hivi:-

"Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kushauriana na Tume husika anaweza kutoa ruhusa ya kuajiriwa kwa mkataba maalum kwa mtu ambaye ana sifa, utaalamu na uzoefu katika nafasi iliyotangazwa na Waziri chini ya kifungu cha 60(1) (b) cha Sheria".

Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, lakini malalamiko hayo pia yamekuwa yakijitokeza katika chombo chako hiki cha Baraza la Wawakilishi, kupitia wawakilishi wa wananchi juu ya kutoa ajira za mikataba, kwa wakati mwengine watu tunaowaita wataalamu. *(Makofi)*

Kwa mfano, huyu ni mtaalamu kwa hivyo anajazishwa mkataba, tayari ameshatumikia muda mrefu pengine wengine wameshapewa mpaka stahiki zao, lakini tunaitumia nafasi ya kuwaajiri upya kwa mikataba. Mhe.Spika, kwa kweli hili ni tatizo. *(Makofi)*

Mhe.Spika, mimi huwa najiuliza huko nyuma kama haya yalikuwa yakifanyika, lakini yalikuwa yakifanyika kwa sheria ipi, kwa sababu ni mambo ambayo yamezoeleka na yalikuwa yakilalamikiwa kwamba, kuna watu wameajiriwa, na Baraza lako hili limekuwa likipiga kelele. Sasa pale mwanzo kulikuwa kunatumika sheria ipi?

Kwa kweli ninao wasi wasi Mhe.Spika, kwamba kifungu hiki cha sheria kisije kikatumika vibaya, yaani Baraza hili lisije likatoa mamlaka ama kwa tume au kwa waziri kutumia nafasi hii vibaya, pengine tumeonekana sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunapiga kelele sana.

Kwa hivyo, tunatakiwa tutumie chombo hiki kwa ajili ya kuhalalisha mambo haya, ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na wananchi. Mhe.Spika, dhana ya kifungu hiki si mbaya, lakini inaweza ikatumika vibaya. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe.Mwanasheria Mkuu ambaye ametuletea marekebisho haya ni mazuri, lakini tunataka kuwe na uthabiti, kuwe na nia njema juu ya utekelezaji wa jambo hili. *(Makofi)*

Mhe.Spika, wananchi wetu wanaona, wanasikia, wanalalamika na kuna wengine hawana utaalamu wowote wanaajiriwa tunawajua wapo mitaani, tunao vijana wetu wengi ambao

tumewasomesha kwa gharama kubwa, wamefikia mpaka nafasi hizo kubwa, yaani wanazo *degrees*, lakini ziko mifukoni wanatembea nazo. Sasa tunaitumia nafasi hii kuwaajiri watu waliokuwa tayari wameshatumikia na tunawaacha vijana wetu wakizagaa. *(Makofi)*

Mhe.Spika, kwa kweli Mhe. Waziri ambaye kwa mujibu wa sheria hii amepewa mamlaka makubwa ya kuzisema hizo nafasi ambazo zinahitaji utaalamu, basi awe makini na sisi Wawakilishi wa wananchi tupo, pale tutakapoona yanaharibika tutasema, maana ndio kazi yetu tutamwambia. Vile vile tutatoa na mifano iliyo hai, ili tuone mambo pamoja na serikali yetu inakwenda vizuri na sheria tunazozipitisha hapa zinatumika kadri ya vile ambavyo zilivyokusudiwa. *(Makofi)*
Mhe.Spika, Katiba yetu inayo mambo mengi, yaani inahitaji marekebisho makubwa na sijui Mhe. Mwanasheria Mkuu anaiona. Kutokana na hali hiyo, basi nataka aje atuthibitishie hapa kwamba ameona matatizo yaliomo ndani ya Katiba yetu, kwa sababu yeye ni mtu ambaye tunamtegemea sana katika serikali hii kwa ajili ya kutushauri, sisi ndio tunaotunga Katiba hii.

Wakati tulipotunga Katiba hii kwa bahati mbaya Mhe. Mwanasheria Mkuu hakuwepo alikuwa Mkurugenzi wa Mashtaka, lakini tumetunga sisi kwa mikono yetu. Lakini tunasema leo kwamba Katiba hii pamoja na kwamba tumeitunga sisi, bado inayo mapungufu makubwa hasa katika maeneo ya utumishi wa umma na maeneo mengine. Kwa hivyo, tumuombe sana Mhe.Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, alione hilo, yaani atafute kila linalowezekana kwa ajili ya kuirekebisha sheria hii, ili iendane na wakati.

Kwa kweli isije ikafika pahala kwamba marekebisho ya Katiba hii yakaletwa kwa *motion* ya Mjumbe, mimi sipendelei hivyo, isipokuwa mara nyingi huwa napendelea kuwa *motion* zinazoletwa hapa zitoke serikalini, ili sisi tupate nafasi ya kuzichangia pamoja na kuzijadili, kuliko sasa kuitumia nafasi ya Mhe.Mjumbe kuleta mswada inakuwa haipendezi.

Mhe.Spika, ni vyema sheria hii ikaangaliwa upya, wapo watu wa kusaidia hapa kama vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ambaye kidogo mambo ya sheria anayafahamu, basi mnaweza kukaa pamoja na kuona ni maeneo gani yanayohitaji marekebisho. *(Makofi)*

Mhe.Spika, misingi mikubwa ya Katiba hii inazungumzia zaidi juu ya mgawanyo wa madaraka, yaani *separation of power*. Sasa kama tunazungumzia namna ya mgawanyo wa madaraka, basi tuwe na mgawanyo wa kweli, kila mmoja afanye kazi kwa mujibu wa Katiba hii pamoja na vifungu ambavyo vimo ndani ya Katiba. *(Makofi)*

Mhe.Spika, sina maelezo zaidi wenzangu wamechangia vya kutosha, isipokuwa na mimi nimeona nitoe mchango wangu juu ya mswada huu. Kwa hivyo, Mhe. Mwanasheria Mkuu wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi atupe ufafanuzi wa kutosha juu ya mambo haya, ili tuweze kuupitisha mswada huu. Kwa kweli hatuna wasi wasi juu ya marekebisho haya kama kutakuwa na nia safi ya kufanya marekebisho haya. *(Makofi)*

Mhe.Spika, naunga mkono hoja hii pamoja na marekebisho atakayofanya Mhe. Mwanasheria Mkuu, ili tuone kwamba tunazipanga sheria zetu vizuri kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar na taifa hili kwa jumla. Ahsante sana Mhe.Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipatia nafasi mchana wa leo kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Umma, kama alivyouwasilisha Mhe. Mwanasheria Mkuu ambaye ni mwalimu wangu.

Mhe.Spika, kabla sijaenda popote nakamata mpenzi wangu Katiba.Mhe. Salmin Awadh Salmin ambaye amemaliza kuchangia hivi punde, alisema kuwa kuna wengine ambao watakaoweza kumsaidia Mhe.Mwanasheria Mkuu kuonesha maeneo ya Katiba yenye kasoro na amewataja hapa kama vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Lakini amemsahau Mhe.Mjumbe mmoja ambaye angeweza kusaidia katika Katiba hii, ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mwakilishi wa Jimbo la Kitope. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe.Spika, nilishukuru sana Baraza lako hili kwa kupitia wafadhili wetu wa *UNDP* kwa kutupa taaluma nzuri sana. Kwa kweli nimepata taaluma nzuri sana, Mhe.Spika hivi sasa Katiba hii naijua juu chini, chini juu. *(Makofi)*

Nakubaliana na wenzangu kwamba kweli kuna maeneo mengi ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho, hayo yapo na tutaendelea huko mbele na kuona ni wajibu na wakati umefika hivi sasa.

Mhe.Spika, usione ajabu Mhe.Makame Mshimba Mbarouk akaja na Hoja Binafsi ya kubadilisha sheria hii, kwa sababu uwezo ninao na Katiba nimeisoma na nimekaa kwenye hoteli ya kuniliwaza fikra pamoja na mawazo na kuweza kusoma Katiba hii kwa muda wote. *(Makofi)*

Sasa nakwenda kwenye mswada wenyewe nikianza na ukurasa wa 51 kwenye kifungu cha 4(a) kinachosema kufuta aya. Mhe.Spika, nilipoanza kusoma chuoni neno aya huwa nashituka sana kuona inatiwa kwenye mkataba kama huu, kwa sababu ukisema aya ni neno kubwa sana na wala halitumiki sehemu ovyo ovyo Mhe. Spika, hiyo ni lazima aya itumike mule inamotakiwa kwenye Kitabu chetu cha *Qur-an* Kitukufu.

Kwa hiyo, neno hili tukilitia kwenye makabrasha haya ya miswada na ambayo miswada hii Mhe. Spika, wakubwa tunashindwa kuitekeleza na hapa tafsiri huwa haiwi nzuri, yaani ni dhambi kubwa. *(Makofi)*

Mhe.Spika, tusicheze michezo hii kabisa, nadhani ni vyema Mhe. Mwanasheria Mkuu akatutafutia lugha ambayo itakayoweza kutuongoza hapa na sio neno la aya, kwa sababu Mhe.Spika ukitumia neno la aya, mwili unanisisimka hapa, kwani si kitu cha mchezo. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli mswada huu unamlenga mwananchi, watumishi wenyewe. Mhe.Spika, nikiendelea huko mbele utaona kweli kuwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aliposema kuwa neno hili la aya lisitumike kwa sababu hiyo. Mhe.Spika, nimeshindwa kusema kuwa nitaunga mkono mswada huu, bado sijaamua hivyo, kwa sababu nimo katika kuuchambua na baadae ndipo nitakaposema kwamba nitauchangia.

Mhe.Spika, nikiendelea kwenye kifungu cha 5 kinachozungumia kuhusu Kamisheni isiwe zaidi ya miezi mitatu kumaliza kwa mwaka wa fedha. Mhe. Spika, jana tulikuwa na watu wa Asasi za

Kiraia (AZAKI), kwa nini Mhe. Spika tusianzie hapa na tukajaribu kuwashajihisha hapa, ili kuungana nao pamoja na kutusaidia mwisho wa mwaka katika kutengeneza fedha zetu za bajeti, ili mara hii mkaweza kutuletea bajeti iliyokuwa nzuri.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika kwa mujibu wa sheria zako ulivyobobea nadhani ni vyema tuwaingize na hapa tuone, na waweze kutusaidia, ili sheria iwe nzuri zaidi, na ioneshe kwamba hizi Asasi za Kiraia (AZAKI) tumezisaidia vilivyo na tumepata michango yao.

Kwa kweli mara nyingi sana uzoefu unaonesha kuwa tunazidharau sana, kwa sababu hawa watu wanaakili za mambo au fani mbali mbali, sasa unapozikusanya pamoja, basi unaweza kupata kitu ambacho ni kizuri (*cream*) kabisa na kitaweza kusaidia serikali yetu katika mwaka wa fedha (bajeti).

Mhe.Spika, historia ni kwamba hata sisi Waheshimiwa Wajumbe wa baraza la Wawakilishi tunakuja hapa na kutetea tu, yaani hatushirikishwi kwenye hizo bajeti, sawa. Lakini hivi sasa tugeuke na hawa wenzetu tuwashirikishe, ili bajeti inapokuja tuweze kuichangia vizuri Mhe.Spika.Nadhani suala hili tuliangalie vizuri Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, ili kuweza kutufikisha pahala pazuri.

Kifungu cha 47(1) Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 47(1) kinaeleza hivi:-

> "Kunaanzishwa Ofisi ambayo itajulikana kama ni Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma, ambayo itakuwa chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu, ambaye atakuwa Msaidizi Mkuu wa Katibu Mkuu Kiongozi kwa mambo yote yanayohusiana na Utumishi wa Umma".

Mhe.Spika, Katibu Mkuu Kiongozi naona tunazidi kumpa mambo ambayo baadaye yataleta athari. Kwa kweli sehemu hizi ni nyeti sana Mhe. Spika, Katibu Mkuu Kiongozi tumeshampa madaraka makubwa, hebu mambo mengine tumpunguzieni, tusiendelee kumpa madaraka mengi na mwisho Mhe. Spika, ni kufika pahala la kuvaa koti na kujisikia vyengine na huko mbele tutakuja kuona jinsi gani madaraka haya makubwa tunavyompa mtu.

Kwa mfano, Mhe.Ismail Jussa Ladhu amesema hapa kuwa leo inakuwaje Katibu Mkuu Kiongozi anamwita Waziri. Mhe.Spika, ningeomba tutafute njia nyengine angalau tuweze kumpunguzia haya madaraka na tumtafutie sehemu nyengine.

Mhe.Spika, nikiendelea na mchango wangu katika mswada huu pengine naweza kwenda mbele na baadaye kurudi nyuma. Tukiangalia ukurasa wa 53 kifungu 60(5) Mhe.Spika naomba kunukuu.

Kifungu 60(5) kinaeleza hivi:-

> "Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kushauriana na Tume husika, anaweza kutoa ruhusa ya kuajiriwa kwa mkataba maalum kwa mtu ambaye ana sifa, utaalamu

wa uzoefu katika nafasi iliyotangazwa na Waziri chini ya kifungu cha 60(1) (b) cha Sheria hii".

Mhe.Spika, hii ni hatari kwa sababu huku tumesema kuwa tusimuongezee madaraka na leo hapa tunampa. Kwa kweli hapa ndipo patakapokuwa na kasoro kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Kwa mfano, hivi sasa wapo watu na ukweli tuuseme, kwa sababu tukisema ukweli tunanuniwa huko nje tunaambiwa watu wale hawapendi Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Wakati mwengine tunaambiwa hivi sasa fulani na fulani hafai. *(Makofi)*

Sasa kitu hiki kinanishangaza sana Mhe. Spika, kwa sababu watu wapo ambao wenye uzoefu mzuri na mpaka leo huo mkataba maalum hawakupewa na wanakwenda kupewa watu hawana uzoefu, isipokuwa kwa kuwa mtu rafiki yake fulani.

Mhe.Spika, ndipo pale niliposema kwamba Katibu Mkuu Kiongozi hafai kupewa madaraka makubwa, hili tulikubali Waheshimiwa Wajumbe na tukasimu mambo mengine kwani wako wengi wenye taaluma, yaani wenye uwezo wa kufanya mambo kama haya.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe.Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba akae naye vizuri Mhe.Rais na umwambie hapa *stop* twende kwengine na tutafute njia nyengine ambayo itakayoweza kutusaidia. Mhe. Spika, tunamtaka awe Katibu Mkuu Kiongozi na wala sio aondoshwe, hapana lakini yale madaraka yasizidi kuwa mengi, kwa sababu mtu ukimpa madaraka mengi. Kwa mfano, kuna wengine ilikuwa uwaziri hawajaupata, basi pale walipopata ule uwaziri tu wametugeukia. Lakini sina maana hiyo kama mimi nikipata uwaziri nitawageukia wenzangu wa *backbenchers* sifanyi utumbo huo hata siku moja, isipokuwa nitakuwa nao tena nitakubali wanishauri kila wakati na ndipo nitakapofika pahala uwaziri wangu utakuwa nautekeleza vizuri. *(Makofi)*

Mhe.Spika, nikizungumzia kuhusu kifungu cha kuhamishwa wafanyakazi wa Utumishi wa Umma kutoka wizara au ofisi nyengine ndani ya utumishi wa umma kufanywa na Katibu Mkuu wa Utumishi wa Umma, au baada ya kushauriana na Watendaji Wakuu wa Taasisi.

Mhe.Spika, leo nimepokea kesi wakati nilipokuwa nakunywa chai kule hotelini, nilipokea kesi ya kusikitisha sana. Kwa kweli alikuja mama mmoja na kusikitika kwamba kifungu hiki hakikumtendea haki, basi yeye alilia na mimi ikanibini nilie, sasa natafuta nani wa kutunyamazisha hajulikani. *(Makofi)*

Mhe.Spika, ni masikini wa Mungu amefanyakazi hapa Idara ya Anga, yaani Uwanja wa Ndege ana miaka 20 ya kufanyakazi pale, watoto wake si chini ya 10 mpaka 12 kama sijakosea. Mhe.Spika, mshahara wetu unaujua ulivyo wa Kizanzibari. Mhe.Spika, mama huyu hajui kosa lake alilolifanya mpaka akahamishwa.

Sasa kifungu hiki kinaponishtua na ndipo pale niliposema kwamba sipendi kuunga mkono kitu ambacho baadae kinageuka, kwa sababu tunatunga sheria vizuri kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, lakini huko mbele sheria hazifanyi kazi vizuri na wala hatuwafanyii haki wananchi.

Mama huyu amepewa barua na Mkurugenzi aende kwa Katibu, sasa barua ile haioneshi kama ni ya Katibu, yaani anapigwa *dane dane* na mwisho wa habari anapelekwa UUB akabebe zana nzito anaweza wapi mwanamke kubeba vyuma vile, hebu niambie Mhe. Spika. Hatimaye huko kwenye meza masikini ya Mungu, anajikuta ananing'inia si popo wala si ndege na sheria hii imemtendea haki wapi?

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe. Spika, siungi mkono mpaka huyu mama nihakikishe amewekwa katika nafasi nzuri, kwa kifungu hiki sikubaliani nacho.

Mhe.Spika, nilikwambia kwamba nataka kwenda Makka, uliniambia kuwa Makka ni nchi ya kutembelea, nakubali, lakini sasa nataka kwenda Kuhiji. Mhe.Mwanasheria Mkuu uliniambia kwenda Makka ni nchi ya kutembea kama nchi nyengine, nakubaliana na wewe Mwanasheria. Lakini kwa kifungu hiki ndicho kitakachonipeleka mimi sasa kwenda Kuhiji, kwa sababu kwenda Kuhiji ni miongoni mwa Nguzo za Kiislamu ambazo Mwenyezi Mungu ameziweka, yaani kila Muislamu atakavyoonja mauti, basi ni lazima aende Kuhiji. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa leo Mhe. Spika, niukubali mswada huu wakati mwanamama nimemuona mwenyewe *physical* kabisa anakuja hapa hotelini analia, basi na mimi Mhe. Spika ikabidi nilie, nani mnyamazishaji, sijui nani.

Kwa hivyo, Mhe.Spika nikaona hapana, yaani hebu tuangalie hii umesema mwenyewe kuhusu uhamisho wa wafanyakazi kwa utumishi wa umma, utatoka kwa wizara au ofisi moja kwenda wizara au ofisi kwenda nyengine, yeye ndivyo alivyofanyiwa hivyo lakini haikwenda kwa utaratibu.

Sasa yule Mkurugenzi wa UUB masikini wa Mungu amekaa tu kwa ile imani yake ndio amemuweka kwenye chumba fulani, yaani hajui naye afanye nini, nadhani ni vyema leo tukauliza mafao yake atayapata wapi.

Mhe.Spika, hizi sheria tunazozileta tuziangalie jamani, tuwe *very careful* kweli tusifanye mchezo, yaani lazima tuwe na uhakika wa hili jambo tunalolipitisha, na halafu tunakwenda kulifanyia kazi kwa wananchi, *otherwise* Mhe. Spika tutakwenda na maji. *(Makofi)*

Mhe.Spika pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tusifanye mchezo, kwa kweli mambo haya tunayopitisha hapa tunawalenga wale wananchi dhalili waliotupa kura, na wala tusiopoge mtu. Kwa mfano, mimi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk nimeshajitolea (*famalillah*) kwamba, sitomwacha mtu yeyote anayekwenda ovyo nitamsema katika Baraza hili. *(Makofi).*

Sasa tena wengine wanataka umaarufa kwa Mhe. Rais, wanasema kwamba Mhe. Makame Mshimba Mbarouk tena watu wakubwa wenye heshima zao, kule kwenye Bango Kitita kunatakiwa maendeleo sio Mshimba, na wala msimpeleke Mshimba kule, isipokuwa pelekeni maendeleo yanayotakiwa kwa jamii. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini namshukuru sana Mhe. Rais, ni mtu msikivu na wala hakubali majungu ya hapa na pale ya kupelekwa, kitu hiki kinanishangaza sana. *(Makofi)*

Mhe.Spika, tujaribu sana tunapoleta sheria, na Mhe. Salmin Awadh Salmin amesema kwamba, hii *level* ni ya wataalamu, kweli mimi pamoja na utaalamu wangu nimejaribu ku-*peruzi* hapa naokota moja moja tu na ndio maana mengine nayafanyia wepesi kwa sababu sitaki kuji-*commit* ndani yake, kwani mna kitu mtego.

Kwa kweli Mhe.Mwanasheria Mkuu ni mtaalamu sana, Mhe. Spika na mtu sifa yake mpe, na ndiye mtu wa mwanzo katika Baraza hili kumpa sifa basi atakuwa ni yeye huyu, lakini waliobakia wote sitoi sifa sasa, kwa sababu ni vitu ambavyo vinaendana na wakati lakini sheria haifuatwi ndio tatizo letu.

Mhe. Spika, tumesema habari ya watu kuwapa mkataba ni kweli kwa sababu sasa hivi natoa mfano, Wizara ya Majenzi sasa hivi wataalam hamna lakini tunaona shida sana kumtafuta mtu ambaye ana uzoefu pale tukampa mkataba maalum mpaka leo wanagwaya gwaya hakuna pale wataalam, tutakaa muda geni kuwatafuta wengine. Lakini wapo wazee tayari wana akili zinafanya kazi ni muda tu uliopita, kwa mfano pale yule Mkurugenzi aliyepita wa upimaji kwa nini tusimrejeshe tusimpe mkataba maalum kwa nini tusimpe, basi tu kwa kuwa mtu anasema hamtaki basi sasa tunakwenda wapi si ndo hatari yenyewe ninayosema hii Mhe. Spika, wapo wataalam wengi tu pale Idara ya Ardhi tumewaondoa kwa chuki zetu wenyewe za ubinafsi kitu kinachosikitisha sana hiki, tumewaondoa kwa sababu za chuki binafsi sio kitaaluma kama huyu mtu hafai kafika muda taaluma yake imegonga ukuta haiwezekani basi tu mtu madhali humpendi siku hizi unaambiwa ondoka.

Hiyo ni sawa sawa na mimi ukija ukisikia Mshimba hatumtaki tunaondoa jimbo la Kitope lakini si kwa wananchi kwa kuwa kiongozi kasema tu, ni haki yako kusema sasa hii ndio inayotukuta, wataalam tunao lakini nafsi ya mtu tu au nafsi za watu tu basi.

Mhe. Spika, mimi sitaki kukwambia mengi mifano mingine tulikuwa nayo humu humu kumtafuta Katibu wetu wa Baraza wala tusiende mbali, ilitupa shida sana kumpaka Katibu wa Baraza na nyote mnajua hapa, hatimae lililoandikwa na Mwenyezi Mungu basi litakuja ni sawa sawa na kuwa Mwenyezi Mungu kaandika Makame Mshimba kuna siku atakuwa Waziri basi halifutiki hata Mansour akikataa basi mimi nitaingia tu, aliandikalo Mungu Mhe. Spika, halifutiki hata siku moja mseme Mshimba wee lakini iko siku nitachukua Waziri wa Kilimo ipo siku tu.

Mhe. Spika, nikiingia katika kifungu cha 7 kifungu hiki kinasema.

> *Bila ya kujali masharti ya sheria hii chombo maalum cha serikali kinachohusika na usimamizi na uhamisho wa kada maalum ya utumishi kwa taaluma ambayo*

sasa unaona mambo ya Mheshimiwa hayo, hebu Mwanasheria maana yake hapa kila eneo watu wa kaskazini wana lugha yao, watu wa Makunduchi wana lugha yao na watu wengine wana lugha yao na Baraza la Wawakilishi litakuwa na lugha yake, Wanasheria watakuwa na lugha yao.
Lakini kuna siku moja kuna mtu mmoja alisema kuwa unaweza kusema lugha ya katiba lakini ndani yake ikasomeka tafsiri nyengine si kweli mimi nakataa, tafsiri itakuwa ni ile ile tu leo ukiniuliza Mhe. Mshimba nini kazi yake nitakwambia mimi kazi yangu, twenda kwenye kifungu

cha 98 ukurasa wa 59 unasema nini. Haifutiki ile Mhe. Spika ndio mimi mzimamizi na mpitishaji wa bajeti hakuna mwengine hatokezei mwengine.

Na kipi ninachokisema mimi hapa Mheshimiwa twenda ukurasa mwengine Na. 5(a) hebu iangalie inasemaje Mheshimiwa, sidhani kama kuna taasisi nyengine itakayoniingilia katika usemaji wangu nina fursa kina na kila kitu, lakini leo ukisema hapa kesho unaitwa wapi sijui ukadhibitiwe, hii inauma sana tena sana.

Mhe. Spika, huyu mama hakutendewa haki katika kifungu hiki na naomba sana Mwanasheria kwa kuwa wewe ndio msimamizi mkuu wa sheria hizi hebu tutafute njia ya kuweza kumsaidia huyu ili na mimi niseme nakuunga mkono. Ni aibu sana kama mimi sikukuunga mkono wewe mwanasheria wangu, inasikitisha ni mama aliyefanya kazi miaka ishirini kazini ameondoshwa kwa kosa ambalo halijulikani kwa mujibu wa sheria za kanuni za kazi lakini amesema ameondoshwa tu na kuondoshwa kwake amepewa barua ukiona hiyo barua utacheka, haijamu-*address* Katibu Mkuu kama kuonesha kama barua hii nimemleta huyu mtu kwa utovu wa nidhamu moja mbili tatu na tunaomba abadilishwe sehemu nyengine haijamuonyesha hivyo. Yeye kapewa barua tu ya kumhamisha yeye, sasa barua imesema imemuhamisha na kumpeleka katika Wizara ya Miundombinu akafanye nini kule.

Ndio maana nikasema kifungu hiki tukiangalieni vizuri leo tunakipitisha hapa lakini kabla hatujakipitisha huko nyuma kumeshapita maovu tayari. Mimi huwa nashindwa sana kupitisha miswada yako nataka sana kupitisha lakini inashinda kutokana na hali halisi ilivyokuwa, tunasema hapa kupitisha vizuri, tunaunga mkono asilimia kwa mia lakini utekelezaji wake unakwenda kinyume kimbele.

Sasa mimi Mheshimiwa wangu nataka nikuunge mkono asilimia zote kwa sababu siku hizi wananchi wa Jimbo la Kitope wameniambia na wamenipa ilani kubwa wamesema Mheshimiwa ukiona mswada ambao hauturidhishi sisi wananchi wa Kitope basi usiunge mkono tuko radhi na wewe na mimi nakubali. Nakubaliana nao na nawasikiliza kweli kweli kwa sababu wao ndio sheria ile itakayowapiga wao sasa hatimae mimi nitakwenda kuwatetea wapi wakati mwenyewe nimeshapitisha.

Kwa hivyo Mwanasheria nakuomba sana kifungu hiki njoo unijibu vizuri niridhike ili wananchi wa Kitope wakusikie kuwa utaratibu unasema hivi, moja mbili tatu kwa maana hiyo huyo mama bado hajaondoshwa au hajaweza kuondosheka kwa mujibu wa sheria atakuwepo hapo hapo Idara ya Anga, hapo mwanasheria nitakwambia *well and good*. Lakini vyengine vyovyote tutakuwa na mashaka nayo sasa mimi sikuungi mkono mpaka utakapokuja kuniambia na wewe una sifa moja nzuri sana mwanasheria wangu unajibu vizuri hiyo sifa nakupa. Hali kadhalika yule mtu hajaridhika na lile jibu, basi anakuwa anacheka anajua hapa nimepigwa na chini lakini basi.

Mhe. Spika: Mhe. Makame Mbarouk Mshimba jitahidi sana uzungumze na kiti.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nakutizama sana kwenye kiti chako inabidi sasa nivae miwani ili nikuone zaidi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia namuomba sana Mhe. Mwanasheria sasa naona wote hapa nilikuwa siwaone lakini wamerudi, naomba atakapokuja hapa kutupa majibu kwa kifungu hiki naomba aweze kutusaidia sana ili watumishi wetu wengine linapotokezea tatizo kama hili wajue waanzie wapi *procces* zao ili weweze kufika pale wasipoteze haki zao na wapate uhamisho ulio halali na unaotambulikana baadaye akitokezea matatizo ikawa mambo ya kuchanganyika.

Kwa hayo machache nangojea hoja nzuri ndio niunge mkono. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi niseme mawili matatu kuhusu mswada huu ambao ni mfupi kidogo, kwa mimi niliyekuwa sio mtaalam wa kusema basi nitachukua muda mfupi sana kwa sababu mswada wenyewe nao ni mfupi sana.

Mhe. Spika, kwanza naipongeza serikali kwa kuangalia uwezekano sasa wa kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali, kwa kweli hili ni jambo la kawaida kwa sababu sheria yoyote inayotungwa na binaadam basi mbele ya safari utakuja kuikuta ina mapungufu ya hapa na pale, kwa hivyo ni vyema kujanga utamaduni huo wa kufanya marekebisho ya sheria zetu pale ambapo tunahisi sasa sheria zetu zina mapungufu.

Mimi nilikuwa nadhani sana kwamba marekebisho ya sheria hii ya Utumishi wa Umma nilikuwa nadhani sana sheria hii ingewasilishwa na waziri wa utumishi wa umma kuliko mwanasheria mkuu, nasema hivi kwa sababu takriban sekta zote za serikali zina sheria mbali mbali na sheria nyingi kuna haja sasa ya kuzifanyia marekebisho zina mapungufu ya hapa na pale. Sasa tukisema kwamba kila sheria zina mapungufu tumuachie kazi Mwanasheria Mkuu kwa hili nafikiri atakuwa nakazi kubwa sana, sasa nilikuwa nadhani zile sekta husika basi wenyewe ndio wa-*propose* marekebisho kuliko kupewa mwanasheria mkuu kila kazi, sijui pengine ndio kazi zake lakini nahisi atakuwa na kazi kubwa sana.

Mhe. Spika, tokea nilipopata mswada huu nilikuwa nauangalia sana lakini siku zote marekebisho ya Sheria huwezi kuyafahamu vizuri mpaka uwe na ile sheria mama yenyewe inayorekebishwa, sasa mimi niliangalia mara ya kwanza nikaona giza, mara ya pili nikaona giza.

Lakini leo tulipopatiwa kuna kile kifungu kinachofanywa marekebisho na kabla ya marekebisho tunatakiwa tuyaeleze, sasa baada ya kupata hii kwa kweli nimeanza kufahamu vizuri sana huu mswada, kwa hivyo nilikuwa naomba sana tutakapopelekewa marekebisho ya Sheria basi serikali ijitahidi kutuletea na ile sheria ambayo inahitaji kufanyiwa marekebisho maana hivi sheria tunazo lakini kuitafuta mpaka kuiona mara nyengine inakuwa ni kazi kubwa sana, lakini wenzetu waliokuwa nayo karibu sana basi wakituletea inakuwa ni jambo zuri sana.

Mhe. Spika, utumishi wa **umme** nafikiri tukubali kwamba pamoja na marekebisho yanayofanywa mara kwa mara lakini bado kuna changamoto kubwa, na mimi nilikuwa nadhani serikali iangalie kwa makini zaidi kwa sababu ndani ya utumishi wa umme ndiko kwenye ajira na vijana wetu sasa hivi wanasoma kwa bidii Mhe. Hamza Hassan Juma kasema hapa ukisema waliokuwa na *degree* sasa hivi basi utakuwa huna nafasi ya kutia mguu, halikadhalika ukitaka *Masters* bado zinahangaika tu huko mitaani.

Lakini tatizo tunalokabiliana nalo hawa vijana wana elimu za ina gani na serikali inahitaji watumishi wa aina gani, sasa hii nasema bado nchi yetu ina changamoto vijana wetu wengi wanaelekea kusoma yale masomo hatimae hayana *market* katika soko la ajira, kwa hivyo na hili nalo kama sera ipo basi ifanyiwe marekebisho kulingana na soko liliopo sasa hivi na vijana wetu wanaosoma basi waelekezwe kusoma huko kwenye soko, wasiwe wanakusanya elimu lakini baadae hatuwezi kuzitumia kwa sababu ya wingi wa watu wa aina ile. Sasa nasema hilo ni moja katika mambo ambayo ni muhimu na yaangaliwe.

Sasa nikienda kwenye vifungu vya mswada huu labda nianze kifungu cha 5 ambacho mimi nitatumia hii kopi ya kiingereza zaidi kuliko ya Kiswahili, kwa sababu hii ya kiingereza kama nilivyosema ina ile *comparison* ya kifungu kabla ya marekebisho na baada ya marekebisho imenivutia sana, sasa Kifungu cha 5 kinarekebisha kifungu cha 29 cha sheria mama.

Naomba ninukuu kidogo hapa inasema.

> Kabla ya marekebisho *the commission shall not lead than three month up the end of each financial year, prepare and submit to the President and copy to the minister and annual report on condition and efficiency of the public service.*

Sasa baada ya marekebisho hayo hiki kinasema kwamba *commission* itaandaa ripoti ya kila mwaka miezi mitatu baada ya kumaliza kima la mwaka kuandaa ripoti na kupeleka kwa Waziri sasa na waziri nae ndani ya siku 30 anatakiwa aipeleke kwa Rais, sasa mimi bado nashawishika kwamba hiki kifungu kabla ya marekebisho basi ni kizuri zaidi kuliko baada ya haya marekebisho, nasema hivyo kwa sababu Mwenyekiti wa kamisheni hii anateuliwa na Rais, kwa hivyo kamisheni hii itakuwa inawajibika kwa Rais moja kwa moja ninavyohisi mimi haiwajibiki kwa waziri.

Kwa hivyo ripoti ipelekwe kwa Rais na kopi ipelekwe kwa Waziri nakubali kwamba kabla ya kupelekwa kwa Baraza la Wawakilishi kwanza upite mwezi mmoja ambao utampa fursa Rais kuipitia ile ripoti, sambamba na waziri na hatimaye ndio itapelekwa kwa Baraza la Wawakilishi. Lakini ukisema apelekewe waziri hiki kifungu kinampa fursa ya kukaa na ripoti ile mwezi mmoja, yeye atakuwa anaisoma lakini nina hakika hawezi kufanya marekebisho yoyote halafu akimaliza anampelekea Rais na Rais anapeleka Baraza la Wawakilishi kwanza Rais hajawekewa muda wa kupitia ile ripoti. Kwa hivyo nafikiri kabla ya marekebisho ripoti hii apelekewe rais na waziri apelekewe kopi wakati rais anapata muwa wa kuipitia na waziri nae kwa sababu kopi anayo anapata muda wa kuipitia na baadae ndio inakuja Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, marekebisho mengine ni ya kifungu cha 6 cha mswada ambacho ni marekebisho ya kifungu cha 47 mimi nadhani hapa labda nimpongeze Mwanasheria Mkuu kwa kuongeza kitu kwa sababu kaongeza kitu tu, tukiangalia pale tayari Ofisi hii ipo na ipo chini ya Katibu Mkuu Utumishi wa Umma, lakini sasa kilichofanywa ni kwamba Katibu Mkuu wa Utumishi wa Umma anaunganishwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwamba sasa yeye anakuwa msaidizi wa Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala yote ya utumishi wa umma. Sasa ni kama kuweka kiungo kati ya Katibu Mkuu Utumishi wa Umma na Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya utumishi wa umma nafikiri ni jambo zuri, kwa sababu lilikuwa lipo hewani.

Lakini katika sekta ya utumishi wa umma tayari kiungo kipo ndio nikasema labda kuna haja ya kufanya marekebisho ya sheria nyingi sana, kwa sababu sasa mimi nafikiri katibu Mkuu Kiongozi ashungulikie utumishi wa umma pekee takriban yeye anashughulikia masuala yote ya serikali, kwa hivyo sasa huenda halafu kukawa na haja na sekta nyengine sasa Makatibu wakuu wa sekta nyengine tukaja tukaona sehemu nyengine na wao kuwa wasaidizi kwa maandishi, maana *automatically* ya wasaidizi wa Katibu Wakuu viongozi lakini sio kwa maandishi kama ilivyowekwa katibu Utumishi wa Umma. Sasa nafikiri kutakuja kuwa na haja ya baadae makatibu Wakuu wa sekta nyengine na wao sasa tufanye maandishi yatakayowafanya wawe ni wasaidizi wa Katibu Mkuu kiongozi katika masuala yao ya sekta.

Mhe. Spika, mimi binafsi kana nilivyosema mwanzo sina mchango mkubwa kwa sababu ya udogo wa huu mswada ulivyo, lakini nilisema nisimame ili nitoe barka kidogo na hatimae niukubali mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahasante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia marekebisho mbali mbali ambayo tokea juzi na leo tunayachangia, kwanza na mimi nichukue nafasi hii niipongeze serikali kwa kuona kwamba kuna haja ya marekebisho mbali mbali ambayo yanaweza kusaidia katika sheira mama.

Lakini Mhe. Spika, nitaungana na wenzangu wale ambao wametangulia kuchangia kwanza niseme kwamba hii katiba yetu ya Zanzibar lazima tuhakikishe tunaipitia tena ili kurekebisha katiba hii isipingane na sheria ambazo tunazitunga humu, inaonesha kwamba katiba yetu kuna baadhi ya mambo hayawiani na sheria ambazo tunazitunga katika Baraza la Wawakilishi. Katiba inasema vyake na sheria inasema vyake, niiombe serikali ipitie upya Katiba ya Zanzibar ili kuhakikisha vile vipengele ambavyo haviwiyani na sheria ambazo tunazitunga basi kuwe na marekebisho ambayo kwa mintarafu ya kusaidia na kutokakugongana na katiba yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, tumesema hapa mgawanyo wa madaraka hebu tujiulize huu mgawanyo wa madaraka tunaufanya kweli kwa baadhi ya sehemu, na kama hatuufanyi ni sababu zipi ambazo zinatufanya kwamba mgawanyo huu wa madaraka tusifuate taratibu na sheria, ilikuwa nasema hayo Mhe. Mwanasheria aje anisaidie.

Mhe. Spika, mswada huu vipengele vingi ni vya utumishi wa umma serikalini, mimi niseme tu amenifilisi kidogo Mhe. Makame Mbarouk Mshimba huyo mototo ambae amemzungumza hapa ni kweli, kwa sababu amenifika mimi nikaona sio kamati yangu nimpelekee mwenye kamati yake na nashukuru wamemsikiliza na mimi nazungumza tena.

Mhe. Spika, hili sio tatizo la Wizara moja ni matatizo ya wizara nyingi ambazo zinatoa uhamisho holela holela kwa mintarafu ya mtu binafsi, hizi kamati zako hizi zinapokwenda kuangalia baadhi ya mambo basi aghalabu katika watendaji wengine au wafanyakazi wengine wakisema ule ukweli basi siku ya pili anaondoshwa pale alipo kwa sababu kasema ukweli, kazungumza kitu ambacho kitaleta maslahi kwa wananchi.

Sasa naomba sana Mhe. Waziri tutakapopitisha haya marekebisho awe muangalifu katika sehemu mbali mbali kuhusu uhamisho wa kiholela holela na kuonewa wafanyakazi, nasema haya

kwa ushahidi sisemi haya kwamba sina ushahidi. Ni vyema katika mawizara ikatizamwa juhudi ya mtu ya kazi na maendeleo yake ya kujisomesha ili kuhakikisha tusimuenee mfanyakazi ambae ana jitihada katika sehemu yake ya kazi.

Mhe. Spika, tunajitahidi sana katika kusomesha vijana wetu lakini la kushangaza kwamba katika Mawizara yetu unapokwenda kutembelea ukauliza mtu hasa katika seksheni yake kama ni *Wahandisi* kama ni daktari au ni mtu mwengine, lakini utasikia kwamba serikali ipo mbioni sasa sijui mbio hizi za marason au mbio gani sijui, utasikia serikali iko mbioni kutafuta mtaalam wa kiasi hiki na sasa hivi tumeshatenga lakini ukenda tena hupati jawabu sahihi. Naiomba sana serikali Mhe. Spika, sasa hivi hebu tubadilike ni wakati wa sayansi na teknolojia, naomba kila wizara ambayo kitengo tunahisi kinataka mtaalam huyu basi wizara husika ihakikishe inapeleka watu wale kwenda kusomea kitu ambacho chenye uhakika.

Lakini kuna madhambi mengine yanatendeka huko nyuma kidogo tumesomesha madaktari wengi sana, tumesomesha *Wahandisi* wengi sana watu wa fani mbali mbali, lakini matokeo yake leo tunalalamika hatuna madaktari hatuna *Wahandisi* hatuna wataalam wa kitu hiki, kilimo na mambo mengine matokeo yake wametukimbia kutokana na uhafifu wa mshahara nay ale marupurupu yake ambayo yanatakiwa yafuatwe kwa mujibu wa taratibu na sheria. Tulikuwa na madaktari wengi sana leo tujiulize wako wapi, tulikuwa na *Wahandisi* wengi sana leo tujiulize wako wapi.

Sasa naomba serikali mtu husamini kile chake kilichomo ndani hebu hawa madaktari tuwaangalie ni mafao gani ambayo madaktari hawa wanahitaji kupewa ili tusiwavunje moyo wakaweza kutukimbia, ma- *Wahandisi* lakini kubwa zaidi la kushangaza madaktari, Wahandisi wenye taaluma ya kutusaidia tunawapandisha vyeo mara Mkurugenzi, Mara katibu Mkuu. Cheo cha Mtu Mheshimiwa ni fedha Mhe. Spika, kama ni daktari cheo chake ni daktari sio tena tumpe dhaana tunamuondoa pale ina maana tunatoa upungufu wa madaktari.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)
(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na utukufu wake kutukutanisha hapa jioni hii tukiwa katika hali ya afya njema. Pia nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kunichagua kua mchangiaji wa kwanza katika jioni hii ya leo. Tatu nimshukuru Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea Mswaada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri katika nchi yetu. Kwani linapelekea kuwatengenezea vyema watumishi wetu ili wawe wameepukana na vikwazo ambavyo vitarudisha nyuma yale maendeleo ya juhudi zao za ufanyaji wa kazi. Kwa kuwa Mswada huu umerekebishwa tu baadhi ya vipengele. Wasemaji wengi asubuhi ya leo wamezungumzia mambo mbali mbali, mimi sitataka kuutumia muda wako mwingi sana kwa sababu mengi yamezungumzwa wakati wa asubuhi. Bila shaka kuna wenzangu wengi baadaye watataka kuuchangia Mswada huu.

Mhe. Spika, naomba nieleze kimuhtasari tunapotaja Utumishi wa Umma kwamba wafanyakazi wengi wanatusikiliza tutachangia nini kuhusu marekebisho haya ili na wao kujenga matumaini katika ajira zao ambazo hivi sasa wanazifanyia kazi.

Mhe. Spika, mimi nakwenda moja kwa moja katika baadhi ya vifungu vya Mswada huu. Niende katika ukurasa wa 51 kifungu kinachosema ripoti ya mwaka ya utumishi wa umma, kifungu 29(1) kinasoma hivi:-

Kifungu cha 29(1) "Kamisheni sio zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka juu ya hali na ufanisi wa utumishi wa umma na Waziri ndani ya siku thelathini Waziri atashindwa kuiwasilisha kwa Rais. Kamisheni itawasilisha ripoti hiyo kwa Rais"

Mhe. Spika, mimi nadhani tamko hili litaleta migongano baina ya kamisheni na Waziri anayehusika kupeleka ripoti ni Waziri si kamisheni. Kwa sababu ya kusema hivyo ni kwamba hapa kuna tamko la "iwapo ndani ya siku thalathini Waziri atashindwa kuiwasilisha kwa Rais.

Kamisheni itawasilisha ripoti hiyo kwa Rais" Nahisi Mwanasheria Mkuu atakapokuja kutoa majumuisho aniwekee bayana kauli hii. Kwa sababu nahisi kutakua na mgongano baina ya kazi ya Waziri na kazi ya kamisheni. Anayehusika kupeleka ripoti hii kwa Rais angekua ni huyu Waziri au kungekua na marekebisho kwamba iwapo ndani ya siku 30 Waziri atakua na dharura ya kimsingi basi kamisheni itapeleka ripoti hiyo kwa Rais.

Nasema haya kwa sababu kifungu namba 2 kinaeleza mara baada ya ripoti hiyo kuwasilishwa kwa Rais, Rais atamuelekeza Waziri kuiwasilisha ripoti hiyo Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo mlengwa hapa angekua ni Waziri moja kwa moja kuliko Waziri atakaposhindwa ipelekwe ripoti hii na kamisheni. Hapa Mheshimiwa atakapoleta majumuisho atueleze vizuri juu ya huu utata ambao mimi nimeuona upo.

Mhe. Spika, niende katika marekebisho ya kifungu cha 49(b) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

Kifungu cha 49 "(b) kuongeza aya mpya ya (i), (j) na (k) kama ifuatavyo:

(i) Itafanya uchunguzi na ukaguzi wa kila mara wa usimamizi wa rasilimali watu;"

Hapa ningemuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu hili tamko la kila mara, nahofia hapa watu itakua kazi yao ni kufanya uchunguzi mara kwa mara. Ningemuomba Mhe. Mwanasheria kifungu hiki akiangalie vizuri na labda kisomeke kwamba "itafanya uchunguzi na ukaguzi kwa wakati maalum" atuwekee wakati maalum kama baada ya miezi mitatu au miezi sita. Lakini hii ukaguzi wa mara kwa mara hili nahisi kwamba linahitaji marekebisho.

Mhe. Spika, niende kwenye kifungu cha 49(k) kinaeleza kwamba:

Kifungu cha 49“(k) itatoa na kukifanyia mapitio mara kwa mara kitabu cha muungozo na Utumishi wa Umma”`

Hapa vile vile utata wangu upo kwenye hili tamko la mara kwa mara. Tamko hili litawafanya watendaji kufanya mapitio ya mara kwa mara huo muongozo ambao utatolewa.

Mhe. Spika, suala la utumishi wa umma ni suala muhimu na linahitaji ufafanuzi wa uwanja mpana sana. Kwa sababu watumishi wa umma wana mambo mbali mbali ambayo ni haki zao ambazo zinahitaji zielekezwe na zifafanuliwe na watendaji wakuu katika watenaji wao.

Mhe. Spika, nizungumzie suala la ufanyakazi bora. Kila mwaka kunakua na masuala ya kutafutwa wafanyakazi bora. Lakini inaelekea kwamba vigezo vile vya kuwatafuta wafanyakazi bora vinakua na mtihani mkubwa kwa wafanyakazi. Labda Mheshimiwa atakapokuja hapa atueleze ni vigezo gani wanavyotumia mpaka apatikane mfanyakazi bora katika Wizara au idara husika. Kwa sababu kuna wafanyakazi mara kwa mara unamkutia huyo huyo kwa nini iwe kila siku huyo huyo na wakati kuna watu wana juhudi kubwa katika kazi na hawapati ufanyakazi bora.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie mikataba ya muda baada ya wafanyakazi kumaliza muda wao wa utumishi wa umma. Hivi sasa tuna wafanyakazi wengi ambao wanamaliza muda wao na miongoni mwao huajiriwa tena katika kipindi cha mkataba wa miaka mitatu.

Namuomba Mheshimiwa hili aliangalie vizuri kwa sababu tuna vijana wengi ambao wamemaliza masomo, wenye fani zile ambazo tunawaajiri watu kwa muda wa miaka mitatu hatuwaajiri wamebakia majumbani wamelemaa lemaa. Naomba suala hili vile vile liangaliwe kwa umakini ili vijana wetu ambao wamepoteza muda mrefu, na fedha nyingi kwa ajili ya masomo na wao kuipata haki hii ya ajira. Na yule ambaye ameshatimiza miaka 60 kama si kwa utaalamu maalum basi wabakie ili tuwaingize vijana wetu katika ajira hii ambayo nao watatoa mchango wao katika taifa letu au katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa mswada wetu ni mfupi sana na wapo wachangiaji kadhaa ambao wataingia sasa hivi badala yangu. Mimi nimalizie hapa na naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia kidogo tu huu mswada kwa yale ambayo niliyokua sijayafahamu.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuuleta mswada huu katika Baraza hili la Wawakilishi na Wajumbe kuweza kuuchangia. Nende katika kifungu cha 3 (a) naomba nikinukuu,

Kifungu cha 3

“(a) kufuta tafsiri ya neno “Afisi Kuu” na badala yake kuweka ifuatavyo:
Ofisi Kuu ya Utumishi “maana yake ni Ofisi Kuu itakayosimamia Utumishi wa Umma iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 47 cha sheria hii”

Halafu nende katika kifungu 3 (b) hichi na wenzangu wameshakizungumza kwa sana lakini na mimi bado sijakifahamu, naomba nikinukuu.

> "(b)Nafasi maalum "maana yake ni utumishi wa umma kama inavyooneshwa katika kifungu cha 60 cha Sheria hii ambapo wataalamu wake ni adimu, au inahitajika watu wenye ujuzi na uzoefu maalum au kwa maoni ya Waziri nafasi hiyo inahitaji wataalamu maalum kutoka ndani au nje ya Zanzibar."

Hapa kidogo hii adimu ndiyo inayonisumbua, pia inanitatanisha hii wataalamu adimu sijui kama ndivyo nilivyofahamu. Ikiwa kama wataalamu ni adimu kwa nini tusiwasomeshe wataalamu wetu kwanza ili tukapata wataalamu ambao waliokua wanaweza kuiendeleza hii sheria.

Mhe. Spika, nikija kifungu cha 29, sijui kama kwenye marekebisho niliiyona, lakini mstari wa kwanza inasema ataiwasilishwa hapa ningesema ataiwasilisha, neno jengine ni "Kuwasilishwa" au "kuwasilisha" kwa Raisi Kamisheni itakayowasilishwa na ripoti hiyo kwa Raisi.

Kifungu cha 49 "(a) Kufuta maneno ya mwanzo na kuweka yafuatayo "Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma itakua ni chombo cha kuratibu na kusimamia uendeshaji wa utumishi wa umma bila ya kuathiri kazi nyengine ambayo imepewa Sheria hii au sheria nyengine, itafanya majukumu yafuatayo:"

Mhe. Spika, hapa kidogo pana nitatanisha, sheria hii au sheria nyengine, itafanya majukumu yafuatayo.

Kifungu cha 65 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa:-

(a) Kufuta kijifungu cha (3) na badala yake kuweka kifuatacho

> "(3) Uhamisho wa wafanyakazi katika utumishi wa Umma kutoka Wizara au Ofisi moja kwenda Wizara au ofisi nyengine ndani ya utumishi wa umma utafanywa na Katibu Mkuu, Mkuu wa utumishi wa umma baada ya kushauriana na watendaji wakuu na taasisi zinazohusika na uhamisho huo"

Mhe. Spika, hapa pametajwa Katibu Mkuu Kiongozi. Lakini hapa unasema kwamba uhamisho huo utafanywa na Katibu Mkuu na kushauriana na watendaji. Hapa naomba kidogo nifahamishwe.

Mhe. Spika, baada ya hapo nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba haya maelezo yote waliyochangia wajumbe na ambayo wameyatoa. Namuomba Mhe. Mwanasheria ayatolee ufafanuzi ili na huko nje wananchi wetu waweze kuelewa. Mhe. Spika, sisi humu ni watunga sheria tu lakini si wana sheria. Na huko nje Mhe. Spika, kuna watu ambao wanaelewa sheria kuliko watu wengine. Maana yake utakapokwenda mtu anakupa sheria yake itakushinda hata kuijibu.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu haya waliyoyasema wajumbe yote aweze kuyatolea ufafanuzi ili wetu nao waweze kuelewa. Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Mswada huu wa sheria. Tumeona madhumuni na sababu ya Mswada huu kufanyiwa marekebisho ya sheria mbili ambazo ni Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na Sheria ya Ruzuku ya Vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1997.

Mhe. Spika, kwanza niombe yale yote ambayo yametolewa na Kamati ya Katiba na Sheria basi kwanza ni jambo la busara kwamba yakafuatwa, yale mapungufu na mapendekezo ambayo yametolewa na kamati.

Mhe. Spika, tunaona kwamba sheria pamoja na katiba ni vitu ambavyo vinakwenda sambamba, si vizuri kwamba sheria ikapingana na katiba. Kwa hivyo sisi kama ni wanasheria wa kutunga na kuzifuta zile sheria kwa hivyo mimi naungana mkono na mwenzangu kwamba sheria hizi ni nzuri na Mswada huu ni mzuri na nimpongeze Mwanasheria kwa kuwasilisha Mswada huu.

Mhe. Spika, kwa kua ni jukumu letu sisi kama Wawakilishi wa wananchi ni lazima kila penye taasisi na kila penye mambo mbali mbali ya kuendesha nchi basi ni lazima kuwe na sheria. Hili ni jambo ambalo likitokea tatizo lolote basi kunakua na sheria ya kuilinda ile taasisi au pale mahala fulani.

Mhe. Spika, kama walivyotangulia wenzangu kutoa mapendekezo au kusoma vifungu baada ya vifungu na mimi nichukue fursa hii ya kuchukua kifungu baada ya kifungu. Nianze na kifungu cha 29 kinasema kama hivi ifuatavyo.

Kifungu cha 29.(1) “Kamisheni sio zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha itatayarisha kwa kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka juu ya hali ya ufanisi wa utumishi wa umma na Waziri ndani ya siku thalathini ataiwasilisha kwa Rais…”

Kama walivyokwisha kusema wenzangu kwamba Waziri ndani ya siku thalathini ataiwasilisha kwa Rais na iwapo Waziri atashindwa kuiwasilisha kwa Rais Kamisheni itawasilisha ripoti hiyo kwa Rais. Hapa kusema Waziri atashindwa kufanya hivyo kwa kweli tunaamini kwamba Mawaziri wetu hawashindwi na kazi. Kwa hivyo hili si neno zuri la kulitia hapa kwamba “Waziri atashindwa” Tunajua Waziri kwamba wao ni wa Serikali, hawawezi kushindwa na mambo kama haya. Kwa hivyo hapa liwekwe neno ambalo litakua zuri zaidi lisiwe hilo.

Mara baada ya ripoti hiyo kuwasilishwa kwa Rais. Rais atamueleza Waziri, kuiwasilisha ripoti hiyo Baraza la Wawakilishi kamka kawaida sisi ndio Wawakilishi wa wananchi na sisi ndio tunaoondosha na kuweka zile sheria zilizokua zitakua na ufanisi zaidi na zitakua kwa wakati huu zinakua ni sheria ambazo tunaziona zitakidhi ile haja.

Mhe. Spika, kuna kifungu 47(1) kuanzishwa ofisi ambayo itajulikana ni Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma ambayo itakua chini ya Afisi ya Katibu Mkuu ambaye atakua Msaidizi Mkuu wa Katibu Mkuu Kiongozi kwa mambo yote yanayohusiana na utumishi wa umma. Hapa kidogo na mie kama walivyosema wenzangu tatizo ni kwamba bado sijafahamu kuanzishwa kwa afisi hii ambayo itakua Katibu Mkuu Kiongozi wa mambo yote haya yatakua yanahusiana na utumishi huu wa umma ambaye atakua pamoja na afisi hii.

Kifungu cha 49 (a) Kufuta maneno ya mwanzo na kuweka yafuatayo "Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma itakua ni chombo cha kuratibu na kusimamia uendeshaji wa Utumishi wa umma bila ya kuathiri kazi nyengine…"

Kifungu hichi Mhe. Spika, vile vile sijakifahamu vizuri, atakapokuja Mwanasheria Mkuu atatuelezea zaidi. Kwa sababu sisi tunachokitaka ni kuziboresha hizi sheria ili tuweze kwenda kwa mustakbali ambao tunaotakiwa tuende.

Mhe. Spika, niende kwenye marekebisho ya "Kifungu cha 65 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa (a) kufuta kifungu cha (3) na baada yake kuweka kifuatacho: -

"(3) Uhamisho wa wafanyakazi katika utumishi wa umma kutoka Wizara au Ofisi moja kwenda Wizara au Ofisi nyengine ndani ya utumishi wa umma utafanywa na Katibu Mkuu wa Utumishi wa Umma baada ya kushauriana na watendaji wakuu wa taasisi zinazohusiana na uhamisho huo"

Kuna kada mbali mbali, kuna kada ya uhasibu sijui kama hapa kwenye uhamisho huu hawa watu wa uhasibu tunao. Kwa sababu tunajua kwamba watu wa uhasibu wapo katika kada ambayo mtu aliyekua ana stahiki kuwahamisha ni Mhasibu Mkuu wa Serikali. Sasa sijui na hawa pia wataingia kwenye mkumbo huu au kutakua na sehemu nyengine au watawasiliana.

Mhe. Spika, kusema kweli sisi kama Wawakilishi tunaunga mkono sheria hii, marekebisho ya sheria hizi. Lakini kwa kweli inakua ni vigumu kujua. Ingekua hizi sheria ni kama kitu ambacho ninajua kama nikitaka kujua Katiba basi nitakwenda moja kwa moja kwenye katiba lakini kwenye sheria hizi ingawaje tuna changia na kuziunga mkono lakini hasa kusema kwamba sheria hii mimi nikienda nitaikuta pahala fulani kwa kweli inakua ni tatizo.

Mhe. Spika, wengi wetu humu ndani tuko wapya, kwa hivyo hatujui hii sheria iliyofutwa ya mwanzo basi tutaipata wapi. Sijui kama na wenzangu wapo hivyo hivyo lakini kwa mimi kidogo najikuta inanipa tabu isipokua ni jambo la msingi ni la kulitafuta na kulichangia. Basi niseme kwa upya wetu na namna tulivyo na haya ni mambo ya lazima tuyajue ilikua tuzipate zile sheria zilizofutwa ili tuweze kuzijua zipo wapi na hizi tunazoziandaa mpya basi vile vile tuzijue. Kwa haya machache Mhe. Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Moh'd Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, jioni hii nami kupata nafasi ya kutoa machache kuhusu Mswada huu ulioko mbele yetu. Nianze kwanza kumpongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea Mswada huu kufanya marekebisho ambao sehemu moja mwaka jana tu Mswada huu unaohusu Utumishi wa Umma ulipopitishwa katika Baraza hili. Lakini kuonekana kama unao mapungufu ukaonekana kwamba uletwe kwa kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, mimi nizungumzie machache tu kidogo katika madhumuni ya marekebisho haya. Madhumuni ya Mswada huu ni kufanya marekebisho ya Sheria 2 ambazo ni:

1) Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya 2011

2) Sheria ya Ruzuku ya Vyama vya Siasa Nam. 6 ya mwaka 1997

Mimi nataka nianze na hii ya pili, ruzuku..

Mhe. Spika: Mheshimiwa hiyo imerekebishwa, baada ya kupata maoni ya wadau. Kwa hiyo, hiyo siyo katika sehemu ya Mswada uliowasilishwa katika Baraza hili. Mswada uliopo mbele yetu hivi sasa ni Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mohd Haji Khalid: Nije moja kwa moja kwenye Utumishi wa Umma. Mhe. Spika, sheria zetu ni nzuri, lakini mara nyingi tunashindwa kuzisimamia na kuzitekeleza. Pale ambapo tutazisimamia vyema sheria zetu kwa kweli ingelikua hatuna haja ya kufanya marekebisho ya sheria zetu mara kwa mara.
Kwa kua utumishi wa umma tuliipitia sheria hii mwaka jana lakini na leo tunaleta marekebisho yake kwa sababu ndani yake labda kumekua na mapungufu kiasi fulani, moja kati ya hayo mara nyingi tunachukua watumishi wa umma ambao umri wao wameshakua wanastaafu na hatimaye tunawapa mikataba ya muda na kurudi tena makazini.

Mhe.Spika, kamati yangu mara hii tulikwenda Dar es Salaam, mimi nilikwenda katika kituo kimoja kupima miwani, daktari aliyenishughulikia ni Mzanzibari ambaye amesoma hapa. Lakini kwa matatizo ya ajira hapa ndani aliposomeshwa, akaona bora aondoke akatafute maisha mahala pengine. Kwa hivyo, serikali yetu inatusomesha, lakini hatimae vijana wetu wengi hawapati yale matunda yao baada ya kupata elimu kulingana na sheria zetu za utumishi zilivyo.

Mhe.Spika, hivi juzi Tume ya Utumishi Serikalini imefanya marekebisho ya mishahara, lakini bado kuna matatizo mbali mbali kwa wafanyakazi wetu ambao bado mishahara yao haijakaa vizuri, na ingawa tuna sheria nzuri tumeipitisha hivi karibuni. Mhe.Spika, vijana wanapomaliza mafunzo yao tujaalie kaajiriwa akiwa na elimu ya kidato cha sita akenda katika mafunzo ya diploma, anaporudi kazini utumishi wanachelewa kumfanyia marekebisho mshahara wake, mara nyengine huwa unafika mwaka mzima bila ya kupata marekebisho kutoka ngazi aliyokuwa na ile ngazi anayoingia, mambo ambayo yanasababisha vijana wetu kuwavunja moyo.

Mhe. Spika, hili la kuajiri wazee ambao wameshaacha kazi, na vijana wenye taaluma wapo pia, vijana jambo hili linawavunja moyo. Kwa hivyo, serikali ningeiomba, hii mikataba ya muda itolewe kwa shughuli maalum na kwa haja maalum. Lakini pale ambapo kijana wa kada ile yupo basi asichukuliwe mzee aliyekwishapata marupurupu yake yote, halafu akarejeshwa pale na mtumishi ambaye bado yuko imara na ana uwezo wa kufanya kazi tukamuacha nje ikawa serikali inasomesha, lakini inashindwa kuwaajiri pale ambapo ajira ile ipo. Mhe.Spika, kwa hayo machache niliyozungumza naunga mkono mswada huu, ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, jioni hii ya leo na mimi kunipa fursa ya kuchangia mswada huu ulioko mbele yetu wa kurekebisha sheria. Mhe.Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii na mimi nitoe pole kwa ndugu zetu wa Jimbo la Bububu kwa kuondokewa na Mwakilishi wao, kwa hiyo Mwenyezi Mungu awape subra katika kipindi hiki cha maombolezo.

Mhe. Spika, baada ya kutoa pole kwa kuondokewa na Mwakilishi mwenzetu, sasa naomba niingie katika mada ambayo tunaijadili. Mhe.Spika, kwanza na mimi nimpongeze Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea marekebisho haya ya sheria katika kipindi hiki ambacho ni kipindi muafaka

katika nchi yetu. Lakini namuomba Mhe.Mwanasheria katika kurekebisha hizi sheria, namuomba aangalie kile ambacho kinahitaji kufanyiwa marekebisho yeye kama Mwanasheria Mkuu atuletee na sisi tuweze kukiangalia na kukifanyia marekebisho pale ambapo panahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mhe.Spika, wenzangu waliopita wamekiri na wamesema hata katiba yetu inahitaji kuangaliwa kwa kina kwani kuna baadhi ya sehemu zinahitaji kufanyiwa marekebisho. Hilo mimi naungana nao, kwa sababu yamo mambo muhimu sana ambayo yanakwaza, aidha sheria zinapingana pingana, kwa hiyo yeye kama Mwanasheria Mkuu anahitaji kutuletea na kufanya marekebisho.

Mhe. Spika, si hilo tu naomba pia aangalie kama katika kufanya marekebisho ya sheria isiwe ni kwa zile ngazi au taasisi za serikali, tuone hata mule ambamo ni sehemu za watu binafsi pia mnahitaji kufanyiwa marekebisho, kwenye sheria zetu tuone kama hizo sheria zinawabana wale wawekezaji wa hoteli. Kwa mfano, Mhe.Spika, utakubaliana na mimi kama kila siku yanakuja malalamiko kuwa wafanyakazi wa hoteli hawapewi mikataba, na serikali baada ya kuongeza mishahara, basi kwa ujanja wa wamiliki wa hoteli ni kwamba wafanyakazi wengi wamewapunguza kwa ajili ya kwamba kumeongezwa mishahara. Kwa hivyo, naomba na hili lionekane kama linahitaji kufanyiwa marekebisho, ili sheria zetu ziweze kuwabana na kuwasimamia kuona kama hawana pa kupita ila wanatekeleza sheria inavyowajibika.

Mhe.Spika, suala jengine nimpongeze sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika mswada huu kifungu cha 7 (b) kinaeleza kama kutakuwa na uchunguzi pamoja na uangalizi kwa wafanyakazi wetu mara kwa mara ili kuona kama wanatekeleza wajibu wao. Kwa hivyo, naomba kifungu hiki Mhe.Spika, Mwanasheria Mkuu akione ni kifungu muhimu kama alivyokiweka, lakini kitekelezwe kwa vitendo sio kwa kusema.

Mhe.Spika, pia uwepo ukaguzi wa kuwakagua mara kwa mara na kuona kama wanatekeleza wajibu wao kwa sababu mara nyingi wafanyakazi hasa wa viongozi wanakuwa wajanja wajanja. Lakini kama kutakuwa na ukaguzi wa mara kwa mara basi kile kitu ambacho watakuwa wanakifanya itakuwa kinaonekana dhahiri na kinafanyiwa kazi. Mhe.Spika, hata kama kuna chembechembe ya rushwa basi ikiwa kuna ukaguzi wataona na watagundua na kitafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, vile vile naomba sasa hivi tuone sheria zetu zinafanyakazi kikamilifu kama zinavyopitishwa, kwa sababu kupitisha sheria ni kitu chengine na kufanya kazi ni kitu chengine. Kwa hivyo, naomba hizi sheria zetu zisimamiwe ili ziweze kufanya kazi vizuri, kwani kufanya kitu halafu usikiendeleze ukakifikisha mwisho wake, ni sawa na kuwa hukukifanya. Kwa hivyo, kukusanya sheria zikawa hazifanyi kazi itakuwa ni sawa sawa na kuwa hatuna sheria.

Mhe.Spika, pia nataka nizungumze katika sehemu ya pili ni kwamba, sehemu hii inaeleza kutakuwa na nafasi maalum maana yake ni utumishi wa umma kama ilivyooneshwa katika kifungu cha 60 cha sheria hii, na wataalamu wake ni adimu au wanahitaji watu wenye ujuzi na uzoefu maalum, na kwa kuwa maoni ya waziri nafasi hiyo inahitaji wataalamu maalum kutoka ndani au nje ya Zanzibar.

Mhe.Spika, kifungu hiki ni kizuri sana, lakini naomba tuone katika sehemu zetu zote za kazi kama kuna upungufu wa wataalamu basi afadhali serikali ione kuwa sehemu hii ina upungufu wa wataalamu, hivyo serikali ijitahidi kusomesha wataalamu wa fani ile ambayo inatakiwa.

Mhe.Spika, kwa sababu wataalamu hawa kama watakuwa hawasomeshwi na wakashika nafasi zao, basi kwa kweli kuwachukua wataalamu maalum kila siku ambao wameshafika muda wa kustaafu halafu tunawachukua tena, hiyo itakuwa ni sawa sawa na kuwanyima wasomi wetu, ndugu zetu ambao wanasoma kwa ajili ya matumaini ya kufanya kazi. Kwa maana hiyo kuwarudisha wataalamu hawa mara kwa mara ni sawa sawa na kuwanyima wale wasomi wetu. Kwa hivyo, tuone kama kuna haja mtu akifika kustaafu basi wawepo watu wenye ujuzi wa kushika nafasi yake.

Mhe.Spika, hapa inatakiwa serikali ifanye kazi ya kusomesha wataalamu kuona kama katika fani fulani wataalamu wana upungufu, basi serikali ijitahidi kuwasomesha. Lakini sio kwamba wale wale waliokwishakustaafu wazuie wenzao kufanya kazi, na wakati muda wao umeshafika wa kustaafu. Kwa hivyo, naomba hapa tuone kama kuna haja ya kuwasomesha wataalamu wa fani hizi ili waweze kushika nafasi hizi na kuwapa moyo ndugu zetu na wasomi wetu ambao wapo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, namuomba Mwanasheria Mkuu aone kama hawa wataalamu ambao wameshafika muda wa kustaafu, basi na wafanye klabu yao wajikusanye kama vile Wazee Klabu ya Arusha, wakishafanya hivyo watakuwa na *NGO's* zao na zitakuwa zinawasaidia, watapata fedha na watasaidia na wenzao. Lakini kama kila siku wataalamu hao hao wanarejeshwa, na huku kuna watu wameshasoma ni bora tuwaendeleze vijana wetu wapate washike nafasi hizo, isiwe ni wao kwa wao kila siku. Mhe.Spika, naomba na hili Mhe. Mwanasheria Mkuu aone kama kuna haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kwa sababu mswada huu ni mfupi sana na umeshazungumzwa sana, hivyo mimi naomba nimalizie hapo, naunga mkono hoja hii.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na kuweza kuzungumza. Mhe.Spika, pamoja na kumpongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuleta marekebisho kuona kwamba hali inaporuhusu au mambo yanavyobadilika na marekebisho yanafanyika, lakini pia nina masikitiko mawili ambayo yamenikaa. Sikitiko la mwanzo tuliambiwa hapa bila shaka Mwanasheria Mkuu ni jukumu lake kwamba miswada sasa itaanzwa kusomwa mara tatu katika vikao tofauti, na hii ina faida yake. Lakini mwaka unafika kati kati sasa hivi bado hali hiyo haijajitokeza.

Kwa hivyo, namuomba Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwamba ile nafasi ambayo ilikuwa tupate kwa kusomwa miswada mara tatu katika vikao tofauti basi tuweze kuipata. Kwa sababu wengi waliozungumza leo imewashtukiza hii sheria kulinganisha kwa sababu miswada ilikuwa ni mingi, na mambo yamekuwa ni mengi. Lakini tungepata fursa ya kusomewa kabla ile miswada inayokuja katika kikao kijacho basi kwa wale ambao wanafanyakazi, wangefanyakazi ya ziada.

Mhe.Spika, sikitiko langu la pili ni kwamba mswada huu kabla haujaletwa katika Baraza tulifanyiwa semina, na katika semina ile palitolewa kauli kwamba ni lazima upatikane huu kwa sababu hakuna sheria iliyotawala utumishi wa umma. Kwa hivyo, sikitiko langu lipo hapa kwamba kama siku za kufanyiwa marekebisho zilikuwa zishafika, basi wangeshirikishwa wale wadau, moja wapo ni vile vyama vya wafanyakazi, wangelishirikishwa ili kuona kwamba mapungufu yaliyokuwepo wakati ule ilipopitishwa sheria hii nayo yanafanyiwa marekebisho.

Kwa hivyo, namuomba Mwanasheria Mkuu itakapotokezea tena fursa ya kufanyiwa marekebisho sheria hii ya utumishi wa umma, basi wadau nao waitwe washirikishwe ili zile dosari ambazo zilikuwa hazikuonekana wakati ule ziweze kufanyiwa marekebisho.

Mhe.Spika, suala langu la pili ni juu ya uwezo na demokrasia pamoja na utawala bora. Mhe.Spika, katika utawala bora uwezo unaondolewa kutoka kwa mtu binafsi na kupelekwa katika utawala wa wengi. Kwa hivyo, katika mswada huu kwa mujibu wa katiba kifungu cha 116, Kamisheni ya Utumishi wa Umma ndiyo iliyokuwa chombo kikuu, lakini kuna dalili ya kuziondoa nguvu zile na kuzipeleka kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mhe.Spika, hizi naona ni dalili za kuondoka kwenye utawala bora na kuelekea utawala ule wa *autocratic*. Kwa hivyo, namuomba sana Mwanasheria Mkuu pale ambapo maamuzi yatokane na chombo ni bora zaidi kuliko maamuzi yakatokana na mtu.

Mhe.Spika, nikija katika baadhi ya vifungu ambavyo vimerekebishwa, kifungu cha 5 cha sheria kinasema:

“Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kushauriana na tume husika anaweza kutoa ruhusa ya kuajiriwa kwa mkataba maalum kwa mtu ambaye ana sifa, utaalamu na uzoefu katika nafasi iliyotangazwa na waziri chini ya kifungu cha 60 (1) (b) cha sheria hii”.

Mhe.Spika, pana mambo mawili ndani yake hapa, moja lile nililolizungumza kwamba chombo cha kutoa zile ruhusa za ajira kama hizi, ingebakishwa bado kwamba ni kamisheni, utumishi tayari imeshaajiri lakini uajiri wa ziada wa mkataba ungebakishwa kwenye kamisheni ili kukafanywa na walio wengi na chombo maalum badala ya kuachiwa mtu. Lakini la pili kuna mgongano baina ya Katibu Mkuu wa ile wizara, nyuma pengine ilikuwa hakuna wizara hiyo, lakini sasa hivi tushakuwa na Wizara ya Utumishi na Utawala Bora. Kwa hivyo, Katibu Mkuu wa Utumishi na Utawala Bora atafanya kazi gani ikiwa maamuzi kama haya anapewa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mhe.Spika, kama alivyosema mjumbe mmoja hapa kwamba Katibu Mkuu Kiongozi ni *over roll* wa Makatibu Wakuu wote, hivyo ingelikuwa ni sawa kwamba akafanywa ni kiongozi wa Makatibu Wakuu wote kuliko kuchukua wizara moja ukamfanya mkubwa zaidi hivyo kutakuwa na msongamano. Mhe.Spika, pia hatumpi uwezo huyo Katibu Mkuu wa Wizara ya Utumishi na Utawala Bora kufanya kazi zake kwa sababu itabidi kila mara afanye *consultation* na Katibu Mkuu Kiongozi kabla hajatoa maamuzi, jambo ambalo katika wizara nyengine hakuna.

Mhe.Spika, katika kifungu kilichofanyiwa marekebisho kifungu cha 65 (b) cha sheria hii kinaelezwa kuongeza kifungu kipya cha 7 kama ifuatavyo:-

“Bila ya kujali masharti ya sheria hii, chombo maalum cha serikali kinachohusika na usimamizi na uhamisho wa kada maalum ya watumishi au taaluma maalum ya watumishi wa umma, kinaweza kufanya uhamisho wa wafanyakazi hao ndani ya taasisi za utumishi wa umma kwa mujibu wa taratibu za uhamisho wa kada hizo au taaluma hiyo”.

Mhe.Spika, hiki chombo maalum nataka Mhe. Mwanasheria Mkuu aje atueleze kwa sababu katika dondoo za nyuma haikuelezwa chombo maalum ni chombo gani na humu katika sheria hii haikuelezwa chombo maalum ni chombo gani. Ndio pale tunaposema kwamba sheria iwe wazi, hatuwezi kutunga sheria halafu zikawa na mibano, sheria iwe wazi ili kila mmoja ajue chombo maalum hiki ni chombo gani. Kwa hivyo, tunamuomba Mwanasheria Mkuu aje atueleze chombo maalum hiki ni gani na kwa nini kisielezwe tafsiri yake kule mwanzo.

Mhe.Spika, mimi kidogo nilikuwa nina suala kuhusu kufutwa kwa kifungu (l) na (n) katika kifungu cha 25 cha mswada. Katika mswada huu wa Kiingereza tulioletewa hapa unasema. *Deleting paragraph (l) and (n).* Kwa hivyo, hapo kidogo nataka nipate maelezo kwa nini vifungu hivi vinafutwa kuna zaidi iliyoongezwa au kumeonekana nini katika vifungu hivi.

Mhe.Spika, labda nirudie kwa yale waliyosema wenzangu kwa kutilia nguvu, sirudii kwa sababu ya utashi tu, narudia kwa sababu ya kutilia nguvu. Pale iliposemwa ripoti ya miezi mitatu ya kila mwaka ambapo Kamisheni inatakiwa ipeleke ripoti kwa Waziri, na Waziri apeleke kwa Rais. Lakini jambo la kushangaza ni namna gani Waziri akichelewa kupeleka ripoti ipelekwe ile ile, hapo mimi ndipo penye suala langu.

Mhe. Spika, kifungu cha 29 (1) kinasema: *Shall submit the same to the President*. Mimi nilifikiria kupelekwa kwa Waziri labda aingize maoni yake, lakini ikiwa ni *same report* basi ipelekwe kwa Rais na *copy* kwa Waziri kwa sababu ripoti inayopelekwa ni ile ile. Kwa hivyo, ikiwa ni *same report* apelekewe Rais kutoka kwa Waziri haina haja ya kupitia kwa Waziri kuikariri, hivyo kamisheni impelekee Rais na *copy* ndio apelekewe Waziri. Kwa hivyo, Rais na Waziri wake watakaa watazungumza, lakini hivi itakuwa sivyo kwa sababu hapa imetajwa neno *same report to the President* ambayo haina haja ya kukaa kwanza kwa Waziri katika meza halafu ndio imfikie Rais.

Mhe.Spika, baada ya kusema hayo ya vifungu naomba nitoe dondoo ndogo kuhusiana na Utumishi wa Umma. Mhe.Spika, namuomba sana Mwanasheria Mkuu afanye utafiti wa kina kuhusiana na dosari zilizopo katika Utumishi wa Umma hasa wakati wa ajira bado tuna matatizo ya wakati wa ajira. Mhe.Spika, hapa hatutaki kusema mengi lakini ubinafsi unatawala, umimi unatawala na mambo mengineyo. Kwa hivyo, ni bora kufanya uchunguzi mapema kuliko kuja kutokea mengi. Kuna taarifa watu wanasema kuwa kuna ajira zimetolewa basi hiyo kada iliyoajiriwa elimu yake ni ndogo sana kuliko ile iliyotakiwa.

Mhe.Spika, mambo kama hayo unapoyasikia na sisi maendeleo tunayoyataka mtu anatakiwa awe na *degree* kwa mfano lakini kwa makusudi mtu anaajiriwa wa diploma tupu wakati wa degree wanatembea njiani. Mhe.Spika, haya mambo lazima yafanyiwe uchunguzi na ikiwa yatafanyiwa uchunguzi na yakabainika wapi tumekwenda kombo, ndio pale wenzangu wanaposema kwamba, tunatunga sheria nyingi lakini hazina msumeno, sheria zinakuwa butu. Kwa hivyo, watu wanafanya watakavyo tu lakini ikibainika hapa mimi nampongeza Mwanasheria Mkuu kuna

kifungu kimoja nimekiona hapa kupitia hizi kada kuna kifungu kinasema kwamba, itapitiwa kila baada ya muda hii Utumishi wa Umma. Mimi nasema kama ambavyo inafanywa kwa mishahara sasa hivi kila baada ya muda utasikia watu wanaambiwa wakapokee binafsi kwa ajili ya mishahara, lakini na taaluma nayo na uzoefu utizamwe.

La mwisho ninalotaka kusema Mwanasheria Mkuu ulikua shahidi ulikuwepo katika ile semina, nilizungumza sana kuhusu *appraisal* ya wafanyakazi, (wafanyakazi tunapaswa kuwatathmini kila mwaka). Leo vyeo vilivyotawala ni Wakurugenzi ndio kada ya kati kati, lakini inapofika wakati Mhe. Rais anataka kuteua Wakurugenzi kila mmoja anajitizama yeye mimi nitateuliwa kwa sababu fulani, mimi kwa sababu fulani, lakini hakuna rekodi ya wafanyakazi inayompa Mhe. Rais kuteua kwa mujibu wa uwezo, elimu na ukakamavu wa yule mfanyakazi. Sasa tunaunda kada gani hiyo ya utumishi wa umma, ambayo kila wakati wa uteuzi wa Mhe. Rais anatizama tu, Kusini sijachukua anachukua mmoja, Kaskazini sijachukua anachukua mmoja, Waziri chini yake aliyekua na *inference* na yeye anapeleka wake na tunawaona humu wamo.

Kwa hivyo, utumishi wa umma tuujenge katika hali ambayo ni ya uwazi na Mhe. Waziri wa Wizara hii kapewa na idara kubwa sana ya utawala bora. Kwa hivyo, naamini kwamba utatunzwa na Mhe. Spika, mimi naomba niunge mkono hoja hii pamoja na marekebisho yake. Nakushukuru sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii jioni hii ili niweze kutoa mchango wangu mfupi kwenye marekebisho ya mswada huu ambao Mhe. Mwanasheria Mkuu ametuletea.

Mhe. Spika, kwanza na mimi nianze kwa kumpongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa uamuzi wake ambao ameamua kutuletea mswada huu, bila shaka ameamua hivi baada ya kuona kuna dosari za kiutendaji katika mswada huu. Mimi binafsi Mhe. Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu na ninamuomba sana kwamba aendelee kufanya utafiti kwa zile sheria zote ambazo zina mapungufu mbele ya jamii yetu zifanyiwe marekebisho. Ni jambo zuri kwa sababu sisi ni Wawakilishi na tunatunga sheria kwa ajili ya Wazanzibari. Wazanzibari wanahitaji sheria ambazo zitawasaidia kuendesha nchi yao na maisha yao.

Sasa kwa msingi huo basi, pia nimuombe Mwanasheria Mkuu aendelee kuzifanyia utafiti hizi sheria ambazo zinawakwaza Wazanzibari. Katika hili naomba nimpe mifano miwili aangalie kwa sababu Wazanzibari wamekua wakilalamika. Kwa mfano, mwaka 2006 tulipitisha sheria ya *VAT*, sheria ambayo inahusiana na *Civil Development Levy*, sheria ambayo waajiri binafsi na Serikali wanatakiwa watoe mafao kwa ajili ya mafunzo ya ufundi (mafunzo ya amali). Lakini tafiti ambazo tunazo waajiri binafsi wamekua wakitoa michango yao lakini Serikali imeshindwa kutoa michango yake ndani ya sheria hii. Sasa ni dhahiri pengine Serikali imeshindwa kwa sababu sheria ngumu haitekelezeki hivyo Mwanasheria Mkuu ni wajibu wako sasa kuangalia kwa nini Serikali haitekelezi mchango uliopangwa na sheria hii. Inawezekana kabisa kwamba sheria hii ni ngumu, inatukwaza na kama inatukwaza basi ni wakati wako Mhe. Mwanasheria Mkuu uingalie basi kwa nini Serikali haitekelezi ili kuifanyia marekebisho sheria hiyo.

Mfano wa pili ambao ningetaka Mwanasheria Mkuu nimwambie ni Sheria ya Uvuvi ambayo tumepitisha mwaka juzi. Wavuvi wetu wa Zanzibar wengi wamekua wakilalamika kwamba

sheria tuliyopitisha hapa imekua ikiwabana na kuwakwaza, sasa ni mambo ya kisheria ningemuomba pia Mwanasheria Mkuu pia aangalie ukweli wa jambo hilo na kama Wazanzibari linawakwaza basi afanye utafiti ili tuweze kuwarekebishia ili maisha ya wavuvi wetu na mwenendo wa sheria hiyo uweze kuwasaidia.

Mhe. Spika, baada ya ushauri huo sasa niende kwenye kifungu moja kwa moja na nianze kwenye kifungu cha 8 ukurasa wa 52. Mhe. Spika, Mwanasheria Mkuu hapa ametupendekeza kwamba kumeongezwa maneno kwenye kifungu (1) (b) cha sheria mama kwamba, "isipokuwa kwa nafasi maalum ambazo zilitangazwa na Waziri katika Gazeti Rasmi la Serikali".

Mhe. Spika, tumempa Waziri nafasi ya kutangaza nafasi ambazo zingefaa kujazwa. Mimi kwa ushauri wangu naona kwamba maneno haya tuyaongeze basi, tuseme kwamba, "isipokuwa kwa nafasi maalum ambazo zitatangazwa na Waziri kwa kushauriana na Tume za Utumishi husika". Kwa nini Mhe. Spika? Nasema hivi kwa sababu inawezekana Waziri akatangaza nafasi lakini kumbe Tume ya Utumishi Mahkamani haina haja ya nafasi ile. Mhe. Waziri anaweza akatangaza nafasi kumbe Tume ya vikosi haina haja ya nafasi ile na anaweza kutangaza nafasi kumbe Baraza la Wawakilishi halina haja ya nafasi ile.

Kwa hivyo, nashauri kwamba kifungu hiki tuongeze maneno hayo kwamba Waziri asitangaze tu kwa vile anavyoona, lakini ashauriane na Tume husika za utumishi ili wenyewe wawe na mahitajio ya nafasi ile kwa mujibu wa sheria. Nashauri hilo kwa sababu Waziri ni mwanadamu na anaweza akafanya hili kwa kupitikiwa au kwa utashi. Kwa hivyo nashauri kabisa kwamba Tume husika za mahakama, vikosi, Baraza la Wawakilishi na Serikalini washauriane na Rais baadae Waziri ndio atangaze kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

Mhe. Spika, kifungu hicho hicho cha (b) kumeongezwa maneno kifungu cha 5 kwamba Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kushauriana na Tume husika anaweza kutoa ruhusa ya kuajiriwa kwa mkataba maalum kwa mtu ambaye ana sifa, utaalamu, uzoefu katika nafasi iliyotangazwa na Waziri chini ya kifungu cha 61(b). Mimi napongeza hatua hii lakini kama Wawakilishi tunapaswa kujiuliza, kwa nini tutoe mwanya wa kuajiriwa watu wa mkataba? Kwamba Zanzibar hatuna wasomi, nafasi nyengine hazina watu wa kujaza?

Mimi kwa mtazamo wangu Mhe. Spika, ni kwamba tumejikwaa pahala, tumeajiri *main power* kubwa lakini haina utaalamu na tumewaacha wataalamu nje wanahangaika. Sasa tumewaajiri watu hatuwezi kuwastaafisha kwa maslahi ya umma hatuna uwezo huo wa kifedha, sasa wanapostaafu tunahangaika kuwaajiri watu kwa mkataba.

Mhe. Spika, nasema hili kwa nia safi kwa sababu, inaonekana *main power* ya waajiriwa wetu Zanzibar ni nyepesi kidogo kufanya kazi, nataka nitoe mfano kwa nia safi wala si kwa kudharau. Ama uwezo wetu wa kitaaluma ni mdogo au tumewapa watu majukumu hatuna vitendea kazi.

Mhe. Spika, juzi kwa bahati mbaya sana ilitokea ajali Jimbo la Mpendae kuna mtu kule aliingia kisimani, bahati nzuri nilipigiwa simu mimi na nikampigia simu Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mbarouk Mussa Wadi (Mtando) na Mhe. Mohammed Said Dimwa mwakilishi wa jimbo tukashuhudie lile tukio. Tangu saa nane mpaka saa kumi na mbili maiti ile ilishindwa kutolewa, licha ya kuwepo kwa vikosi vyetu vya uokozi, sasa unajiuliza je, vikosi havina uwezo?

Mhe. Spika, unapoangalia vikosi vile wapo wengi na wana uwezo lakini hawana vifaa, tumempa chupa ya gesi ambayo uwezo wake ni dakika tano, kisima cha pima 16 gesi ile haimudu kwenda chini. Sasa namna gani tunamuwezesha mfanyakazi wetu, kwa bahati nzuri baada ya kushindwa akatokea mwananchi mmoja akaingia kisimani bila ya gesi akaitoa maiti ile ambaye si mfanyakazi. Ukiangalia ni aibu haipendezi kwamba tuna vikosi vyetu vina gari kubwa la zimamoto lakini tunashindwa kumtoa maiti zaidi ya masaa sita. Hapa ni dhahiri kwamba vifaa hatukuwapa na hatimaye sasa akatokea mtu mwengine tukamkodi ndio akatutolea maiti.

Sasa Mhe. Spika, mimi nimshauri Mhe. Mwanasheria Mkuu kua tuangalie sababu ambazo zinawakwaza wafanyakazi wetu, je ni uwezo au hatujawawezesha kuwafanyisha kazi ili waweze kufanya kazi kwa mujibu wa uwezo wetu.

Mhe. Spika, jingine kifungu cha 9(a) kuna maneno hapa yanayosema kwamba, "Uhamisho wa wafanyakazi katika utumishi wa umma kutoka Wizara au ofisi moja kwenda ofisi nyengine ndani ya utumishi wa umma utafanywa na Katibu Mkuu wa Utumishi wa Umma baada ya kushauriana na watendaji wakuu wa taasisi zinazohusika na uhamisho huo".

Mhe. Spika, ni jambo zuri lakini mimi napendekeza kwamba tuongeze neno 'baada ya kuwepo kwa sababu za msingi'. Sisi Wawakilishi wako tumekua tukiona wafanyakazi wanahamishwa bila ya sababu ya msingi, mfanyakazi anapofanya wajibu wake akimkosea bosi kwa mujibu wa majukumu yake tayari anahamishwa, sasa lazima tuweke sentensi ambayo mfanyakazi akihamishwa bila ya sababu ya msingi aweze kujitetea, kwamba nimehamishwa kwa sababu nimemkosea bosi vyenginevyo wafanyakazi wetu wazuri watahamishwa bila ya sababu za msingi.

Ziko taarifa kwamba kuna wafanyakazi hapa na Pemba kua hapa wamepelekwa Pemba na wa Pemba wamepelekwa Unguja kwa nini? Wamekataa kufanya wajibu wao kwa mujibu wa sheria, sio kwa uzembe, sheria inasema hivi nitafanya, bosi anasema usifanye hatimae siku ya pili anaambiwa hama. Sasa lazima tuweke sentensi hii kwamba baada ya kuwepo kwa sababu za msingi za uhamishao huo.

Mhe. Spika, kifungu chengine cha saba na cha chini yake kwamba ikizingatiwa kua uwezo wa kufanya uhamisho huo chini ya kifungu hiki utafanywa pale tu ikiwa ameruhusiwa na sheria maalum au ikiwa hakuna sheria hiyo kwa ruhusa ya Waziri itakayotolewa kwa taarifa maalum ya Gazeti Rasmi la Serikali. Bado tunasema kwamba lazima uhamisho huu uhusishe taasisi na Tume husika ili tuwape nafasi wafanyakazi wetu watumie ujuzi wao bila ya kujenga hofu kwamba mimi nikifanya hivi nitahamishwa bila ya matarajio.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye uwezo aliyetujaalia kufika jioni hii tukiwa wazima wa afya. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili nami niweze kusema machache mno juu ya mswada huu muhimu kwenye Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wako wameshazungumza vya kutosha juu ya mswada huu pamoja na ufupi wake kwa maandiko lakini ni mkubwa na una umuhimu wa aina yake. Kwa sababu hiyo basi, nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wauchukue mswada huu wa sheria kwamba kwetu sisi ni mzigo wetu tumeubeba na wale tunaowawakilisha kwenye chombo hiki tumewabebea. Hivyo basi, tutakachokifanya sisi hapa tunakifanya kwa niaba yao kama kitakua na heri kwao tutajipongeza wote na kikiwa na kasoro sisi ndio tutakaobeba lawama hiyo.

Mhe. .Spika, nataasaf kwa kusema hilo kutokana na mifano ambayo leo tunaipigia kelele na masikitiko makubwa kwa yale yaliyotangulizwa na wenzetu kabla yetu. Mhe. Spika, kwa kukumbusha dogo tu ili twende sambamba na waheshimiwa wenzangu ni pale wazee wetu pengine kwa nia safi kwa wakati huo lakini imekua tafsiri kwetu sisi si sahihi nia hiyo, na wale wenzetu ambao walikua wanaing'ang'ania pale ambapo sisi tulikua tunawasha moto kuikataa wakatwambia rukeni mtoje hali iko hivyo. Walikua wanasema vile kwa sababu ni sheria.

Sasa Mhe. Spika, hapa ni lazima tuwe makini sana kwa sababu tukiipitisha na ikishapata baraka za Mhe. Rais hii itatumika kua ni sheria. Itategemea ni muda gani itakavyodumu lakini pengine ikija ikivuta muda kama tulivyokujairithi sisi hiyo ninayoisema ina umri wa miaka zaidi ya arobaini na kitu sasa inaendelea kutusokota na ilipitishwa na wenzetu, wazee wetu. Mhe. Spika, pengine nitaitaja baadae lakini nakusudia kusema kwamba, Waheshimiwa Wajumbe tunamsifu Mhe. Mwanasheria Mkuu, tuna kila sababu ya kumsifu anastahiki sifa hizo Mwenyezi Mungu ampe uwezo zaidi aweze kututengenezea yale mazuri na yafutike yote yale mabaya.

Lakini mimi nataka nimsifu sana Mhe. Rais, Rais wa Zanzibar aliteua ndugu yetu, mwenzetu, Mwanasheira Mkuu wetu, alimuona na anamuamini amempa dhamana nzito kubwa tu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali sio jambo dogo. Lakini alilolifanya tena Mhe. Rais kumteuwa Mhe. Haji Omar Kheir akampa Wizara hii ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, amemuamini na mimi sina shaka naye na Waheshimiwa Wajumbe hatuna sababu ya kumtilia mashaka, hii shughuli anaiweza, lakini niwaombe Waheshimiwa wenzangu kwamba hawa ni watu wawili mambo haya na hasa kwa historia tunayoiona peke yao kama wao walivyo itawawiya vigumu kuyaweka mambo haya mazuri yaweze kuleta faida na maslahi kwa muda tunaouhitaji. Ni lazima tufanye kazi sote kama timu moja tuwasaidie ili mafanikio yaliyokusudiwa yaweze kupatikana.

Mhe. Spika, baada ya tanbihi hiyo mimi nataka kuchangia kwa ujumla. Kuna sehemu ya pili ya mswada kifungu cha 3(b), mchangiaji wa asubuhi Mhe. Salmin Awadh alikua na wasiwasi kwa maneno yale 'nafasi maalum, wataalamu, adimu'. Tafsiri inahitaji watu wenye ujuzi na uzeofu maalum yakamtia mashaka.. yalimtia mashaka kwa sababu tu ya uzeofu tulionao kwamba maneno haya yanaweza yakatoa mwanya kwa wenzetu ambao bado hawajataka, narudia, kwa wale ambao bado hawajataka kule ambako umma wa Wazanzibari wanataka twende, wapo. Sasa hawa ni wachache Mhe. Spika, lakini kwa sababu hii ni sheria wakipata *loop hole* za namna hii wanaweza wakafanya vibaya kwa kuisingizia sheria ndio wasi wasi uliokuwepo.

Sasa nimuombe Mzee wangu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba sasa tuna miaka 48 ya Mapinduzi Matukufu, masuala haya ya wafanyakazi adimu, wataalamu adimu, tufute sasa neno adimu, hebu tujipange kwamba tunachokitaka tuna miaka miwili kufika nusu karne, sasa

tukipata ile *three quarters* watakaojaaliwa wengi hatutofika tena, lakini tuwapangie wenzetu basi kwamba robo karne inayobaki hiyo kufikisha ile *three quarters* tuwe na kada hii, tupate kada ile, tuwe na hiki kwenye hii taaluma.

Mfumo wa elimu tunaokwendanao huu sasa tunabeba lawama na tunabeba lawama kwa sababu vijana wapo huku nje hawana ajira hawaajiriki, hawauziki, hawajiajiri wao wenyewe, wao wenyewe pia hawawezi kujiajiri, sasa tubadilisheni namna ya taaluma ya elimu yetu iweze kusaidia jamii yetu. Kwa kufanya hivyo masuala adimu nadhani tutaondokana nayo.

Mhe. Spika, Nam. 5 Kifungu cha 29 cha sheria mama kinafutwa, kilikua kinaleta mgongano baina ya Kamisheni na Mhe. Waziri kwa ile ripoti ya Mhe. Rais. Nilikisoma kwa makini kabisa nikaona kumbe Mhe. Waziri amepewa siku thalathini, Kamisheni ina siku tisini (miezi mitatu). Kwa hivyo, inaonekana kwamba ripoti ya Mhe. Waziri inatarajiwa itangulie na kama kwa siku thalathini itakua bado basi Kamisheni kwa sababu the *same report* ni hiyo hiyo ndio sasa iende itakua kuna kasoro hapo na ni *obvious* siku tisini kama bado chombo hiki kitawasilisha ripoti kwa Mhe. Rais.

Nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu alikusudia hivyo, nadhani kwa sababu hapa ni pahali mimi binafsi napaheshimu sana sina fani hii, lakini kinadharia naona kama inafanana hivyo.

Jengine Mhe. Spika, ni Katibu Mkuu Kiongozi kua atasaidiwa na Katibu Mkuu wa Utumishi. Hata mimi nilikua najiuliza Katibu Mkuu Kiongozi ni Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi. Je, atakapokua hayupo katibu huyu wa ofisi hii atafanya kazi za Katibu Mkuu Kiongozi? Ana uhusiano na Baraza la Mapinduzi? Nilikua najiuliza, huyu Katibu wa Utumishi hapa ametajwa ni msaidizi wa Katibu Mkuu Kiongozi. Tafsiri ya kirahisi unaweza ukaona akiondoka kiti kile msaidizi wake ndiye atakayekaa kumbe mambo sivyo, kule Baraza la Mapinduzi atakwenda mtu mwengine huyu atabaki kua ni msaidizi kwa masuala ya utumishi tu. Nadhani hali iko hivyo ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu cha 47 cha sheria mama kinarekebishwa sasa mimi nataka nizungumzie (b), (i) na (j) yake. Hapa hasa ndipo Mhe. Mwanasheria Mkuu na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora nakuombeni sana msije mkamuangusha Mhe. Rais. Kwenye Wizara na idara kuna manyago makubwa, Mhe. Spika, narudia kusema sisi ndio tutakaobeba kwa hivyo, tuwasaidie hawa wenzetu ili *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu wote kwa umoja wetu tufike salama.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nina mwalimu wangu mmoja tulikua tunamalizia dakika za mwisho za majeruhi, ilikua mitihani yake hakuna anayepata 50 hata siku moja, lakini alitwambia *"I want all of you to live in peace and not in pieces)."* Sasa *inshaallah* na sisi Mwenyezi Mungu atujaalie kwa rehema zake tufike salama na jahazi hii tuifikishe mahali stahiki tukiwa wote wenzetu watakaokuja kuturithi wasifie kazi ambayo watairithi kutoka kwetu.

Mhe. Spika, hapa ni kwamba itafanywa uchunguzi na ukaguzi wa kila mara wa usimamizi wa rasilimali watu. Kifungu (i) "Itahakikisha kuwa miundo ya utumishi wa umma, uendeshaji,

usimamizi, mahusiano ya utekelezaji wake katika utumishi wa umma unatathminiwa kila mara na kupendekeza kwa Waziri hatua ya kurekebisha kunapotokea matatizo ya utekelezaji."

Mhe. Spika, wamesema wajumbe wako kuna maeneo Mawizara yetu haya, ofisi zetu hizi wanahitajika watu waajiriwe wenye kada fulani sasa hivi matokeo yake hawaajiriwi hao wanachukuliwa wengine wapo hapa hapa. Sasa wenzetu hawa tukiwapa *challenge* hii peke yao nadhani tungewasaidia pia kwa kuwaambia ni mahali fulani, Wizara fulani iko hivi, kwa hiyo amekwenda kutenda wajibu wake sawa hakwenda tutaweza kuja kumsulubu hapa lakini tukimfungia hivi hatujamsaidia sana. Mimi ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe wale ambao wanazifahamu ni maeneo yepi kuna ukiukwaji wa sheria hizi tuwasaidieni kwa kuwaelekeza hasa.

Mhe. Spika, eneo hili la mara kwa mara mimi naomba ibaki hivi hivi kwa sababu kuna mtindo hivi sasa lakini wale wahusika ningewaomba sana badala ya kubadilishana mawazo wakatusikiliza kwamba kuna upande siku zote hao ndio wanaowakagua wenzao lakini wao hawakaguliwi. Sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Waziri hebu tubadilishieni hao wenye mawizara haya. Waheshimiwa Mawaziri Wizara zenu tunataka mjenge utamaduni kuna kukaguliwa Pemba wakaguzi watoke Unguja, kuna kukaguliwa Unguja wakaguzi watoke Pemba. Hebu tuone mtindo huu ujengwe huu utamaduni isiwe upande mmoja tu ndio unaojua kukagua wengine wajue kukaguliwa hapa hakutendeki haki.

Wafanyakazi hewa wapo kila upande na hapa ndipo hii mara kwa mara tunataka ibaki na maana na tafsiri kama ilivyoandikwa isibaki hivi. Mhe. Mwanasheria Mkuu mara kwa mara na maana halisi, wafanyakazi hewa wapo lakini siku zote wapo upande mmoja. Kuna watu wanalipwa mishahara ya kada ambayo haiwahusu, analipwa mtu mshahara wa kada anayoisomea hajamaliza hata mwaka lakini anapata mshahara huo haya tunayo hapa. Sasa mara kwa mara hii itafsirike kwa vitendo vyake. Mhe. Spika, kuna watu wanalipwa dola hapa wenzao wanalipwa shilingi za Tanzania kwa sifa zipi tunataka mkayatafute myapate halafu mtueleze yule ilikuwa si fani hii.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na jumla jumla nimpongeze tena kwa mara nyengine Mhe. Mwanasheria Mkuu lakini bila ya kusahau kile chombo cha kifungu cha 9 (b) namba 7 naomba kunukuu "Bila ya kujali masharti ya sheria hii chombo maalum cha serikali kinachohusika na usimamizi." Kote tulikotoka bahati mbaya ni kibinaadam hakikutajwa, naogopa pale pale kuja kuuziwa mbuzi kwenye gunia. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa maoni yangu mawili matatu. Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri na naishukuru sana serikali kwa kuweza kutuletea mswada huu muhimu ambao ni kiini cha watu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, huu ni Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka masharti bora ndani yake. Mhe. Spika, sheria hii mimi kwanza naipongeza sana na naiunga mkono kabla sijasema hayo nitakayosema. Kwa sababu kuna sheria mbali mbali zilizokuwa zina vikwazo vinatubana sana watu wenye ulemavu zikiwemo sheria za majengo na sheria za kazi mpaka hizo kwenye huo utawala wa umma katika kazi na masharti mengine yanayofuatana na mswada huu. Mhe. Spika, mimi nashukuru sana kuletwa mswada huu hii ni sheria mama

iliyofanya marekebisho na kufanya marekebisho mengine yatakayoonekana katika sheria nyengine.

Mhe. Spika, watu wenye ulemavu kwa sheria hii na wao tunaona labda tunaweza angalau tukavuta pumzi na sisi. Kuna sheria mbali mbali zilizokuwa zinatukwaza hata katika sheria za kuajiriwa katika taasisi za serikali, taasisi za binafsi na mambo mengine.

Mhe. Spika, kuna unyanyapaa dhidi ya watu wenye ulemavu katika hayo maofisi na kuonekana mtu mwenye ulemavu hawezi kitu chochote, akiajiriwa akija pale atatia watu madoa na mambo mengine. Mhe. Spika, ikipita sheria na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia atatupa uwezo tutaipitisha bila ya vikwazo vyovyote ili tuweze kupata msaada na sisi watu tuliokuwa hatujiwezi katika hizi sheria za nchi ziliomo katika sheria hii.

Mhe. Spika, mimi nampongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na nampongeza Mhe. Waziri na serikali kwa jumla kwa kutuletea mswada huu wa kuweza kutukomboa na kuweza kutuwekea masharti na sisi tutakayoweza kufanya kazi zetu bila ya vikwazo vyovyote.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa sina mengi ila nilitaka ninyanyuke niuunge mkono mswada huu ili wenzangu wasije kuona kuwa mimi huu mswada nimeudharau. Mswada umetugusa sana kwa sababu ni wa kurekebisha sheria mbali mbali na zimo sheria nyingi sana zilizokuwa sisi zinatutia mitihani na vikwazo.

Mhe. Spika, nauunga mkono mswada huu mia kwa mia pamoja na wenzangu na Mwenyezi Mungu akitujaalia mswada tutaupitisha ili uweze kututupia jicho la huruma. Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kuniwezesha jioni hii ya leo na mimi kupata fursa hii ya kuchangia hoja hii ya marekebisho ya Mswada wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011.

Mhe. Spika, pili nikushukuru kwa kunipa fursa hii lakini vile vile niungane na wenzangu katika kumpongeza sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kukubali mapendekezo ambayo sisi kama wizara tumeyapeleka serikalini na leo hii tunayajadili.

Lakini vile vile niungane na wenzangu wote na niwashukuru sana wajumbe ambao wamepata fursa ya kuuchangia mswada huu. Mimi katika mchango wangu Mhe. Spika, sitaki niingie katika katiba wala sitaki niingie katika vifungu vya sheria ambavyo Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa nguvu kubwa sana ametakiwa atoe ufafanuzi ili Waheshimiwa Wajumbe waweze kuelewa madhumuni ya marekebisho ambayo yamefanywa katika sheria hii.

Mhe. Spika, sisi wizara tumefahamu kwamba tumepitisha sheria kikao cha mwezi wa Januari mwaka 2011 na hatimaye Julai, 2011 Mhe. Rais amesaini sheria hii. Katika kusema hili nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wote wale waliosisitiza suala la usimamizi kwamba tunapotunga sheria ni vizuri tusimamie sheria ili tuweze kuzifanyia kazi vizuri.

Nataka niwahakikishie wajumbe kwamba marekebisho haya tunayoyafanya yanatokana na huo usimamizi katika kuitekeleza sheria hii. Baada ya kugundua kwamba kuna baadhi ya maeneo yana mapungufu ndio maana hatukujali kwamba sheria hii ni mpya imetungwa muda mfupi tumeileta Barazani ili hii sheria iweze kuwa na tija ya wananchi wa nchi hii kwa jumla.

Mhe. Spika, naomba nizungumzie zaidi suala la utendaji kuliko kuzungumzia taratibu za ufafanuzi wa kisheria na hilo eneo namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kama alivyoombwa na wajumbe atajitahidi kufanya hivyo.

Mhe. Spika, wajumbe wengi hasa waliochangia asubuhi katika kuchangia sheria hii wametushauri kuanzisha *human resource data base* yaani *data base* itakayokuwa na taarifa za watumishi wa umma. Kama nilivyosema kwenye *budget speech* yangu kwenye mwezi wa Juni ni kwamba sisi kama wizara tayari kitu hichi tumeshakianzisha kwa sababu sheria imetutaka tufanye hivyo na katika kuisimamia na kuitekeleza sheria basi tayari tumeianzisha.

Nataka niwahakikishie wajumbe kwamba *human resource data base* karibu vifaa vyote vinavyohitajika vimeshakuwa *installed* pale wizarani na hivi sasa tunasubiri kitu kidogo tu ambacho kitaweza kukamilisha hiyo *data base* yenyewe. Tunafanya hivyo kwa sababu ya kile ambacho tumekipokea kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Nataka niwahakikishie tutakapofika mwezi wa Juni wakati nakuja kuwasilisha hotuba ya bajeti yangu eneo hilo tayari litakuwa limekamilika na tayari tutakuwa tumeshalifanyia kazi na tutakuwa tunajua hasa wataalam tulionao ni wangapi na wanafanya nini na wapo katika maeneo yepi na yepi. Kwa hivyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba hilo eneo tayari tumelifanyia kazi.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa karibu na wajumbe wote kila aliyesimama kuzungumza hapa ni indhari ambayo tumepewa serikali na hasa sisi tunaosimamia suala hili la utumishi wa umma linaloshabihiana na suala zima la mikataba kwa wataalam maalum *(rare profession).*

Nataka niwathibitishie wajumbe kwamba kwanza ukiliangalia katika sheria hii kabla ya marekebisho na ukiliangalia marekebisho ambayo yameletwa hayo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wamekuwa na hofu nayo na mimi nawakubalia ndio sababu iliyofanya sasa kuja na marekebisho haya.

Mimi nataka niwahakikishie pamoja na kwamba waziri ndie amepewa mamlaka ya kutangaza hizi nafasi maalum haitakuwa waziri anaibuka tu na kuweza kufanya kazi ya kutangaza hizi nafasi. Isipokuwa kwenye utumishi wa umma kuna vyombo vinne kama wenzangu walivyokwisha kusema, kuna Tume ya Baraza la Wawakilishi, kuna Tume ya Utumishi Serikalini, kuna Tume ya Uajiri ya Mahakama, kuna Tume ya Idara Maalum.

Hizi taasisi ndizo zitakazoanza kupokea mahitaji ya watumishi au kada zitakazo kuwa ni muhimu kwao na kuangalia kama serikalini zipo basi zinatangazwa, kama serikalini hazipo vile vile zinatangazwa ili kwa ajili ya kutafuta wataalam hao katika maeneo mengine.

Wala serikali haikuwa na nia kabisa ya kufanya hivi kwa kuwaacha kwa lugha za mitaani kwa kuwaacha vijana wetu wasomi waliopo sasa solemba la hasha. Ndio maana tukasema kada maalum yaani wataalam wa kada maalum *(rare profession)* na ikatajwa mfano alipokuwa akiwasilisha hoja yake hapa Mhe. Mwanasheria Mkuu akasema kada ya afya na nyenginezo zipo na mifano ipo hai. Unaweza ukawa na madaktari katika hospitali au katika Wizara ya Afya lakini kuna *specialist* mmoja ambaye huna mwengine zaidi ya yule. Mwengine ambaye pengine wewe unamsomesha muda wake wa kumaliza chuo haujafika inakusudiwa mtu kama huyu.

Mhe. Spika, mfano mwengine naweza nikautoa ambao ni hai tuna wataalam wa kilimo ilitokezea kwamba Zanzibar nzima kwenye Wizara ya Kilimo kuna mtaalam mmoja tu wa masuala ya udongo, mtaalam huyu amemaliza muda wake ule wa kawaida ule wa miaka miwili na ule wa mwaka mmoja kwa mujibu wa Sheria hii ya Utumishi wa Umma inayompa nafasi Katibu Mkuu Kiongozi. Lakini wizara haijamuandaa mwengine kwa hiyo hatuwezi kusema kwamba Zanzibar tukose kabisa kuwa na mtaalam wa udongo lazima tuwe nae labda kama litatokezea la Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo, mtu kama yule kama yupo ndipo pale tume husika itakapoweza kuleta maombi yale kwenye vyombo vinavyohusika na hatimaye waziri atalazimika kuitangaza nafasi ile kwenye gazeti rasmi la serikali.

Kwa hiyo, nataka niwaombe wenzangu kwamba watuamini na mimi naikubali indhari ambayo wametupa najua indhari hii wametupa kutokana na mambo ambayo yamewahi kujitokeza huko nyuma. Nataka niwahakikishie kwamba hivi sasa tunakwenda kwa mujibu wa sheria hii. Niwatoe wasi wasi vile vile kwa vijana wetu wasomi ambao bado hawana ajira serikali inalitambua hilo na haisemi kwamba itawachukua wote lakini inatafuta namna ya kuweza kutatua tatizo hili hatua kwa hatua. Kwa sababu hawa ni vijana wetu kama walivyosema wajumbe tumewasomesha wenyewe na hii ndio nchi yao na wangependa pengine waitumikie nchi hii kama tunavyoitumikia sisi.

Kwa hiyo, nataka niwatoe hofu Waheshimiwa Wajumbe kwamba hili halina lengo hilo lakini inaweza ikatokezea kwamba kuna *profession* ambayo haipo. Kwa mfano, hivi karibuni Tume ya Utumishi Serikalini imetangaza nafasi za ajira ya walimu wenye diploma ya *science* na *degree* ya *art* lakini iwe sio dini na kiarabu peke yake. Hii haina maana kwamba mwenye dini lakini ana masomo mengine asichukuliwe, tunafanya hivyo kwa sababu inaonekana tatizo ni walimu wa sayansi. Nataka niwahakikishie kwamba katika hao walimu wa *science* tuliowataka na wa *degree* ya kwanza katika walimu karibu 1,350 walioleta maombi serikali uwezo wake ni kuajiri walimu 500, lakini tumemudu kupata watu 322 mchanganyiko kati ya hao *degree* ya kwanza ya *art* pamoja na *science*. Kwa hiyo, hili tunalizingatia na tunahakikisha kwamba serikali inapofanya basi itahakikisha inafanya kwa kuzingatia sheria. Sitaki nikubaliane au sitaki nikatae moja kwa moja kwamba masuala ya upendeleo huko nyuma hayakuwepo, lakini kwa kuifuata sheria ya sasa nafasi ya upendeleo haipo. Kwa pale nafasi za utumishi zinapotangazwa kuwa zinahitaji wataalam fulani kwa mfano taasisi inataka wataaalam 50 lakini waliojitokeza 300, hapo lazima taratibu za kuwafanyia *interview* zifanyike ili upate wale ambao wana nafasi za mwanzo katika wale 300. Kufanya vyenginevyo huwezi kupata nafasi hiyo kwa sababu nafasi kwanza lazima itangazwe na ikitangazwa lazima ufuate utaratibu.

Sasa mimi sitaki kukataa moja kwa moja lakini nataka niwahakikishie kwa hivi sasa jambo hilo kwetu sisi litakuwa ni gumu kuweza kufanya mambo ya upendeleo.

Nataka niwahakikishie kwamba toka sheria hii imesainiwa tumeweza kufanya uajiri kwa mara ya kwanza ni hao walimu lakini vile vile tumeweza kufanya uajiri kwa nafasi zile *rare profession* hasa madaktari. Unataka madaktari 50 au 20 lakini wanatokea madaktari watatu, sasa wewe unataka madaktari 20 lakini wapo watatu kwa hiyo lazima uwachukue wale watatu, lakini haina maana kwamba utawachukua bila ya kufuata vigezo.

Nataka nitoe mfano vile vile kwa hao wataalam wa Wizara ya Afya ambao wameletwa kwa ajili ya kuajiriwa wengine ambao kuna mambo mengine hawakuyakamilisha wamekuwa *disqualify*. Kwa mfano, mtu ana diploma yake ya unesi lakini cheti cha *form IV* kafoji taratibu zimetulazimisha kwamba mtu huyo tumuache ndio utaratibu na huo utaratibu upo kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Spika, katika jambo jengine la jumla ambalo lilizungumzwa hapa ni suala la *status* ya Makamishna wa Kamisheni ya Utumishi. Mhe. Spika, hawa ni makamishna kwa nafasi zao hawa ni kama chombo cha *tribunal*, ni chombo ambacho kinakutana kila baada ya muda fulani, si chombo ambacho kinakutana kila siku. Kwa msingi huo, utaratibu wao hawa masuala ya ku-*quote* katiba namuachia Mwanasheria Mkuu vile vifungu ambavyo rafiki yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu amevi-*quote* kwamba je, hawa wametajwa kwenye katiba wanalipwa mshahara au wanalipwa nini.

Mhe. Spika, hawa ni makamishna wanaofanya kazi zao kupitia vikao. Kwa msingi huo, kwa tafsiri ile ile ya katiba kule kwenye katiba inasema mshahara na posho. Pia kuna vifungu vyengine vinasema taratibu nyengine zitafanywa kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi. Sheria tuliyoipitisha Baraza la Wawakilishi hawa ni makamishna wanaofanya kazi kwa kupitia vikao na sio wafanyakazi wa kwenda ofisini siku zote. Kwa maana hiyo, malipo yao ni posho sio mshahara.

Lakini vile vile makamishna hawa *qualification* zao nyengine kwa mujibu wa sheria ili wawe makamishna wasiwe waajiriwa wala wasiwe watumishi wa umma. Ni watu ambao *retired* ndio wanaopata sifa hizi pamoja na sifa nyengine ambazo zimetajwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, kwa utaratibu na kwa mujibu wa sheria hii hawa si wafanyakazi wa muda wote, kwa maana hiyo hawa ni sawa sawa na bodi wanakutana kila baada ya muda wanafanya kazi zao kwa utaratibu ule wa kazi ambazo zipo kwao. Isipokuwa Sekretarieti ya Kamisheni ndio itakayokuwa inafanya kazi za siku kwa siku.

Mhe. Spika, suala jengine la jumla ni suala la kuwatunza wataalam wetu na hili limezungumzwa na wengi yaani tuwape maslahi ili wasikimbie. Mhe. Spika, mimi nakubaliana nao na ndio maana serikali kuanzia mwaka huu wa bajeti imewapandishia mishahara watumishi wa umma. Lakini moja kati ya vigezo vilivyotumika ni taaluma ya mtu, nia ya Serikali ni kuona kwamba hawa wataalamu wasitukimbie tunawapa maslahi ili washawishike kufanya kazi nchini kwao. Kwa hivyo, nakubaliana na wale waliosema kwamba ni vizuri ili wataalamu wetu wasitukimbie basi tuwape maslahi mazuri. Nasema Serikali imeanza na itaendelea mwaka hadi mwaka kutengeneza maslahi ya wataalamu wetu.

Vile vile Serikali kwa kupitia Wizara yangu tunaandaa utaratibu maalum wa mikataba maalum kwa watumishi watakaokua wanakwenda kusoma nje na namna tutakavyoweza kushirikiana nao katika kurudi kufanya kazi zao hapa nchini.

Tumeshauriwa kufanya utafiti wa wataalamu waliopo nchini kama nilivyosema, pamoja na zoezi ambalo sasa tunalifanya la mishahara, lakini vile vile tunafanyakazi hiyo ya kufanya utafiti kujua wataalamu ni wa aina gani na ni wangapi waliopo na kazi hii tayari imeshafanyika na hivi karibu tu ripoti itawasilishwa Serikalini na panapo majaaliwa chombo hiki nacho kitapata taarifa rasmi.

Mhe. Spika: Zingatia muda.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kua nitazungumzia yale mambo mengine tu, yale ya vifungu vya sheria nitamuachia mwenyewe Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Kuhusu kupima watumishi, limezungumzwa hapa na ni kweli tuliahidi, yaani wasipandishwe vyeo wafanyakazi pengine kwa upendeleo lakini kuwe na utaratibu wa kupima watumishi ili kujua vigezo gani vilivyofanya watumishi hao waweze kupandishwa vyeo. Suala hili nalo tumeshamaliza kazi na hivi karibuni tutaanza kuchukua hatua ya kutoa taarifa juu ya hatua ambayo tumefikia.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache napenda niwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wamechangia mswada huu. Mimi nataka niungane nao katika kumpongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kutukubalia kuja kuwasilisha mswada huu. Lakini ilitoka hoja kwa nini sekta husika isiwasilishe.

Nataka niseme kwamba sisi tungekua tayari kuwasilisha, lakini kwa sababu ya utaratibu uliopo huu mswada ulikuja katika marekebisho ya sheria mbali mbali, ime-*happen* kwamba ile sheria moja imeondolewa kwa muda iende kamati ikakae, ndio maana ameendelea kuiwasilisha Mwanasheria Mkuu. Lakini kama usingekuja kwa utaratibu huu, basi hii sheria tungeiwasilisha wenyewe. Hatutosita tutakapoona marekebisho yanayohitajika baadae, basi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba sio tatizo kuwasilisha sisi wenyewe hii sheria.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kufanya majumuisho ya hoja mbali mbali zilizotolewa na wajumbe. Pili naomba nichukue fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa wajumbe wote waliochangia.

Mhe. Spika, ni wazi kwamba michango yao itasaidia sio tu kuboresha sheria hii, lakini nadhani na taratibu za sheria nyengine na hata kwa katiba ya nchi yetu. Mswada huu umepata kuchangiwa pamoja na kuwa ni mdogo, lakini inaonesha umuhimu wake, umechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 17.

Mhe. Spika, kuna wajumbe ambao wamechangia hapa ndani ya Baraza, lakini na kuna mjumbe mmoja amechangia kwa maandishi. Kwa hivyo, wote wamechangia wajumbe 18 kwa jumla. Naomba niwataje kwa haraka haraka, kwa sababu ya muda.

1. Mhe. Panya Ali Abdalla
2. Mhe. Hamza Hassan Juma
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4. Mhe. Salmin Awadh Salmin
5. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
6. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
7. Mhe. Asha Bakar Makame
8. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
9. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
11. Mhe. Fatma Mohammed Said
12. Mhe. Mohammed Haji Khalid
13. Mhe. Subeit Khamis Faki
14. Mhe. Rashid Seif Suleiman
15. Mhe. Hija Hassan Hija
16. Mhe. Assa Othman Hamad
17. Mhe. Raya Suleiman Hamad
18. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora
19. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

Mhe. Spika, zilitolewa hoja mbali mbali, namshukuru Mhe. Haji Omar Kheir amezijibu baadhi yake hasa zile za utendaji. Kwa hivyo, mimi naomba nijibu kwanza zile hoja za jumla ambazo zilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi.

Kwanza ni kuhusiana na marekebisho yenyewe kwamba yamekuja haraka. Nadhani haikua hoja lakini wengi walipongeza. Tumeiona hiyo, lakini na mimi nataka niseme kwamba sheria ya utumishi wa umma inagusa mambo mbali mbali. Kwanza inagusa uhusiano baina ya mwajiri na mwajiriwa, yaani Serikali na watumishi wa umma, lakini inagusa utendaji wa Serikali na pia inagusa ufanisi wenyewe wa Serikali.

Kwa hivyo, ina mambo mengi na sheria yote uzuri wake na ubaya wake tutaijua baada ya kuanza kuitumia na ni mara ya kwanza kua na sheria *comprehensive* kuhusiana na utumishi wa umma kama hii. Tuliwahi kua na sheria hapo nyuma mwaka 1959 ilipopitishwa sheria ya utumishi wa umma kama hivi ya *public service* nambari 38 ya mwaka 1959, lakini baadae ikafutwa baada ya Mpinduzi.

Mhe. Spika, hii sheria ina haja ya kurekebishwa mara kwa mara na wengine wamo wengi watu wazima humu waliofanya kazi zamani, basi watakumbuka ile GO zamani ilikua inafungwa kwa *screw*. GO zamani ilikua sio kama hivi tunavyo-*bind* vitabu vyetu sikuhizi, lakini ilikua inatiwa *screw*. Madhumuni yake ni kwamba GO ni kitu kinachobadilika kila siku, hivyo unafungua *screw* unapenyeza yale mabadiliko halafu unafunga tena, kwa sababu kesho yanaweza yakatokea tena na keshokutwa na mwezi ujao vile vile. Sasa labda baadae hatukufahamu ndio maana sasa GO ilipoanza kufungwa kitabu kama hiki ikawa hakuna mabadiliko, tukawa tunafanyakazi kwa

mazoea kwa sababu hatukua na mabadiliko ya mara kwa mara. Lakini suala la sheria ya utumishi wa umma na kanuni zake ni kitu ambacho kitahitaji marekebisho ya mara kwa mara kama zilivyosheria za kodi.

Hoja nyengine iliyokuja ya jumla ni kwamba hivi vyombo vinavyosimamia utumishi wa umma vimekua vingi. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahakikishie kwamba hivi vyombo takriban ni vile vile, iliyoongezeka ni moja tu, ni *public service commission* nayo imekuja kama ni *regulator*, lakini *chief secretary* alikuwapo, Katibu Mkuu wa utumishi zamani alikuwa Afisi ya Rais, lakini hakutetea hii *mandate* maalum, hiyo ofisi kuu ya utumishi ilikuwepo zamani ikiitwa Idara ya Utumishi, lakini kutokana na matatizo yaliyotokezea ndio maana hii sheria imekuja kuirekebisha.

Hizi Tume zote za utumishi zilikuwepo. Kwa hivyo, kwa kweli hakuna kitu ambacho kimeongezeka isipokua zimekua *streamlined* kwa ajili ya kupata ufanisi katika usimamizi.

Suala jengine ni haja ya marekebisho ya katiba ya Zanzibar yaendane sambamba labda na mwenendo wa sheria zetu tunazozipitisha. Mimi nadhani Mhe. Spika, hoja hii leo tuiwache inaweza ikapata siku yake tukaizungumza. Lakini mimi niseme tu kwa ufupi kwamba nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kwamba kuna haja ya kuiangalia katiba yetu, kwa sababu ya maendeleo na mageuzi ambayo yanatokea kila wakati. Mhe.Spika, naomba niwaambie kwamba katiba muhimu ya kuiangalia ni utendaji wetu, ufanisi wetu na namna tunavyofanya.

Mhe. Spika, ukiangalia katiba ya Marekani, nchi yote ile basi ina karatasi 30, katiba yetu ina karatasi 95. Sasa unaweza ukajiuliza wenzetu wanaendesha vipi kwa karatasi 30 lakini sisi karatasi 95 bado tuna matatizo. Kitu cha msingi cha kuangalia nadhani tujitathmini sisi wenyewe tunavyoendesha mambo yetu, kama tukijitathmini basi naamini hii katiba haya mambo mengine ni rahisi kuweza kuyatekeleza.

Pengine kwa sababu tunakabiliwa na lile kubwa la marekebisho ya katiba ya Muungano, basi mimi nilidhani kwamba tusubiri yale marekebisho ya katiba ya Muungano halafu tuje na hii ya kwetu. Kwa sababu moja tu, kwa sababu tuwe na kitu kimoja, yaani tuwe na *unit of purpose*, kwamba sasa hivi tunachokabiliwa kua sote tu-*focus* katika hilo. Tukianza kua tunataka na marekebisho ya katiba ya Zanzibar, basi tutaparaganyika na hatutokua na *unit of purpose* katika jambo hili muhimu sana. Kwa hivyo, ni wazo zuri, lakini mimi nadhani wakati wake pengine sasa hivi sio muafaka kwa hili ambalo linatukabili mbele yetu.

Hoja nyengine iliyotolewa na wajumbe wengi, Mhe. Makamo Mwenyekiti alieleza kwa ufupi mambo ambayo yamejadiliwa katika mswada na nashukuru kwa kuyaunga mkono na mawazo ambayo aliyatoa vile vile Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ni wa pili katika kuchangia, nadhani mengi aliyoyazungumza basi Mhe. Haji Omar Kheir ameyatolea ufafanuzi.

Mhe. Spika, labda nizungumze suala moja tu ambalo lililozungumzwa na wengi kwamba kamisheni itakapopeleka ripoti kwa Mhe. Waziri na kama hajaipeleka kamisheni itajuaje. Mimi nadhani tungeyaangalia yale majukumu ya kamisheni, ukiangalia majukumu ya kamisheni ni kwamba kamisheni ni chombo ambacho kiko karibu sana na Rais na madhumuni ya hii ripoti kupelekwa kwa Waziri kwanza ni kwamba Mhe. Waziri yeye pia anatakiwa amshauri Mhe. Rais.

Kwa hivyo, baada ya kupata ripoti ni lazima aiangalie aone kama kuna jambo la kumshauri Mhe. Rais kuhusiana na ile ripoti kabla haijaja Barazani basi amshauri na kama kuna hatua za kuchukua basi hatua hizo zichukuliwe.

Mhe. Spika, pia yeye Mhe. Waziri mwenyewe ndiye ambaye ataileta Barazani. Kwa hivyo inabidi kuna mambo lazima ajiridhishe kama kuna ya kujibu hoja, kama ya kusawazisha ayasawazishe kabla suala lenyewe halijaja hapa Barazani. Kwa hivyo, ndio ilionekana kuna umuhimu badala ya kupewa kopi, maana ukipewa kopi sio yako hiyo ripoti, itakua ni ripoti ya Mhe. Rais, lakini ukiletewa wewe inakua ile ripoti ni ya kwako na unaweza ukachukua hatua na baadae ndio ukaripoti kwa mkubwa, ndio kitu rahisi kilichoonekana, lakini nia ni nzuri kwa ajili ya kusema kwamba ukileta Barazani tu haitokua na maana kama kuna vitu vya kurekebisha hukuweza kurekebisha.

Hivyo ilikua nia yake ni kwa ajili ya kumuwezesha Waziri na yeye kupata fursa. Lakini ndio tukasema aah! Inatokea au inaweza ikatokea basi akichelewa kamisheni yenyewe bila shaka itapata taarifa au inaweza ikapata taarifa yenyewe ikalipeleka hilo suala, maana yake huko tunakotoka haya mambo yameshawahi kutokea. Kwa hivyo, ndio maana tukasema *eventuality* hiyo ikitokea basi ni vizuri sheria iliweke bayana hilo. Lakini nia yake ni nzuri na nia yake ni kuimarisha na nia yake ni kujenga.

Jengine ambalo alilizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma ni suala la Mamlaka ya Tume ya Utumishi, suala hili lilizungumzwa pia na Mhe. Ismail Jussa na waheshimiwa wengine. Suala hili ni ule wasi wasi ambao mimi nasema ni wa msingi kwamba labda mamlaka yale ya Katibu Mkuu Kiongozi, mamlaka ya Katibu Mkuu Utumishi pengine yanaingiliana na Mamlaka ya Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, yeye alikwenda mbali zaidi akauliza kwamba je, hii haigongani na katiba. Lakini tunaposema kitu kinagongana na katiba ni lazima ueleze kimoja kimoja wapi vinagongana vitu hivi, maana vikigongana kuna *point of clash*, sasa *point of clash* ni pahala gani.

Labda nianze kwa utaratibu wa sasa hivi Mhe. Spika. Utaratibu wa sasa hivi ni kua Tume za utumishi zote hizi zina mamlaka ya kuajiri na kufanya *promotion*. Lakini kabla ya kuajiri kuna kitu kinaitwa kuamua idadi gani ya watumishi iajiri na wa aina gani iwaajiri. Sasa hiyo ni kazi ya kitu kinachoitwa *central establishment*. Serikali zote duniani zina kitu kinaitwa *central establishment,* yaani Ofisi Kuu ya Utumishi ambayo ndio inashughulikia *quantity* na *quality* ya watumishi wa umma kuamua kwamba Serikali kwa uwezo wake au kwa bajeti yake mara hii jamani tutaajiri watumishi 2,000 na 2,000 hao Baraza la Wawakilishi nyinyi tunawaruhusu muajiri 20, wengine 10 na wengine 30 na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali 200, Wizara ya Afya 500. Sasa hiyo kazi haifanywi na Tume ya utumishi maana inakua haijui na huwezi kui-*contol* ikiwa kila Tume ya utumishi ikiamua mimi nataka 2,000.

Kwa hivyo, hii Serikali yenyewe itafika pahala naona itazidiwa, itakua uzito wake mkubwa uliobeba kuliko hata uzito wake wenyewe. Sasa hayo ndio madhumuni ya kua na *central establishment.* Sasa ukishapata idhini ya *central establishment*, halafu ndio unakwenda kufanya uajiri. Hiyo ni kwa utumishi wa kawaida kwa *pensionable service.* Lakini inapotokezea ni utumishi wa *non pensionable service* ndio hapo anaye-*control* ni *chief secretary,* anasema

kwamba *ok* nyinyi mnataka mtu wa namna hii, ndio, basi *ok* tunatizama idadi tuliyonayo basi mnaruhusiwa. Sasa yeye anafanyakazi ile ile, lakini kwa *non pensionable service*, lakini yeye hafanyi kazi ya kuajiri wala hafanyi kazi ya ku-*promote*. Kwa hivyo, sioni pahala ambapo Tume ya utumishi ya Baraza na hivi vyombo vya *central establishment* vinapogongana kila mmoja anafanyakazi yake kwa mamlaka yake ambayo amepewa. Maana suala la kua kuna mgongano au hakuna mgongano, hilo ni suala la tafsiri, mimi ninachoomba ni kwamba tusiwe na madhehebu katika tafsiri katika chombo hiki. Sote tuwe na kauli moja.

Naomba nirudie Mhe. Spika, kwenye chombo hiki, kwa sababu bahati mbaya hapa sio mahakamani, kwamba tunaweza tukabishana kwa hoja za kisheria, jaji akaamua nani aliyekua sahihi. Mimi ninachosema ni kwamba kwenye tafsiri hapa ningeomba sana katika chombo hiki, kama kuna pahala hatujaelewana basi ni vizuri tukazungumza tukaelewana, tukasema na tukafanya utafiti, lakini tukafika pahala tukasema jamani hii ndio tafsiri ambayo tunakubaliana. Lakini tukianza kua na madhehebu ya Othmaniyya na Jusaiyya na Hamziyya hapo tutapata matatizo katika suala hili. Kwanza litakapotokea tatizo kwamba tumefanya maamuzi sisi ni kinyume na katiba, basi anayeshtakiwa ni Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, mmepitisha marekebisho ya 10 hapa, nasema Othman hakuwemo hapa kama ni Mwanasheria Mkuu sahihi, lakini sasa hivi anashtakiwa yeye Mwanza na bwana mmoja wa Kisukuma kafungua kesi Mwanza anashtaki Serikali kwa marekebisho ya 10 ya katiba, lakini anamshtaki Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ndio maana nikasema ni lazima tukubaliane kitu ambacho tunatoka nacho hapa. Mimi ninavyoona ni kwamba kwa kweli hakuna mgongano baina ya sheria hii na katiba hasa kuhusiana na mamlaka ya Tume ya utumishi ya Baraza la Wawakilishi.

Jengine ambalo Mhe. Hamza Hassan alilizungumza na wajumbe wengine walilizungumza vile vile ni kuhusiana na kuwepo kwa Ofisi Kuu ya Utumishi labda kuanzishwa na kulikua na wasi wasi kwa nini inaanzishwa. Mhe. Spika, hii ofisi haianzishwi ipo tayari kwenye sheria, isipokua sasa hivi kulifanyika makosa mawili, ile *cross reference* kama aliieleza vizuri Mhe. Ismail Jussa kwamba kilitumika kifungu cha 46 kufanya *reference* wakati ni kifungu cha 47, kwa hivyo ile tafsiri ikabidi ielezwe vizuri. Lakini pia ile *wording* tu ndio iliyorekebishwa, lakini haianzishwi ipo tayari na tulishaipitisha toka tulipopitisha sheria hii nambari 2 ya mwaka 2011.

Suala jengine lilikua nadhani nimeshalieleza ni kuhusiana na mamlaka ya *chief secretary* na mamlaka ya Baraza la Wawakilishi.

Hoja nyengine ambayo aliizungumzia Mhe. Ismail Jussa. Kwanza namshukuru Mhe. Hamza Hassan alieleza kuridhika kwake na masuala mbali mbali yaliyorekebishwa katika sheria hii. Namuahidi kwamba tutafanyakazi kwa karibu na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi, hii sheria nayo inatatizo la kufahamika kwa watumishi. Tunafanya maandalizi ya mafunzo maalum kwa watumishi wa umma kuifahamu hii sheria yenyewe ili iweze kutekelezwa vizuri zaidi.

Mhe. Ismail Jussa, yale ya indhari nafikiri Mhe. Waziri hapa ameshaeleza kuhusiana na *public service reform* kwamba iendane na *local government reform*. Naomba kumuhakikishia kwamba

hayo ya *local government reform* yamo katika hatua za utekelezaji, sasa hivi inakwenda sambamba na ile ya *legal sector reform*.

Mhe. Spika, labda nizungumzie yale masuala aliyotoa indhari na alihitaji ufafanuzi. Kuhusu suala la wastaafu kwenye hizi nafasi maalum. Ni kweli kwamba labda huko tunakotoka yalikua ni mazoea na huu ni mfumo ambao tumekwenda nao kabla ya haya mageuzi ambayo yanafanyika sasa hivi. Mtu akishakaribia umri anakwenda Mambomsiige anabadilisha cheti anapata kuongezwa muda wa ziada. Pia kuna mwengine anajulikana mwenyeji alwatani basi hastaafu, hayo yapo na yalikuwepo wala hatuwezi kukataa na ndio maana yakaja haya mageuzi. Hayo yaliyotokea ya kwamba watu kuajiriwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo hayo yalitokea kabla ya sheria hii. Kama tutakumbuka ni kwamba kabla ya sheria hii ilikua haijaanza kazi. Lakini sasa hivi ndio maana nikasema tumekuja na haya marekebisho kwa sababu tunataka kuyafanya yale *genuine case.*

Kwa mfano, ya Wizara ya Afya, lakini imeshindikana kwa sababu sheria hii inazuia. Kwa hivyo, kwa sasa hivi huu utaratibu nadhani unazingatiwa na Serikali iko *determine* kuyazingatia.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu cha 25 kwamba kwa nini kinafutwa. Kwa uhakika hakikufutwa isipokua kimebadilishwa msimamizi tu, ndio maana hivi vifungu vulivyofutwa huku vimehamishiwa kwenye kifungu cha 49, kwa hivyo utavikuta viko katika kifungu cha 49 vimeingizwa kule, ni vifungu ambavyo ni vya utendaji kuliko kuwa *regulator* ndio maana vikahamishiwa katika utendaji wa ofisi kuu ya utumishi.

Kuhusu lile suala la Rais kwamba Tume itajuaje kama Rais hajapelekewa, nadhani nimelijibu. Suala la mgawanyo wa madaraka, nadhani nimejaribu kulijibu na lile suala la Katibu Mkuu Kiongozi kwamba yuko juu ya Tume zote, nadhani nalo nimelijibu, kwamba kwa kawaida Katibu Mkuu Kiongozi hiyo ndio kazi yake, yeye ni *central establishment.* Kwa hivyo, kazi yake sio kuziingilia lakini ni kuzi-*regulate* hii *central establishment* kujua *quality* na *quantity* ya wafanyakazi na kuhakikisha kwamba yeye ni kama *internal auditor* kufanya kazi ya kuchunguza yale mambo ambayo Serikali yenyewe imeshindwa kuweka utaratibu. Sasa yeye ni mtu wa kuchunga *discipline* kabla *auditor* hajaja, ndio maana nikasema *chief secretary* anakua kama *internal auditor,* ndio maana haya mamlaka mengi aliyokua nayo zaidi ni ya *internal auditor* kuweka mambo sawa *discipline* na haya mamlaka mengine ni kwa sababu anafanyakazi zile za *central establishment* na yeye ndio kiongozi wa hiyo *central establishment* yenyewe.

Jengine lilikua ni suala la malalamiko ya utumishi, labda lile suala la hadhi zao, nadhani Mhe. Haji Omar Kheir alilieleza vizuri. Lakini ukisoma sheria, sharti la wao kulipwa mshahara ni kwamba Baraza hili limepitisha sheria inayosema wao walipwe mshahara. Mhe. Spika, Baraza hili halijapitisha sheria ya kusema wale makamishna walipwe mshahara, kwa sababu sheria iliyopitishwa ni hii ya *public service* ambayo inamkataza mtu ikiwa anataka kua kamishna basi asiwe mtumishi wa umma, kwa hivyo wao ile ni kamisheni na wanachostahiki ni posho. Kwa hivyo, ni sawa posho zao haziwezi kuwa sawa sawa na bodi, Serikali imeandaa utaratibu ambao posho zao ni tofauti na hizi posho za bodi. Lakini ni binadamu mtu hajaridhika, sasa hayo ni mambo yao wao na Waziri wao wa utumishi, labda wakifanya *engagement.* Humu ndani zimefanyika nyingi tu *engagement* za namna hiyo, sasa na wao vile vile wangefanya *engagement,* haya sio mambo magumu, kwa maneno ya siku hizi yanazungumzika. Lakini suala

la mshahara bila shaka hawastahiki kwa sababu sio watumishi ambao wameajiriwa kwa mkataba wala vyenginevyo.

Jengine ambalo alizungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kama alivyosema kuwa amesikia umbea na mimi nauchukulia hivyo hivyo. Lakini labda kwa kutanabahisha tu kwamba kuitwa kuna maana nyingi kwa kweli, lakini maana mbaya ambayo inahitaji mamlaka kisheria ni ile ku-*summon*. Sasa kama mtu *the fact* ana m-*summon* Waziri, *I think that, this is very wrong*, na hana mamlaka hayo. Hili ni jambo la kuambizana wazi kabisa kwa sababu sheria haijasema hivyo.

Mhe. Spika, kwa sababu *the fact* pia ni *cabinet secreteriety* ndio maagizo ya Mhe. Rais anayachukua mengine kuyapeleka huko kwa mawaziri. Sasa mengine yanahitaji mtu mwenyewe aende akayasikie. Sidhani kama ni kuitwa kwamba bwana njoo hapa unaitwa kama *senior officer* anavyoitwa na Katibu Mkuu, wala sio kwa sababu yeye ni mkubwa kuliko waziri, lakini ni suala la utendaji kazi, mimi sija-*experience* hilo.

Kwa mfano, wakati mwengine yeye anakuja ofisini kwangu, kama kuna jambo akinieleza, basi kwa *nature* ya hili jambo lenyewe namwambia nitakuja mimi na wala hahitaji kuniita, bila ya shaka mwengine hayuko *comfortable* na huo utaratibu inategemea na wakati mwengine.

Lakini madhumuni yake kwa kweli makubwa ninayoyaona mimi ni haya. Mhe.Spika, ni binadamu nadhani hayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu wameyasikia najua ni salamu na kama kuna tatizo hilo, basi salamu zimefika.

Mhe.Salmin Awadh Salmin kuhusu Bango Kitita. Mhe. Spika, Bango Kitita tatizo tulilonalo hivi sasa hatuna Sheria ya Kiswahili hii ya *Public Service*. Sasa kama tungeleta Bango Kitita la Kiswahili ungeshindwa kuli-*relate* na hii sheria yenyewe, ndio maana tukatayarisha kwa lugha ya kiingereza, ili ikusaidie kusoma hii Sheria ya kiingereza na hayo marekebisho. Kwa hivyo, ingekuwa Bango Kitita la Mswada basi tungeleta kwa Kiswahili na ndio tumeleta kibango kitita kidogo katika ule mswada, yaani kwenye yale marekebisho kwa lugha ya kiswahili, hivyo isingewezekana kufanywa kwa lugha ya kiswahili.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika tunaomba radhi kama Mhe. Mjumbe hilo lilimkwaza, lakini nia yetu ilikuwa ni nzuri kabisa na tuliona kwamba hatukuwa na njia yoyote nyengine ya kufanya. Kwa hiyo, tutajaribu mara nyengine vipi tunaweza kulifanya hilo kwa vizuri zaidi.

Mhe.Spika, suala jengine kuhusiana na Ofisi Kuu ya Utumishi na alikwenda mbali na kusema kwamba labda *A.G* atushawishi kwamba hicho kifungu kwa nini hakipingani na Katiba, nadhani nimejaribu kutoa maelezo. Lakini kama nilivyosema katika masuala haya tafsiri siku zote ni jambo ambalo watu mnaweza kutofautiana, ndio maana kuna rufaa, inatoka Mahakama Kuu inakwenda Mahakama ya Rufaa.

Kwa mfano, *last time* tulikuwa na Rufaa ya mbele ya Mahakama ya Rufaa ya Majaji saba, lakini mwenzao mmoja aliyekuwa Jaji Mkuu aliyepita akawa-*challenge* alisema walikosea, yaani majaji saba na wali-*argue* pale ni *professors* wawili pamoja na sisi wengine, lakini bado mwenzao mmoja yeye ameshaondoka akawaambia ata! Mlikosea katika uamuzi huu. Sasa hayo ni masuala ambayo ni ya kuzungumza na kupata tafsiri ambayo sote tunaweza kuitumia.

Vile vile kuhusu suala la Katibu Mkuu Kiongozi, nadhani nimejaribu kulijibu na jengine Mhe. Salmin Awadh Salmin alizungumzia labda matatizo yaliomo kwenye Katiba. Mhe.Spika, nafikiri nimeyaeleza kwamba mimi nakubali kwamba Katiba yetu inahitaji marekebisho. Lakini hivi sasa si wakati muafaka labda tujipe muda na suala hili tuliangalie kwa kina na tujue tunataka Katiba ya aina gani na baada ya hii Katiba ya Muungano. Je, Katiba yetu sisi sasa iwe ya namna gani?

Mhe.Makame Mshimba Mbarouk Mwanasheria Mdogo, anasema aya inamkwazwa najua yeye ni Alhajji lazima itamkwazwa, lakini ndio maana ya Kiswahili na wala hatuna neno jengine, labda tusaidiane tutafute neno zuri la Kiswahili, kwa sababu hii ni tafsiri ya *paragraph*. Sasa Mhe. Mjumbe akitusaidia kupata tafsiri au neno zuri lisilokuwa aya, basi tutashukuru na tutafurahi. *(Makofi)*

Kuhusu Asasi za Kiraia (AZAKI) kwamba zishirikishwe mara nyengine. Mhe.Spika, nakubaliana na Mhe.Mjumbe. *(Makofi)*

Suala jengine kubwa ambalo alitaka ufafanuzi ni kuhusu suala la uhamisho. Mhe.Spika, sheria kama ilivyo hivi sasa ni kwamba inatoa mamlaka na kuleta athari hiyo aliyoizungumza Mhe.Mjumbe. Kwa kweli hivi sasa Makatibu Wakuu au Wakuu wa Taasisi wanaweza kukubaliana mtu huyu ahamishwe bila ya kujulikana Utumishi na wakafanya hivyo.

Sasa ni binadamu inawezekana wana urafiki, pamoja na mambo mengine kama vile mitaa yao wanayotembea ni mimoja. Kwa hivyo, hili ndio likaonekana aa! Mambo ya serikali huwezi kufanya namna hii, basi angalau tuweke *control*.

Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba jibu sasa limepatikana, na pengine ile athari yupo Mhe. Waziri ukizungumza naye, nadhani anaweza kuzingatia kuona kwamba huyo mtu je hatua zilizochukuliwa zilikuwa zinastahiki, ama kulikuwa na tatizo, nafikiri ni jambo ambalo linaweza kurekebishwa.

Mhe.Abdalla Juma Abdalla nakushukuru kwa michango pamoja na ushauri wako, na lile na mswada kuwasilishwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, nadhani limejibiwa. Vile vile kuhusu suala la ripoti kupelekwa na waziri nalo pia nimelijibu.

Mhe.Asha Bakari Makame kuhusu suala la Jumuia ya Uamsho ambalo alilizungumza mwisho. Mhe.Spika, naomba niungane na Mhe. Mjumbe kwa kusema jambo dogo tu, kwamba mwelekeo unavyokwenda si mzuri sana. Hivyo ni vyema sote tukatanabahi kuwa linaweza kutuondolea, yaani kila mtu akivuta kwa upande wake, basi itatuondolea kile kitu kinachoitwa *unity of purpose*, lazima sote tu-*focus* kwamba sisi tunapotaka kwenda ni hapa, lakini mwengine akisema uvute huku na yule uvute kule. *(Makofi)*

Mhe.Spika, nadhani ni vizuri tukawatanabahisha wenzetu kwamba, fursa hii ambayo haijawahi kutokea na sidhani kama itatokea tena. Sasa kama hatukuitumia vizuri basi wa kwanza wa kuwalaumu ni wao, na kila mtu atawalaumu wao, kwa sababu wamewaondoa watu katika *focus*.

Kutokana na hali hiyo, basi ni vyema kuwaelimisha na watu wakafahamu na kuweza kutoa maoni yao, kuliko kuwawekea msimamo, mimi nadhani halitotusaidia. Mhe.Spika, suala hili kwa vyovyote vile hili halikuwemo kwenye mswada, lakini nilisema na mimi nili-*comment*, kwa sababu Mhe. Mjumbe amelizungumzia.

Mhe.Spika, mengi aliyotoa Mhe.Mjumbe ni ushauri na tumeupokea na Mhe. Waziri amejaribu kutolea ufafanuzi.

Mhe.Mahmoud Muhammed Mussa alitoa ushauri na tumeupokea pia.

Mhe.Mohammed Mbwana Hamad alisema kwamba kutakuwa na mgongano kati ya kifungu cha 29 kuhusu suala la waziri na ripoti, nadhani nimelizungumza kwa urefu na wala sina haja ya kulirudia tena.

Mhe.Spika, kwa kweli Mhe. Mjumbe alikuwa na wasi wasi kifungu cha 49, labda hawa watu kazi yao itakuwa ni kufanya ukaguzi tu, labda hili neno ni tatizo. Lakini kinachokusudiwa hapa sio ukaguzi wa mara kwa mara kwa maana ya kila siku, yaani sio *daily*, isipokuwa ni *regular inspection*.
Kwa hivyo, nafikiri wale walimu akina Mhe. Rashid Seif Suleiman wanajua kwamba *regular inspection* ndicho kitu ambacho kinatakiwa katika usimamizi na kilichokusudiwa ni hicho.

Mhe.Spika, kuhusu suala la mfanyakazi bora vigezo gani na alitaka ufafanuzi Mhe.Mjumbe. Lakini ukisoma hii sheria kifungu cha 102 kimeeleza na wala hakujawahi kuwa na sheria iliyotaka lazima uandaliwe utaratibu wa watu kupewa motisha. Kwa kweli sheria hii imeweka kifungu cha 102, yaani ukisoma kinamtaka waziri aandae kanuni za kuonesha namna gani watu watapewa motisha, mfanyakazi bora kwa njia za uwazi na zenye kufahamika.

Kwa hiyo, suala hilo limo kwenye sheria na hivi sasa imebakia kazi ya Mhe. Waziri kulifanyia kazi kwa ajili ya kuliweka sawa na mengi ilikuwa ni ushauri.

Mhe.Mwanajuma Faki Mdachi, mengi alitutanabahisha kuhusu mapungufu ya kiuandishi. Mhe.Spika, nadhani Mhe.Waziri kuhusu suala la *rare professional* alilitolea maelezo vizuri. Vile vile kuhusu suala la uhamisho kufanywa na Katibu Mkuu wa utumishi nafikiri limetolewa ufafanuzi pia.

Mhe.Fatma Mbarouk Said mengi aliyoelezea ilikuwa ni ufafanuzi, isipokuwa alikuwa na wasi wasi kwenye kifungu cha 65 kuhusu Kada ya Uhasibu.

Mhe.Spika, tukiangalia kuna kijifungu katika marekebisho ya kifungu cha 9 kuna kijifungu (b), sasa kile kijifungu (b) kimeongeza kijifungu kipya cha 7, ambacho kinasema kwamba hawa watu wa kada kama hizo wataendelea na utaratibu wao, almuradi wapate idhini ya Waziri wa Utumishi kama hawana sheria, ikiwa wanayo sheria, kwa mfano *CAG*, basi wataendelea na utaratibu huo. Kwa hivyo, hilo limewekwa bayana.

Mhe.Mohammed Haji Khalid mengi aliyoyaeleza ni ushauri na tumeupokea.

Mhe.Subeit Khamis Faki pia tunakushukuru na mengi aliyoyaeleza ni ushauri, na zaidi kusisitiza kwamba hii sheria isiwe ni *gamble*, lakini iwe sheria ambayo itatekelezwa kwa umakini.

Mhe.Rashid Seif Suleiman masikitiko yake mawili kwanza alianza nayo. Mhe.Spika, kuhusu suala la miswada kusomwa mara tatu, nadhani ukisoma ile Orodha ya Shughuli zitakazokuja Barazani ni pamoja na Marekebisho ya Kanuni, ili kufanya hilo liweze kutekelezeka. Kwa hivyo, tunategemea baada ya hapo kuanzia Kikao cha Juni itakuja miswada kusomwa kwa mara ya kwanza na halafu iletwe tena Kikao cha Oktoba wakati huo, kwa hivyo litaanza karibuni.
Mhe.Spika, suala jengine ni ushauri wa kufanyiwa semina, na kwamba huko tunakokwenda, basi hizi semina ziweze kuandaliwa.

Vile vile Mhe.Mjumbe alizungumzia kuhusu suala la waziri kupelekewa ripoti, nadhani tayari nimeshalitolea ufafanuzi. Mhe.Spika, labda niseme tu kuwa *actual* itakayopelekwa sio *same report*, yaani ukisoma pale ilivyoandikwa pale sio *the same report*, lakini inasema *shall submit the same*.

Mhe.Spika, kwenye Kiingereza cha Kisheria ukeshasema hivyo inakuwa sio *adjective*, yaani *same* inakuwa sio *adjective* na inakuwa ni *pronoun*. Kwa maana hiyo, ile ripoti yenyewe ndio inayozungumziwa kwa kutumiwa neno *same*, hivyo kitakachopelekwa ni ripoti iliyorekebishwa ama kama hivyo ilivyo, lakini haina maana kwamba ni *same report*, lakini the *same* kwa maana ya ripoti.

Kwa kweli mengi aliyoyaeleza Mhe.Mjumbe yalikuwa ni ushauri.

Mhe.Hija Hassan Hija na yeye pia alitoa ushauri kwamba tufanye mapitio ya hizi sheria, tunauchukua ushauri wake na ninamuahidi kwamba tutaufanyia kazi. Mhe.Spika, pia nakubali ule ushauri wake kwamba labda wakati wa kutangazwa hizo nafasi basi Mhe. Waziri kushauriana na Tume ya Utumishi husika.

Lakini nafikiri si jambo baya, kwa sababu *after all* wale Tume ya Utumishi wenyewe ndio watakaojua labda ni nafasi zipi zilikuwa zimepata maombi ya kuajiri.

Kwa hivyo, nakubaliana na hoja yake pamoja na yale mapendekezo yake kwamba suala la uhamisho kuwe na sababu za msingi katika kufanya hivyo.

Kwa kweli nadhani tutakuwa tunaongeza, lakini kimsingi ndivyo inavyotakiwa na kwa kuondoa wasi wasi sidhani kama hilo litakuwa ni tatizo, na ninaomba iwe ni marekebisho kwamba tutayaongeza katika maneno ya kile kifungu, nikubaliane naye yale maneno ambayo ameyapendekeza.

Mhe.Asaa Othman Hamad, nadhani ile tafsiri uliyotaka ya wataalamu wa dini. Nadhani Mhe. Waziri ameyatolea ufafanuzi na ushauri wako kwamba Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali afanye kazi kuondoa hii ya dini. Nadhani nayo Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ameyasikia.

Kwa ufupi sasa hivi tatizo kubwa ni kwamba hizi *rare disciplines* zinaibuka kila siku. Leo utakuja na *discipline* hii kesho utakuja na nyengine kwa sababu *technology* inaendelea kila siku, watu kila siku wanavumbua na wataalamu ni kidogo. Hilo sio jambo geni, kwa sababu hata wenzetu nje nchi kama Uingereza iliyoendelea zamani, Marekani wanawachukua wataalamu wa dini kutoka nchi mbali mbali.

Vile vile hata hapa kwetu utashangaa kwamba, moja katika wataalamu wa *forensic* katika mambo ya *Digital Forensic* ni mtaalamu ambaye anayetoka hapa Zanzibar.

Mhe.Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu, nadhani muda unakaribia kumalizika, kwa hivyo ili tuimalize kazi hii nafikiri tuwaombe wajumbe wakubali kufanya hivyo.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliobakia hautoshelezi kumaliza kazi iliyo mbele yetu. Kwa hivyo, nakuomba uliombe Baraza lako tukufu likubali kuongeza muda, ili tuweze kumaliza shughuli zilizopangwa kwa leo. Mhe.Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe.Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe.Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe.Mwanasheria Mkuu: Mhe.Spika, nakushukuru. Mhe.Asaa Othman Hamad mengi aliyoyaeleza ilikuwa ni ushauri kuhusiana na ile tafsiri ya Katibu Mkuu wa Utumishi na Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi, kwamba ni Msaidizi wake, nadhani ameieleza vizuri.

Vile vile ile indhari yake ya kufanyika kwa uchunguzi wa mara kwa mara, nafikiri Mhe. Waziri amesikia kwamba, labda wakaguzi wasiwe wao kwa wao, yaani kesi ya ngedere ukampelekea ngedere pia. Kwa kweli ni ushauri mzuri na Mhe.Waziri ameusikia.

Mwisho Mhe.Spika, naomba nimshukuru Mhe. Raya Suleiman Hamad kwa mchango wake, na kutupa moyo pamoja na kuungana na sisi katika kuunga mkono mswada huu.

Mhe. Spika, mwisho kwa kumalizia naomba sana kwa yule ambaye anahisi hoja yake sikuijibu, basi ni kwa sababu zaidi ya muda.

Mwisho nilimsahau Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yeye alifafanua hoja na pia namshukuru kwa kunisaidia kujibu mambo mengi ya msingi, ambayo nadhani Waheshimiwa Wajumbe wameyafahamu.

Mhe.Spika, kubwa niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwamba wote wameunga mkono mswada huu, hata Mhe.Makame Mshimba Mbarouk Mwanasheria Mdogo naye alisema kuwa huu anaunga mkono. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba baada ya hapo tuupitishe, ili tuwawezeshe sekta husika waweze kufanya kazi vizuri na tuiwezeshe serikali kuweza kuendelea kufanya mageuzi katika Utumishi wa Umma. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja.

Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe.Spika, naafiki.

Mhe.Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria
mbali mbali ya mwaka 2012

Mhe.Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa taarifa.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria
mbali mbali ya mwaka 2012

Kifungu cha 1 - Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 2 - Kusomwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 3 -

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 3(b) kilichozungumzia kuongeza kwa tafsiri ya maneno mapya yafuatayo kwa mpangilio wake kwa kiherufi, yaani nakusudia hili neno ambalo lililotiwa kwenye *inverted comma* “Nafasi Maalum” ambayo na tafsiri yake kama inavyooneshwa kwenye kifungu cha 60.

Mhe.Mwenyekiti, nimesikia ufafanuzi wa Mhe.Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa kweli hoja hii ilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi kuhusu hii Nafasi Maalum, yaani tunakusudia hii iwe ile nafasi ambayo inaweza kupewa mikataba maalum.

Mhe.Mwenyekiti, kama ulifuatilia basi Waheshimiwa Wajumbe wengi walikuwa wanajaribu kusisitiza hapa, kwa sababu hizi sheria Mhe. Mwenyekiti tunazitunga nyingi tena nzuri, lakini tatizo linakuja pale kwenye utekelezaji.

Sasa katika hili Mhe.Mwenyekiti, hivi karibuni tulipitisha sheria hapa, kwenye sheria ile Mhe.Mwenyekiti naomba kutoa mfano, kwamba nafasi ya Mkurugenzi anatakiwa awe na *degree* ya kitu fulani, lakini Mhe.Mwenyekiti, hapa sifa zile hazikuzingatiwa.

Kwa maana hiyo, kuna vitu vizuri tunavitengeneza kwenye sheria, lakini ukija katika utekelezaji na hapa Waheshimiwa Mawaziri wanatuambia kwamba tuwaamini. Lakini katika kuamini kuna suala baadae linakuja, yaani ukija kumchunguza mtu yule basi utaona amekuwepo pale kinyume na ile sheria ambayo tumeipitisha.

Mhe.Mwenyekiti, hapa nilikuwa najaribu kutoa angalizo kwamba hebu hivi sasa na Mhe. Mwanasheria Mkuu amezungumza vizuri kuwa Katiba ya Marekani ina kurasa 34 tu, lakini wanazitekeleza, yaani ile Katiba kurasa zake ni 34 na zinatekelezwa kama zilivyoandikwa. Mhe.Mwenyekiti, sisi tunazo 93 na wala hatuzitekelezi na badala yake tunatumia uzoefu pamoja na mambo mengine, nafikiri tunatumia *business as usual*.

Kwa hivyo, ni vyema tubadilike kama maneno ya Mhe. Rais wetu hebu tuzifuateni hizi sheria, na wenzetu Uingereza wao hata Katiba hawana, lakini mambo yao yanakwenda kutokana na yale maandiko yake. *(Makofi)*

Mhe.Mwenyekiti, tuendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, alisema mapema kwamba anatoa angalizo. Tunaendelea. *(Makofi)*

Kifungu cha 3 -

Mhe.Salmin Awadh Salmin: Mhe.Mwenyekiti, ahsante.Wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia juu ya suala la Mhe.Mwanasheria Mkuu au Mhe. Waziri yeyote anapoleta sheria ya kufanya marekebisho madogo madogo, basi ni vyema tukatayarishiwa Bango Kitita.Vile vile nilisema kwamba Mhe. Mwanasheria ametuletea Bango Kitita kweli, lakini limeandikwa kwa lugha ambayo sio rasmi inayotumika katika Baraza hili.

Mhe.Mwenyekiti, wakati alipokuwa akifanya majumuisho Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema kwamba sheria zetu zote ambazo zinazoandikwa hivi sasa zinaandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Mhe.Mwenyekiti, nadhani unakumbuka kwamba tulikubaliana katika vikao vya awali kwa kuwa sheria tunazozipitisha hapa ni sheria ambazo zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili, basi Mhe. Rais anapopelekewa kwa ajili ya kusaini ni vyema apelekewe sheria zote mbili, yaani Sheria ya Kiingereza na Sheria ya Kiswahili. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu anaposema kwamba sheria zote zilizokuwepo zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, basi nadhani itakuwa bado tunakiuka yale makubaliano ambayo

tumekubaliana na ni mambo ambayo yanakwenda kinyume na Katiba yetu ya nchi. Kwa hivyo, ushauri wangu sheria tunazozipitisha ni vyema tuendelee kuziandika kwa lugha mbili, yaani ya Kiswahili na Kiingereza na hizo anazopelekewa Mhe. Rais kama tayari ameshawahi kupelekewa au bado, lakini tumekubaliana kwamba sheria ziwe mbili ambazo Mhe. Rais atasaini.

Mhe.Mwenyekiti, kwa sababu sheria hii ya Kiingereza inakuwa inatumika pale panapohaja, lakini sheria zinatakiwa ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili, ambayo ndio lugha rasmi ya wananchi wa Zanzibar na wataweza kuzifahamu vyema. Mhe.Mwenyekiti, naomba tuendelee, lakini kwa huko mbele tunakokwenda kama Mhe. Waziri anawasilisha marekebisho madogo, basi atuletee Bango Kitita ambalo limeandikwa kwa lugha ya Kiswahili.Ahsante. *(Makofi)*

Mhe.Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wengine wamesikia, kutayarisha kama ni Mabango au Vibango Kitita viwepo tena kwa Lugha ya Kiswahili.Tunaendelea. *(Makofi)*

Kifungu cha 3 - Marekebisho ya Kifungu cha 3 pamoja na marekebisho.

Kifungu cha 4 -

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba uniruhusu nimpongeze sana Mhe.Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ufafanuzi wao mzuri na wa kina kwa vifungu vyetu tunavyoviibua katika mjadala hapa, na ndio maana hakuna masuala mengi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe.Mwanasheria Mkuu kupitia kwako Mhe.Mwenyekiti anisaidie kitu kimoja. Wakati alipokuwa akijibu hoja au mchango wangu nilioulizia kwa nini tumefuta kifungu L na N. Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema kwamba kimsingi havikufutwa isipokuwa vimehamishiwa na alinielekeza kwenye kifungu cha 49 kama sikosei, ambacho kimerekebishwa sasa kwa kuongezwa kifungu kidogo cha (b) ambacho kimeongeza vifungu vya (i), (j) na (k).

Sasa nimeviona Mhe.Mwenyekiti, lakini ukitizama *construction* ya vifungu hivi vilivyoondoshwa na hivi vipya kidogo kuna tofauti, nilikua naomba Mhe. Mwanasheria Mkuu katika hilo kidogo anisaidie na kile kilichopo katika (i) na (j) ambacho naweza kusema vimeunganisha na (a) havinipi shida sana. Lakini hichi cha (n) kilichofutwa Mhe. Mwenyekiti kinazungumzia *to issue and review public service staff manual from time to time.*

Hiki kilichoongezwa kinazungumzia *to issue and review from time to time public service guide manual*, sasa nilivyofahamu mimi tangu tunapitisha sheria mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, kwamba *Staff manual* mimi nilidhani ile *manual* ambayo itakua na orodha ya watumishi wa Serikali kama ilivyokua zamani. Lakini hapa kumeonesha utofauti kumeongezeka na staff na neno *guide* hebu naomba atusaidie hasa, dhamiri ya kilichokusudiwa hapa ni nini hasa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti kwanza nikubaliane na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba kile kilichoondolewa na hichi kilichoongezwa hapa kina tofauti ndogo katika matumizi ya neno badala ya *manual* kutumia *guide line*, hili ni suala la lugha tu lakini tunasema kwamba wengine wanaita *manual wengine hizo guide*. Lakini madhumuni yake mule yanakubaliana

isipokua tulisema kua labda neno zuri la kutumia ambalo halitomkanganya mtu maana *manual* sisi tupo tuliopitisha sheria tuloiona lakini kwa mtu mwengine baadae anaweza kuja kuuliza hii *manual* maana yake ni kitu gani.

Sasa hapa uliokusudiwa hasa ni muongozo wa hatua kwa hatua katika utendaji wa shughuli za serikali, ungeweza kutumia *manual* lakini tumeona neno zuri kusema hizi *manual* zaidi ni miongozo ya jumla, kwa hivyo ni suala la lugha tu lakini kilichokusudiwa ndio hicho hicho.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, majibu ya Mhe. Mwanasheria Mkuu yamenikanganya zaidi, kwa sababu hiki kilichoongezwa kimetolewa yote mawili *guide manual* ninachouliza mimi baina ya *staff manual* na *guide manual*, sio kwamba huku kuna *staff manual au* kuna *staff guide*. Huku kulikofutwa kwa Kiswahili imeandikwa "*Itatoa na kufanyia mapitio mara kwa mara kitabu cha muongozo wa utumishi wa umma".* Ambacho nakipata kwenye ukurasa wa 52 kifungu cha 7, lakini huku kulikofutwa ndio niliko mimi Kiswahili chake hatukukiona lakini kwa kiingereza ambayo ndio lugha ya sheria tulivyoambiwa hapa, kwamba pametumika "*to issue and review public service staff manual from time to time".* Huku kumeandikwa "*to issue and review from time to time the public service guide manual"*.

Sasa ndio maana nikasema yeye kanambia tofauti ya *guide* na *manual* hapa katika kifungu hichi yametumika yote mawili, sasa kama ungetumia *Staff guide* nitaweza kuelewa hiyo aliyosema sasa nataka tujue hapa tunapatisha nini Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nikiri kwanza kwamba mimi bahati mbaya nilikua nasoma ya Kiswahili na kichwani mwangu ninacho kile ambacho tulikubaliana neno la kutumia kwamba ni *staff guide line* kuliko kutumia *staff manual* ndio ambalo tulikubaliana na watu wa utumishi, wao ndio walilolipenda na kusema ndio neno zuri zaidi. Sasa labda kwa huu wa kiingereza labda tufanye marekebisho kwa kuzingatia kile ambacho tulikubaliana, hata hicho cha Kiswahili kinaelekea huko huko maana yake ni kitabu cha muongozo ambacho ni *staff guide line* ndio kilichokusudiwa hasa.

Mhe. Imail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nimeridhika naomba tuendelee. Ahsane sana.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo neno sahihi liwe ni *staff guide line.*

Kifungu cha 4 Marekebisho ya kifungu cha 25 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 5

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili kupata ufafanuzi wa ziada kwa Mwanasheria Mkuu, Mhe. Mwenyekiti nilipokua nikichangia nilipojaribu kuzungumza kifungu cha tano marekebisho ya kifungu cha 29(1) imezungumzia suala la kwamba kamisheni isiwe zaidi ya miaka mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri. Mimi sentensi hii yote sina matatizo nayo lakini tatizo lilikuja hapa niliuliza suala Mwanasheria Mkuu kajibu kama sheria vile ilivyoeleza mimi nimefahamu.
Lakini tatizo langu lipo hapa je, kwa kua kamisheni wameshapewa muda siku thalathini kwa kupeleka ile ripoti yao kwa Waziri na baadae wampelekee Mhe. Rais, lakini vile vile akasema

kwamba kama ikifika kipindi cha huo mwezi mmoja kama Waziri hajaipeleka kwa Rais wataipeleka wao wenyewe. Sasa hapa nataka kujua kutakua na mawasiliano gani baina ya kamisheni na rais ili kujua kwamba Waziri ameshapeleka ile ripoti. Sasa hapa kidogo nilikua nataka ufafanuzi wa ziada akinifafanulia vizuri tu nitakua sina matatizo. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nilijaribu kueleza labda ilikua ngumu kwa sababu muda kufahamika, nilichosema ni kwamba hiki ni kifungu ambacho kinawekwa ya kwamba muda umefika na waziri ameshindwa, sasa hapa sio waziri kushindwa hata lile alilozungumzia Mhe. Fatma pale kwamba Waziri kwa kawaida hawashindwi, lakini Waziri ni binaadam inaweza ikatokezea dharura yoyote ya ugonjwa haya ni mambo ambayo yanatokea kwa kawaida.

Sasa ndio ninaposema kwamba inapotokea dharura hiyo tatizo ni kuja kuijua wao watakua na haki sasa ya kupeleka moja kwa moja, maana yake isiwe kikwazo kwamba wamsubiri Waziri ndio aipeleke, kwa sababu na wao ni washauri wa Rais katika masuala ya utumishi ndio maana tukasema suala la watajua mimi siwezi kusema kwamba watajua kwa utaratibu gani, lakini uwezekano na haki ya kujua pia wanayo labda wanaweza kuuliza kwa sababu wanayo haki ya kuuliza na wakijibiwa kwamba haijapelekwa basi wao wenywe wana haki ya kuipeleka maana hawajazuiwa na sheria haijawazuia kuuliza suala kama hilo na wakapata majibu sahihi.

Kwa sababu na wao ni watu wa karibu ni chombo cha karibu cha Mhe. Rais cha kumshauri katika hili, hii imewekwa ikitokea dharura kama hiyo wao waweze kuitumia kwa ajili ya kukuza ufanisi katika masuala haya.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua tunatunga sheria na tunapotunga sheria inapotoa muongozo, lakini sasa huu muongozo ikawa kidogo hasa haujaonesha ule utaratibu wa moja kwa moja kidogo inanipa mashaka, kwa sababu mfano kamisheni imeshampelekea ripoti Mhe. Rais na kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu katika ufafanuzi wake pale mwanzo kwamba kwanza ile ripoti anayopelekewa hasa ni Mhe. Rais lakini kwa kua yeye haingii hapa barazani moja kwa moja kwa utaratibu wa kawaida wanaingia Waziri, ataingia Waziri aliyempa majukumu yale.

Sasa anasema kwamba Waziri anapopelekewa na yeye anatia zile *input* zake lakini sasa kama hajapeleka kwa Rais inaonesha hata zile *input* zake atakua hajapeleka, sasa hii hatuoni kama haijaoneshwa kwamba lazima kuwe kuna utaratibu wa wao kuwasiliana na Mhe. Rais kuliko wao tu kujipeleka kule.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tukubali katika kazi zetu wakati mwengine kuna *conflict* za ndani pengine baina ya fulani na fulani pengine kama inawezekana hata kama kuna mswada fulani wa sheria umetakiwa kwamba ndani ya siku fulani iwe imeshamfika Mhe. Rais na anatakiwa katika ile sheria vile vile anatakiwa ndani ya siku fulani awe ameshafanya kitu fulani Mhe. Rais na hiki pengine kitakua hakijafanyika. Nani atakua na mamlaka sasa ya kupenya akenda kumkumbusha Rais unajua tunapitisha sheria lakini tunaangalia na uzoefu, tunataka yasije yakatokezea matatizo madogo madogo hapa lazima kitajwe kiungo au lazima kuwe na utaratibu ambao utakaofata kupata ile message.

Kwa sababu inawezekana Mhe. Waziri ameshapewa pengine ana shughuli nyingi na safari nyingi maana kuna wengine hawakai hapa, akitoka Dubai anakwenda Uingereza Air port tu yeye hata ofisini haonekani, sasa inawezekana kwamba mwezi umepita lakini suala halijafanyika Mhe. Mwenyekiti, ukiona hawa watu wa Kenya hayo mambo ndio yanavyotokea.

Sasa hebu atusaidie Mhe. Mwanasheria Mkuu ili yasije yakatokezea matatizo kama ambayo yanaweza kutokezea. Ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Kama ingelikua Mhe. Hamza anayo ile sheria ningemwambia labda asome kifungu cha 26 kifungu kidogo cha kwanza kuhusiana na mamala ya kamisheni ya utumishi wa umma, ina mamlaka ya kutaka taarifa kutoka kwa Afisa yoyote yule na kuchukua hatua kadri itakavyoona inafaa, kwa hivyo mamlaka ya kupata hizi taarifa kama nilivyomwambia. Lakini na sheria chini ya kifungu cha 26(1) imeipa tume hii au kamisheni hii mamlaka ya kutafuta hizo taarifa na kuzipata na kuzifanyia kazi na ukichanganya na mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 25 hilo wala sio jambo kubwa, wala sio jambo ambalo haiwezekani tume kulifanya na ndio maana likawekwa kwenye sheria kwamba inapotokea hivyo basi waweze kuifanyia kazi. Kwa hivyo mimi naomba kumhakikishia Mhe. Hamza Hassan Juma labda wasiitumie ipasavyo kifungu cha 26 lakini tukiitumia ipasavyo basi uwezo huo ni mdogo sana katika kufanya kazi zake.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kuna kitu kidogo Mhe. Jaku kanipa kitu kidogo kimezidi kunipa tafrani lakini kimenifurahisha, sasa mimi nafikiri ile *message* ambayo umekusudia kuipeleka kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu nadhani ajaribu kuiangalia hii sheria sawa tutaipitisha lakini ili yasije yakatokeza matatizo haya ambayo tunahisi yakitokezea yanaweza kutupa *implication* katika hizi sheria zetu.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee.

Kifungu cha 5 Kufutwa na kuandikwa upya

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kimsingi kuhusiana na kifungu hiki sina marekebisho zaidi isipokua katika majumuisho yake Mhe. Mwanasheria Mkuu kuna maneno kayatamka na bila ya shaka yameingia hata Hansard kwa mtazamo wangu nahisi kama si sahihi Mhe. Mwenyekiti ningependa tuelewane. Kwa sababu baadae itakuja kutizamwa dhamira ya watunga sheria itakuja kuangaliwa kwa umoja wake.

Mhe. Mwanasheria alipokua akijibu hoja zetu kuhusiana na suala hili hili la ripoti badala ya kupita kamisheni kwenda kwa Waziri halafu kwenda kwa Rais nani atajua vipi, alitwambia katika maelezo yake kwamba ripoti ikenda kwa Waziri inakua ni ya Waziri halafu anaipeleka kwa Rais kwa sababu pia madaraka yake ni mshauri wa Rais katika masuala ya utumishi wa umma, lakini kilichonitatanisha mimi aliposema kwamba hii inampa nafasi kwa sababu baadae yeye ndie analeta katika baraza la Wawakilishi pia kuona kama kuna haja ya kuifanyia marekebisho kama kuna vitu ambavyo vinaweza kupasua hoja zile. Hili ndio lililonitia wasi wasi na kwa hivyo naomba ulifanyie marekebisho kabisa.

Mimi nilivyokisoma kifungu hiki hakitoi mwanya huo na naomba ibaki hivyo kwa dhamiri ya watunga sheria hii, kifungu hiki kinasema kamisheni 29(1) sio zaidi ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka juu ya hali na ufanisi wa utumishi wa umma na Waziri ndani ya siku thalathini ataiwasilisha kwa Rais, iwapo ndani ya siku 30 Waziri atashindwa kuiwasilisha kwa Rais kamisheni itawasilisha ripoti hiyo kwa Rais.

Sasa kwenye Baraza la Wawakilishi inakuja cha pili hapo mara baada ya ripoti hiyo kuwasilishwa kwa Rais, Rais atamuelekeza Waziri kuiwasilisha aripoti hiyo Baraza la Wawakilishi, sasa kimsingi bado naona ripoti itakayopelekwa kwa Waziri ni ya Rais aliyepelekewa na kamisheni, ndio maana rais akamuelekeza Waziri kuwasilisha ile ripoti ya kamisheni kwenye baraza. Kwa hivyo nasema kimsingi hairekebishwi chochote katika *drafting* katika lugha iliyotumika hapo. Lakini nataka ile dhamiri tu isije ikabakia pale kwa mwanasheria mkuu ibakie kwa Waziri hana mamlaka ya kubadilisha katika ripoti ya kamisheni atatuletea kama ilivyopitishwa na Rais na yeye akiwa ni mjumbe anaitoa kamisheni na kuipeleka kule. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilikua namuona Mhe. Ismail Jussa nilipokua nikifanya majumuisho alikua ananisikiliza kwa makini sana, lakini kwenye hili kidogo alitoka sehemu yenyewe nadhani mawazo kidogo yalitoka nje kidogo na hakunisikia vizuri, nakataa sikusema kwamba Waziri atairekebisha. Lakini nikubaliane nae hapo hapo kwamba Waziri kwenye ripoti hana mamlaka ya kuirekebisha, isipokua nilichosema kuna mambo ambayo yamekua *raised* kwenye ripoti unapoipeleka kwa Rais wewe ndie Waziri wa utumishi kuna mambo unaweza kuulizwa, kwa nini yafike mpaka barazani wakati yapo ambayo mnaweza kuyarekebisha, mnapokuja barazani mkaja na ripoti lakini mkaja na majibu, pengine mengine anahitaji mwenyewe Mhe. Rais kwa hivyo ni hayo ambayo anaweza kurekebisha yaani ni mambo ambayo ya kuyafanyia kazi sio ripoti yenyewe.

Naomba kama alinisikia vibaya basi naomba nikubaliane nae kwamba waziri hana uwezo wala hatorekebisha ripoti, bali atayafanyia kazi baadhi ya mambo yamekua *raised* kwenye ripoti ili yawe na majibu hata itakapokuja ripoti hapa barazani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti kwa ufafanuzi huu ambao hivi sasa nimemsikia vizuri bila ya kutoka sio nje ya baraza, nje ya yale aliyoeleza nakubaliana nae tuendelee.

Kifungu cha 5	Kufutwa na kuandikwa upya kifungu cha 29 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 6	Kufutwa na kuandikwa upya kifungu cha 47 pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 7	Marekebisho ya kifungu cha 49 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 8	Marekebisho ya kifungu cha 60 pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 9	Marekebisho ya kifungu cha 65 pamoja na marekebisho yake,
Kifungu cha 10	Kusomwa pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, ilivyokua kamati ya Baraza zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji waheshimiwa wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali ya Mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Mwanasheria MKuu: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kua Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali ya mwaka 2012 kusomwa mara ya pili.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji waheshimiwa wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa wajumbe nikushukuruni kwa kazi nzuri tumemaliza na sasa naakhirisha kikao hiki hadi kesho Saa 3.00 asubuhi.

(Saa 2.15 Usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 03/04/2012 Saa 3.00 asubuhi).